Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Tano – Tarehe 15 Juni, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

Spika (*Mhe. Anne S. Makinda*) Alisoma Dua

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatayo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. DKT. ABDALLAH O. KIGODA - MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:**

Taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi Kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2010 pamoja na tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2010/2011 na Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

**MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA FEDHA - CHRISTINA L. MUGHWAI (K.n.y. MHE. KABWE Z. ZITTO):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Fedha juu ya Hali ya Uchumi wa Taifa na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na Mfumo wa Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 48

### Utekelezaji wa Azma ya Kuhamia Dodoma

**MHE. DAVID M. MALLOLE** aliuliza:

Ile dhamira ya Serikali kuhamia Dodoma imeanza kutekelezwa kwa baadhi ya Ofisi za Serikali kuhamia Dodoma ikiwemo Ofisi Kuu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:-

Je, Serikali inaweza kuwaeleza wananchi wa Dodoma, wafanyabiashara waliowekeza Dodoma kuwa uhamiaji huo utakamilika lini?

**WAZIRI NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa David M. Mallole, Mbunge wa Dodoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimpongeza sana Mheshimiwa Mallole kwa uchungu wa Maendeleo ya Dodoma na kwa kufuatilia sana kwa bidii maendeleo ya wananchi wa jimbo lake hili la Dodoma Mjini.

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali kuhamia Dodoma itakamilika baada ya kukamilika ujenzi wa miundombinu mbalimbali na huduma muhimu zinazohitajika kwa madhumuni hayo. Mahitaji ya raslimali kwa ajili ya kuendeleza miundombinu na huduma hizo ni makubwa, hivyo Serikali inalazimika kutekeleza hatua kwa hatua kwa kadri bajeti inavyoruhusu.

Kwa mfano; mwaka huu wa fedha pekee Serikali itatekeleza miradi yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 30, ambapo fedha hizi zitatoka katika mfuko wetu wenyewe fedha za ndani na pia fedha za Benki ya Dunia. Utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kuboresha miundombinu kwa mwaka huu utaanza mwezi wa nane. Aidha, katika mapitio mapya ya *Master Plan* ya Dodoma. Serikali imetenga eneo jipya lililopo kati ya Ihumwa na Chamwino kwa ajili ya kujenga majengo ya Wizara, Ofisi za Mabalozi na Taasisi nyingine litakalojulikana kama mji wa Serikali. Tayari Taasisi za Kiserikali zipatazo 19 zimepewa viwanja katika maeneo mbalimbali ya mji wa Dodoma kwa ajili ya kujenga ofisi zao. *(Makofi)*

**MHE. DAVID M. MALLOLE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza maswali mafupi sana kama matatu hivi ya nyongeza. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Wanakucheka.

**MHE. DAVID M. MALLOLE:** Mheshimiwa Spika, basi nitauliza mawili.

**SPIKA:** Haya ahsante, nashukuru kwa kunisaidia kulinda Kanuni za Bunge.

**MHE. DAVID M. MALLOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Swali la kwanza kwa vile katika mpango wa miaka mitano haijaonekana mahali popote ambapo

pamezungumziwa kuhusu Maendeleo ya Mji Mkuu wa Dodoma na kwa vile hata katika Bajeti ya mwaka huu sikuweza kubaini mahali popote panapoonesha wazi kabisa kwamba Serikali imedhamiria kiasi gani kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi ya Mji Mkuu wa Dodoma.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza labda kuwafafanulia wananchi wa Mji wa Dodoma kwamba taratibu hizi za ujenzi na uendelezaji wa mji mkuu ambazo amezitamka katika jibu lake zitapata mafungu ya fedha kutoka wapi ili ujenzi huu uweze kutekelezeka kikamilifu?

Swali la pili, tangu *CDA* kuingia hapa mjini Dodoma kwa takriban sasa kama miaka 37 hivi iliyopita limekuweko tatizo kubwa sana la mahusiano mazuri kati ya chombo hiki na wananchi wa Mkoa wa Dodoma. Katika maana kwamba wananchi wa Dodoma na hasa wakazi wenyeji wa mji huu wamekuwa wakinyang'anywa ardhi yao ya asili na hata viwanja na kuendelea kusukumwa pembezoni kabisa mwa mji huu wa Dodoma.

Kila walipofika bado waliambiwa kwamba wazidi kusogea kwenda mbali zaidi. Wakati mwingine mambo haya yamefanyika kwa kubomolewa nyumba zao pasipo kulipwa fidia, ama kulipwa fidia kidogo sana ambazo hazikuweza kukidhi mahitaji ya kujenga nyumba nyingine.

Je, Mheshimiwa Waziri kwa upendo mkubwa sana na kwa maombi ya wananchi wa Dodoma ambao wengi wanapenda kumwita Mjomba, kwa sababu wengi wametoka Uheheni huko Iringa. Anaweza kutamka siku ya leo tamko rasmi la kuwasaidia Wagogo kwamba pale itakapokuwa inaonekana kwamba mji unazidi kwenda pembezoni, moja eneo la nyumba zao na hasa kama zile nyumba hazipitiwi na miundombinu kama vile barabara na kadhalika.........

**SPIKA**: Mheshimiwa sasa unahutubia eeh! Mpaka hatuelewi swali.

**MHE. DAVID M. MALLOLE:** Mheshimiwa Spika, basi nyumba hiyo au nyumba hizo ziweze kubaki bila kubomolewa na vipimwe viwanja sehemu hizo ili wananchi waweze kumiliki viwanja maeneo hayo. Aidha pengine nyumba zingine zinakuwa zina familia mbili, tatu au zaidi ya moja?

**SPIKA:** Aah, Mheshimiwa hiyo sasa ni hotuba umetumia dakika ...(*Kicheko*)

**MHE. DAVID M. MALLOLE:** Pia waweze wananchi kugawiwa viwanja vingine vitatu pasipo malipo yoyote?

**SPIKA:** Tusikilizane, ukifanya hivyo umetumia dakika saba peke yako, sasa na dakika tano inatakiwa zitumike kwa swali zima, Mheshimiwa Waziri wa nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu. Halafu haku-*declare interest.* Mheshimiwa Mallole ni *Board Member* wa *CDA* unatakiwa ku-*declare interest* kwa mujibu wa Kanuni ya 61.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mallole kama ifuatavyo.

Kazi ya ujenzi wa Makao Makuu ni kazi endelevu na ni kazi ambayo inatengewa Bajeti na vipaumbele mbalimbali kila mwaka. Kwa hiyo, kama hakuiona katika mpango wa miaka mitano, ni kwa sababu ni kazi inayoendelea. Na ujenzi wa makao wa makuu haujengwi na Serikali peke yake, ujenzi wa makao makuu ya Dodoma ni shirikishi kama ulivyojitambulisha mwanzo wewe umesemea unawasemea wafanyabiashara na wawekezaji hao vilevile ni sehemu ya mchango wa ujenzi wa makao makuu Dodoma. Lakini kwamba hatukutenga Bajeti pesa nyingi tu hapa nimesema miundombinu peke yake tunaanza kutekeleza hii miradi yenye zaidi ya shilingi milioni 30 katika mji wa Dodoma. Tuna nusu ya miradi ambayo itatekelezwa na Manispaa ya Dodoma na nusu ya miradi itatekelezwa na *CDA.* Kwa hiyo, fedha zipo na shughuli hii inaendelea na wewe unajua tena tuna kazi kubwa ya kupitia *Master Plan* mpya ambayo inaendelea hivi sasa kwa ajili ya kuweka Mji wa Dodoma uwe katika mipango mizuri.

La pili ni kuhusu mahusiano, ni kweli mahusiano yamekuwa mabaya kutokana na baadhi ya watendaji wa *CDA* lakini jambo hili tumekubaliana na Mheshimiwa Mbunge nataka kusisitiza kwamba mimi na yeye tunaweza tukarejesha mahusiano haya maana yake wote tuko kwenye Bodi ya *CDA.*

Tushirikiane, niko tayari kushirikiana na yeye na viongozi wa Dodoma ili kuhakikisha tunarejesha mashirikiano ili kazi za *CDA* zifanywe zile kazi kwa mujibu wa sheria waliyopangiwa kufanya. Hayo yote hayo uliyonayo nafikiri itakuwa ni mchango wa kunisaidia mimi ili nikuwezeshe wewe na wananchi wa Dodoma kukaa Dodoma kwa amani na vilev vile *CDA* na wenyewe wafanye kazi yao kwa mujibu wa Kanuni na sheria. Kwa hiyo, nakuomba tu Mheshimiwa Mallole tushirikiane tutarekebisha hayo maovu ambayo yamekuwa yanatokea.

Na. 49

**Fedha za Mfuko wa Wajasiriamali**

**MHE. ESTHER L. MIDIMU** aliuliza:-

Serikali ilitoa fedha za kukopesha wananchi zijulikanazo kama fedha za JK ili kupambana na umaskini.

(a) Je, ni wananchi wangapi walifaidika na fedha hizo katika Mkoa wa Shinyanga?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kilitolewa kwa wananchi hao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, wajasiriamali wa Mkoa wa Shinyanga walionufaika na fedha za mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuongeza ajira zijulikanazo kama Mabilioni ya JK kwa lengo la kupambana na umaskini ni 3,219.

Mchanganuo wa wajasiriamali hao na fedha walizopata Kiwilaya ni kama ifuatavyo:-

Kahama ni wajasiriamali 1,357 na wamenufaika na sh. Milioni 753.84; Maswa ni wajasiriamali 282 ambao wamenufaika kwa sh. Milioni 378.69. Bariadi wajasiriamali 906 na wamepata sh. Milioni 193.94. Bukombe ni wajasiriamali 102 wamepata sh. Milioni 139.85. Shinyanga Mjini ni wajasiriamali 115 na wamepata sh. Milioni 133.38. Kishapu ni wajasiriamali 309 wamepata sh. Milioni 56.16. Meatu wajasiriamali 88 ambao wamepata sh. Milioni 134.99 na Shinyanga Vijijini wajasiriamali 60 ambao wameepata sh. Milioni 5.50.

(b)Mheshimiwa Spika, kiasi cha fedha kilichotolewa kwa wananchi hao katika awamu ya kwanza 2006/2007 na awamu ya pili mwaka 2007/2008 ni jumla ya shilingi 1,796,350,000/=. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba nimwulize maswali mawili ya nyongeza.

(i) Naomba Waziri anieleze. Je, mfuko huu bado unaendelea?

(ii) Ni namna gani utawafikia wananchi wa hali ya chini hususan wanawake, watanufaikaje na mfuko huo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Kwanza namshukuru sana kwa swali lake la nyongeza na kwamba Mfuko unaendelea na uwezeshaji wa wananchi kwa ujumla unaendelea, na kwa vyovyote vile watakaonufaika zaidi na ambao ndiyo wanatoka jasho zaidi ni wanawake. Kwa hiyo, asiwe na wasiwasi pamoja na wanawake hawa, vijana nao watanufaika na wengine wote ambao watakidhi masharti ya mfuko huo.

**MHE. ESTER BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona, kwa kuwa vijana wengi ndiyo wana tatizo kubwa la kukosa ajira na kwa sababu Mheshimiwa Waziri amesema watakaonufaika na mpango unaokuja ningependa kujua ni kiasi gani

kimetengwa kwa ajili ya vijana na utaratibu gani ambao utatumika ili vijana waweze kunufaika na fedha hizo ukizingatia vijana wengi hawana kazi? Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hakuna kiasi maalum kilichotengwa kwa ajili ya vijana lakini nina hakika kwamba vijana ni wanufaika wa mfuko huu na kwa siku za usoni tutahakikisha kwamba tunatenga kiasi maalum kwa ajili ya vijana ili na wao wajue kwamba wanastahili kupata kiasi gani. Lakini kama takwimu zinavyoonyesha idadi ya watu inaonyesha kwamba walio wengi ni vijana. Kwa hiyo, ni haki yao na wapate kile wanachostahili. Ila nawaomba vijana wa Watanzania wachukue nafasi yao ya nguvu kazi na kwamba wao ndiyo wahimili wa Maendeleo ya nchi yetu na ndiyo watakaolinda uchumi wa nchi yetu.

Sasa namna gani watapata ninaomba vijana kwa sababu wengi nao wana uelewa mkubwa waangalie masharti hayo ni yapi na wajitahidi sana kuyafuata masharti hayo lakini kwa upande wa Serikali kwa sababu ni Wizara ya Uwezeshaji itajitahidi sana kutoa elimu kama namna moja la kuwawezesha.

**SPIKA:** Maswali mengine ya nyongeza, yanatoka kwa wazee, Mheshimiwa Kange Lugola. (*Kicheko*)

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge pia tunapoidhinisha fedha hizi za kuwakopesha wajasiriamali huwa zinatufanya kufika majimboni na kuhamasisha wananchi wanaanzisha vikundi. Na kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi kwamba fedha hizi huwa hazifiki kwa walengwa na hata takwimu alizozisoma hapo Mheshimiwa Waziri inaonekana ni fedha aidha zinaenda Benki au zinaishia Wilayani.

Je, kuna chombo gani ndani ya Wizara husika ambacho huwa kinafanya *monitoring and evaluation* ili kuhakikisha kwamba kweli ile fedha imemfikia mwananchi aliyelengwa Nyemitwebire? Na hili Waheshimiwa Wabunge tusionekane kwamba ni matapeli kuanzisha vikundi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI, NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kangi Lugola kama ifuatavyo.

Kwanza kabisa napenda kumpongeza na nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuhamasisha vikundi vya kiuchumi katika majimbo yao kwa sababu ndiyo kazi kubwa zaidi ya siasa lazima tujenge uchumi.

Sasa kuna malalamiko kweli kwa sababu fedha zenyewe kwanza ni kidogo kwa hivyo kwa vyovyote vile hatuwezi kukosa malalamiko, lakini ameuliza ni chombo gani ndani ya Wizara inayoshughulikia uwezeshaji wa wananchi, napenda kumweleza kwamba kuna Baraza la Uwezeshaji ambalo kazi yake kubwa kwanza ni kuratibu na kuhamisha kwanza wananchi waone kwamba kuna umuhimu wa kuwa na vikundi na katika vikundi hivyo Serikali itakuwa na urahisi wa kuwezesha.

Napenda kulieleza na kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Mheshimiwa Rais ameunda Wizara hii chini ya Waziri Mkuu kwa kutambua kwamba Watanzania wanapaswa washiriki kikamilifu katika kujenga uchumi wao na hiyo ni nia njema ya Serikali inaomba tushirikiane na Waheshimiwa Wabunge waendelee kuhamasisha vikundi wakati huo huo Serikali itajitahidi sana kuona kwamba wanapewa elimu na tunajaribu kufuata njia zile ambazo zitawafikia walengwa hizi fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya kuinua hali ya wananchi wetu walio wengi. *(Makofi)*

Na. 50

**Ahadi ya Ujenzi wa Daraja la Makutupora**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu 2010 Mheshimiwa Rais aliahidi kwa wananchi wa Kata ya Chikuyu kuwa atajenga daraja la Makutupora lililopo katika Kata mpya ya Chikuyu.

Je, lini ujenzi utaanza?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya kujenga daraja la Makutupora ikiwa ni nia njema ya Serikali ya Awamu ya Nne kuwaletea wananchi wake maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya upembuzi yakinifu kufanyika, gharama za ujenzi wa daraja la Makutupora zinakadiriwa kuwa shilingi milioni 500. Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni katika Bajeti ya mwaka 2010/2011 ilituma maombi maalum Wizara ya Fedha na Uchumi ya Shilingi milioni 500, ili kujenga daraja hilo.

Kiasi kilichoidhinishwa na Serikali ni shilingi milioni 300 kutokana na ukomo wa Bajeti ya Serikali. Hadi sasa shilingi milioni 50 zimepokelewa kwa kazi hiyo. Halmashauri inaendelea kufuatilia kiasi cha shilingi milioni 250 ili kutimiza ahadi ya

Mheshimiwa Rais ya kujenga daraja hilo. Katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 zimeombwa shilingi milioni 200 kama maombi maalum kwa kazi hiyo. Kwa hiyo, mara fedha hizo zitakapokuwa zimepatikana ujenzi huo utaanza.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa jibu la msingi limeonyesha ni shilingi 50,000,000 tu zimeshapelekwa Manyoni. Pamoja na jitihada kubwa zilizofanywa na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo Kapteni John Chilligati. Na kwa kuwa Halmashauri imeshindwa kutangaza hata tenda kutokana na kiwango hicho kidogo. Je, Serikali haiwezi kutamka hiyo shilingi 200,000,000 ni kwa muda gani zitafika Manyoni ili tenda iweze kutangazwa?

Swali la pili, kwa kuwa daraja hili ambalo toka limevunjika ni zaidi ya miaka mitatu sasa ambalo ni kiungo kikubwa cha Kata ya Makutupora mpya yenye vijiji vya Dabia, Makutupora na Mbwassa mpaka kwenda Chikuyu kwenye barabara kuu.

Je, kwa kuwa Halmashauri imeomba hizi fedha HAZINA kidharura kutokana na umuhimu wa daraja hili?

Je, Serikali haiwezi kuchukua suala hili kidharura kama vile Halmashauri ilivyoomba kidharura ili wananchi hawa waweze kuondokana na adha hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ilitengewa shilingi 483,000,000 na mpaka tunavyozungumza sasa hivi imepelekewa shilingi 470,000,000, hizo zilizobaki kidogo ndizo zimebaki. Hili daraja analolizungumzia Mheshimiwa Mbunge ninakubaliana naye kabisa ni daraja muhimu sana ndilo linalounganisha ile *Railway Station* iliyoko kule Makutupora kama alivyoeleza. Kuna shule za msingi, kuna ufuta, mahindi na kila kitu. Kwa hiyo, nakubaliana nae kabisa kwamba ni kweli eneo hili na mimi mwenyewe nataka nikuambie Mheshimiwa Spika, kuwa nimefika katika eneo hilo na hilo daraja linalozungumzwa nalifahamu. Sasa kinachosemwa hapa ni kwamba fedha hizi zinatoka wapi?

Fedha ambazo zimekuja, *so far* ni shilingi 50,000,000, kwa maneno mengine shilingi 250,000,000 ambazo zilikuwa zimeahidiwa mpaka sasa hivi hazijatoka. Nimezungumza na Mkurugenzi Mtendaji asubuhi hii na hivi nikitoka hapa nikienda ofisini nakwenda kuzungumza na Mama Kayanda ambaye anahusika na eneo hili, lakini wakati huo huo tutafuatilia kule Hazina kujua kwamba fedha hizi zitapatikanaje. Namwomba Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge, aniamini kwamba ninaposema kuwa nitafuatilia jambo hili nitabeba faili kwa mkono wangu mimi mwenyewe na nitahakikisha kwamba hizo fedha zinapatikana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mimi kusema madaraja yanafanana na Makutupora sipendi.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la Makutupora ndivyo walivyoandika linafanana sana na upande wa Mbozi Magharibi.

Kwa kuwa mwaka 2009 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, alifika katika Kata ya Kamsamba akakubaliana na wazee, Machifu kwa kuingia mkataba wa kimila wa Lifinga kuhakikisha kwamba maana yake pale kuna tatizo la daraja kutoka Kamsamba kwenda kijiji cha Kiliamatundu, upande wa pili wa Kamsamba akaahidi kwamba atalitekeleza.

Je, nikawaeleze nini wananchi wa Kamsamba kuhusiana na daraja hilo ambalo lilikuwa ndani ya ahadi ya Rais ambayo haijatekelezwa mpaka sasa?

**SPIKA:** Hilo suala ni mpya itakuwa ni huruma tu ya Waziri kwamba labda anakujua huko Kamsamba vinginevyo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, Rais akishatoa tamko huwa hatumfuatilii tukamwuliza Rais zile hela ziko wapi? Sisi tunapokea maagizo yale na tunakwenda kutekeleza kama Rais alivyokuwa anaagiza.

Kwa hiyo, nataka nimwambie tu kwamba nitahitaji kwenda kuliangalia jambo hili vizuri kipindi kilichopita mpaka sasa hivi ni miezi 5 tu tumechaguliwa hapa mwezi Desemba ndio tumekuja hapa leo tunazungumza habari ya Bajeti. Naomba Mheshimiwa tuwasiliane twende tu kuangalia nijue ukubwa wa jambo lenyewe, nijue uzito wake, lakini kwetu sisi Rais akishasema hivyo ni maelekezo kwa Wizara. Kwa hiyo, tutakwenda kufanya kama Mheshimiwa Rais mwenyewe alivyoagiza.

**SPIKA:** Tunaendelea haiwezekani kuwa Silinde ikawa madaraja yanafanana haiwezekani.

Na. 51

**Ujenzi wa Barabara ya Nyakanazi-Kidahwe**

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA** aliuliza:-

Wilaya ya Kasulu haina barabara yoyote inayoweza kupitika nyakati zote, na kwamba barabara ya kutoka Nyakanazi hadi Kidahwe iko kwenye mpango wa ujenzi kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM:-

Je, ni lini sasa ujenzi wa barabara hiyo utaanza na kukamilika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, Mbunge wa Kasulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni wa barabara ya Nyakanazi-Kidahwe yenye urefu wa kilometa 296 umekamilika. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 Serikali imepanga kuanza ujenzi wa barabara hii.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara hii ni ya Kidahwe /Nyakanazi ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kuunganisha mkoa wa Kigoma na Tanzania.

**SPIKA**: Ebu Agripina Mkoa wa Kigoma na nani?

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Naomba niendelee Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Hatujakuelewa unaunganisha mkoa wa Kigoma na Tanzania au wapi?

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ninaomba nirudie. Kwa kuwa ujenzi wa barabara hii ya Kidahwe/Nyakanazi ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kuunganisha Mkoa wa Kigoma na Tanzania. *(Makofi)*

Na kwa kuwa ninachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuwa ni Rais wa kwanza wa kutoa ahadi na kuonyesha dhamira ya kweli ya utekelezaji. Naomba niulize swali kama ifuatavyo.

(a) Ili kutekeleza ahadi hiyo ikamilike Waziri yuko tayari kuheshimu na kutekeleza agizo la Rais la kuanza kutekeleza mradi huo kuanzia Kidahwe kuelekea Nyakanazi na siyo Nyakanazi kuelekea Kidahwe?

(b) Kwa kuwa Wilaya ya Kasulu haina barabara hata moja inayopitika kwa muda wote Mheshimiwa Waziri utakuwa tayari kuipandisha hadhi barabara ya Makele, Kitanga ambayo ni barabara muhimu kwa utekelezaji wa mradi wa kilimo kwanza na kwa kuwa Katibu wa Wizara ya Ujenzi ameshafika Kigoma na kushirikiana na Meneja wa *TANROADS* ili kuharakisha kukamilisha ujenzi wa barabara hiyo? Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante, haya nadhani wewe unaelewa vizuri ebu Naibu jibu halafu nitamwita Mheshimiwa Machali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote ningependa tu kuzipokea pongezi zake kwa Mheshimiwa Rais kwa mikono miwili na kumpongeza yeye mwenyewe kwa kuonyesha ukomavu wa kisiasa wa kupongeza pale ambapo inabidi kupongeza. Pamoja na kwamba tunapotosha vijana wetu wanaotusikiliza sasa hivi kwamba Kigoma sio sehemu ya Tanzania. sidhani hiyo ni sahihi kwa sisi wanasiasa ambao ndio *responsible.*

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza la barabara kwamba ianzie Kidahwe badala ya kuanzia Nyakanazi. Hayo ni masuala ya kitaalamu. Hapa kuna suala la utekelezaji wa ahadi ya Rais. Tumeshafanya upembuzi yakinifu, tumeshafanya usanifu wa kina *ditaled design* na hii barabara sasa baada ya kukamilisha kipande cha kutoka Kigoma kuja Kidahwe tunaendelea kukamilisha sasa kipande cha kilomita 296 mpaka Nyakanazi.

Sasa suala la tuanzie katikati, pembeni, kulia, kushoto tukianza hapa kupanga Mheshimiwa Spika tutakuwa tunapotosha dhamira ya Serikali ya ujenzi wa barabara zetu. Tuwaachie wataalam, tuwaachie Wakandarasi ataanzia wapi penye madaraja, tuweze kusema tuanze penye mito tuache wataalamu wanaanzia wapi mradi barabara ya Kidahwe/Nyakanazi inajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili kuhusu barabara ya Makele kwenda Kitanga kwamba ipandishwe daraja, ningemwomba Mheshimiwa Mbunge afuate taratibu ambazo wote wanazifuata hapa za kupandisha hizo barabara ziweze kutufikia na Waziri wa Ujenzi aweze kuchukua hatua stahili.

**SPIKA:**Kwa hiyo, anatakiwa atumie *Roads Board* kule ya kwao. Mheshimiwa Machali nilishamwita.

**MBUNGE FULANI**: Taarifa.

**SPIKA:** Kwenye maswali sipokei taarifa.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa katika Bunge la Aprili, 2011 nilimwuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi juu ya fedha iliyotengwa mwaka jana 2010 kwa mwaka huu ambao unaishia mwezi huu tarehe 30 Juni, 2011. Lakini mpaka leo hii tunapozungumza hakuna kazi yoyote ambayo imeweza kuanza kwa barabara inayoanzia Kidahwe, Kasulu na hatimaye kuelekea Nyakanazi.

Je, Waziri anawaambia nini wakazi wa Mkoa wa Kigoma yaani Kigoma Mjini, Kidahwe, Kasulu kuhusiana na fedha zilizotengwa ili kuanza ujenzi wa barabara ile, lakini mpaka leo haijaeleweka. Nini kauli ya Serikali kuhusiana na fedha zaidi ya shilingi bilioni 6 zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara ile kwa kiwango cha lami?

Badala yake leo tunaona kwenye Bajeti kwamba wametenga fedha za kuanzia Nyakanazi ambayo sio sehemu ya Kigoma. Kuna tatizo gani la kutokuanzia mkoa wa Kigoma hususan Kidahwe wapite Kasulu na kisha waende Nyakanazi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana aliowajibu. Wananchi wa Kigoma na nilitegemea kwamba Mheshimiwa Machali asingeweza kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa ufafanuzi tu ni kweli kabisa kwamba katika Bajeti ya mwaka jana 2010 zilipangwa karibu bilioni 6 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kilomita 50 kutoka Kidahwe hadi Kasulu. Lakini ni kweli pia katika barabara za Kigoma kilomita 36 za kutoka Kigoma hadi Kidahwe zimemalizika kwa kiwango cha lami, kilomita 60 kutoka kwa jimbo la Mheshimiwa Zitto hadi Manyovu nazo zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami na Rais anakwenda kufungua kule tarehe 4 Julai, 2011. Lakini ni kweli pia kutoka Kidahwe hadi Uvinza kilomita 76.6 kuna kandarasi sasa hivi anajenga kwa kiwango cha lami. Lakini pia daraja la Malagarasi limetengewa zaidi ya shilingi bilioni 78 na kandarasi yuko kule kwenye *site* na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa T^anzania,Mheshimniwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, tarehe 5 Julai, 2011 anakwenda kuweka jiwe la msingi la daraja la Malagarasi.

Lakini ni kweli pia katika Bajeti ya mwaka huu katika mipango yetu tumepanga kilomita zote 296 kutoka Kidahwe, Kasulu, Kibondo hadi Nyakanazi nazo tuanze kuzijenga. Sasa suala la kuanzia Nyakanazi, Kasulu, Kibondo wapi yote ile ni Kigoma. Ningeomba Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Machali atuache tufanye kazi, asituchagulie tunaanzia kujenga wapi. Hata ukitaka kunyoa nywele unaweza ukaanzia nyuma, unaweza ukaanzia huku mbele, kitu kikubwa ni kuzinyoa nywele katika kichwa kizima. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Nyakanazi sio Kigoma.

**WAZIRI WA UJENZI:** Lengo letu ni kutengeneza barabara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zitto ufuate utaratibu.

**WAZIRI WA UJENZI**: Kidahwe/Kasulu, Kibondo hadi Nyakanazi. Lakini pia kutengeneza barabara ….

**SPIKA:** Zielezwe kwa utaratibu, sio ku-*shout* tu, tunasikiliza wanavyozungumza. Mheshimiwa Waziri endelea.

**WAZIRI WA UJENZI**: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kama nilivyoeleza lengo letu ni kuhakikisha barabara za Kigoma ambazo ni *Trunk Roads* zote zinajengwa kwa kiwango cha lami, kama ilivyofafanuliwa vizuri kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 ukurasa 72 hadi 82. Mengine wakitaka ufafanuzi wasubiri wakati wa Bajeti tutawatolea ufafanuzi. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

Na. 52

**Mbolea ya Ruzuku Kutowafikia Walengwa**

**MHE. MOSES J. MACHALI** aliuliza:-

Mbolea ya ruzuku haiwafikii wakulima katika muda muafaka, na hata inaposemekana kwamba mbolea hiyo inasafirishwa kwenye vijiji mbalimbali lakini haiwafikiii wakulima:-

Je, kwa nini Serikali isiangalie na kubadilisha mfumo wa kusambaza mbolea hiyo?

Kama Serikali inakubaliana na ushauri huo. Je, ni lini sasa itabadilisha utaratibu huo?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Moses J. machali, Mbunge wa Kasulu Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianza kutumia mfumo wa matumizi ya vocha katika kutoa ruzuku kwa wakulima kuanzia mwaka 2008/2009 hadi sasa (2010/2011). Utaratibu huu ulianza kutumika baada ya utaratibu wa awali wa Serikali kuingia mikataba na makampuni binafsi ya pembejeo kwa ajili ya kusambaza pembejeo zenye ruzuku kwa wakulima kuonekana kuwa na kasoro. Utaratibu wa awali ulikuwa na mapungufu yafuatayo:-

- Pembejeo kutowafikia wakulima walengwa (wakulima wadogo).

- Aina moja ya pembejeo kuwa na bei mbili (yenye ruzuku na bei ya soko) hivyo kiwango cha udanganyifu kuwa kikubwa.

- Hakukuwa na takwimu sahihi za majina ya wakulima kwa kila kijiji wanaopata ruzuku inayojulikana.

- Mbolea ya ruzuku ilisafirishwa kwenda nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa kasoro zilizojitokeza kwa utaratibu wa awali Serikali iliamua ruzuku ya pembejeo kwa mkulima imfikie moja kwa moja kwa kutumia utaratibu wa vocha. Manufaa yaliyopatikana kutokana na utaratibu huu ni kama ifuatavyo:-

- Wakulima walengwa wanapata ruzuku.

- Uelewa wa wakulima kuhusu matumizi ya pembejeo umeongezeka.

- Idadi na majina ya wakulima wanaonufaika inafahamika, mathalani idadi ya wakulima walionufaika ni 700,000 (2008/2009), 1,500,000 (2009/2010), na 2,000,000 (2010/2011).

- Kumekuwepo na ongezeko la uzalishaji wa mazao kwa eneo mathalani:-

  Ongezeko la uzalishaji wa mazao ya chakula hususan mahindi na mpunga umeongezeka kutoka wastani wa tani 0.8 hadi tani 2.5 kwa upande wa mahindi na mpunga kutoka wastani wa 0.6 hadi tani 2.4 kwa ekari.

- Upatikanaji wa pembejeo karibu na wakulima umeongezeka (wastani wa duka moja katika kijiji ambapo utaratibu huu unatumika). Kitaifa umbali wa upatikanaji wa pembejeo kutoka wastani wa kilomita 40 hadi kilomita 16.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo haya kwa Serikali haioni umuhimu wa kubadilisha mfumo huo kwa sasa. Serikali inaamini kuwa utaratibu wa kutoa ruzuku kwa kutumia vocha bado unafaa. Aidha, Serikali itaendelea kuangalia mianya inayosababisha hasara au udanganyifu kwa:-

- Kuimarisha ukaguzi wa ndani.

- Kufanya ukaguzi maalum.

- Kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria wote watakaohusika na udanganyifu.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuweza kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza kwa Waziri.

(a) Kwa kuwa, inaonekana Wabunge nikiwemo mimi Mbunge wa Kigoma Mjini, nimekuwa mfuatiliaji sana wa tatizo la mbolea kutokufika kwa wakati na wananchi wanaonekana kuikosa, naomba kuiuliza Serikali kuna tatizo gani la kutokuwashirikisha Waheshimiwa Wabunge wakashiriki katika mchakato mzima wa usambazaji wa vocha za mbolea mpaka mbolea inapokuja kuwafikia wananchi, na hili ningeomba turejee Ibara ya 63 ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo inaeleza kazi na wajibu wa Bunge na Wabunge ni kuisimamia na kuishauri Serikali ili kusudi tuweze kushirikiana pamoja na viongozi wengine katika kuhakikisha kwamba vocha na mbolea zinafika kwa wakati ili kusudi wakulima wetu waweze kupata mbolea kwa wakati muafaka?

(b)Kwa kuwa, tatizo la *powertiller* Mkoani Kigoma, *powertiller* zimeonekana kutokuweza kulima vizuri kwenye ardhi yetu ya Mkoa wa Kigoma na nimewahi kuuliza

swali hapa Waziri akaahidi kuja kutembelea Mkoa wa Kigoma hususani Wilaya ya Kasulu, ili kusudi tuweze kuzunguka hapa na pale ili kuhakikisha kwamba tunaangalia matatizo ya mbolea ambayo yamejitokeza katika Wilaya ile, ikiwa ni pamoja na suala zima la *Powertiller* ambalo linalalamikiwa na wananchi kwamba haziwasaidii lakini zinaendelea kutolewa.

Nimekuwa na wasiwasi sasa kuona Waziri aliniahidi kufanya ziara mwezi wa tano na hakuja, hii inanipa wasiwasi kwamba inawezekana mpango wa vocha kutowafikia wakulima kwa wakati na mbolea kutokufika kwa wakati, inawezekana ni tatizo la kuanzia Wizarani na Waziri atakuwa analijua ndiyo maana hakuja. Waziri anatamka nini kuhusiana na hili?

**SPIKA**: Mheshimiwa Waziri naomba ujibu kwa kifupi na mwulize maswali ya nyongeza kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO,CHAKULA NA USHIRIKA:**Mheshimiwa Spika, nianze na swali la pili, suala la *powertiller* halina uhusiano moja kwa moja na suala la mbolea, kwa huruma tu nitamjibu kwamba nilikuwa nimemwahidi ndugu yangu Machali kwamba ningekwenda nifanye ziara na pamoja na yeye, lakini kutokana na shughuli nyingi ambazo nilikuwa nazo sikuweza kwenda na tumewasiliana naye tukakubaliana kabisa kwamba tukimaliza nitajitahidi kutimiza ahadi yangu, sasa nashangaa ndugu yangu Machali bado unaleta hili suala ambalo tungeweza kulimaliza kule wenyewe.(*Kicheko*)

Kwa hiyo hili ni suala ambalo ninaamini kabisa tunaweza tukalimaliza mimi na yeye, na siyo yeye tu, na sehemu zingine naendelea kuzitembelea na Waziri anaendelea kuzitembelea. Kwa hiyo kuhakiki, upatikanani wa mbolea, *powertiller* na ubora hilo liko ndani ya uwezo wetu. Naendelea kumhakikishia kwamba nitakwenda, Kigoma ni kwetu pia asiwe na wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hili la kwanza la kushirikisha Wabunge, labda Mheshimiwa Machali ni vizuri tu wakati mwingine mambo mengine tuyaulize hata kabla hatujaja hapa. Wabunge ninyi pia mpo katika Kamati ile, mnaweza kabisa kushiriki katika Kamati ile ya pembejeo na Mwenyekiti ni Mkuu wa Wilaya, hakuna kuzuizi chochote cha ninyi kushiriki. Lakini kama bado mnafikiri mmetengwa basi afadhali mtuambie tuwaeleweshe ni wapi mnaweza mkashiriki na hakuna kuzuizi chochote katika kushiriki hili.

Mheshimiwa Machali nadhani hapa hakuna tatizo lolote, wote tunataka kujenga nyumba moja, tusigombee vitu.

**MHE. DEOGRATIUS A. NTUKUMAZINA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona, naomba niulize swali moja la nyongeza;

Wakati Mheshimiwa Mbunge wa Kigoma Mjini anazungumzia suala la mbolea ya ruzuku kutowafikia wakulima kwa wakati muafaka, wakulima wa Wilaya ya Ngara

hawajawekwa kwenye utaratibu wa mbolea ya ruzuku. Namwomba Waziri awaeleze wakulima wa Ngara ni lini watawekwa kwenye utaratibu wa mbolea ya ruzuku?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze tena Mheshimiwa Ntukamazina kwa jinsi alivyofuatilia mpaka nikamaliza ziara na hatimaye kwa bahati mbaya nikachelewa kufika Kasulu, lakini nimetokea kwake ndiyo sababu nikachelewa ikabidi nikimbilie huku.

Pamoja na hayo nataka nimhakikisie Mheshimiwa Ntukamazina kwamba wakati nilipotembelea Wilaya yake suala hili lilijitokeza na liliahidi kwamba nitakaporudi Wizarani tutakwenda kushirikiana na wenzangu ili tuangalie utaratibu wa Wilaya au maeneo ambayo bado hayajafikiwa tuangalie Ngara kama itafikiwa, kwa sababu yapo maeneo mbalimbali hata Tabora Mjini nao wanadai na maeneo kadhaa bado wanadai.

Nataka nikuhakikishie kwamba nitakaporudi, tutaangalia pamoja na wenzangu pale Wizarani ni maeneo gani ambayo tutayafikia katika msimu huu ujao. Kwa vyovyote vile haiwezekani kuwafikia Watanzania wote kwa mara moja. Hili nina hakika kabisa hatutaliweza, lakini lazima tutachagua maeneo.

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Fedha Mheshimiwa Said Amour Arfi, naona tumetumia zaidi ya dakika arobaini hapo naomba sana tuangalie muda, bado nina maswali sita dakika kumi.

Na. 53

**Kero la Suala la Mirathi na Mafao ya Wastaafu**

**MHE. ANNA M. J. MALLAC (K.n.y. MHE. SAID A. ARFI)** aliuliza:-

Suala la upatikanaji wa mafao ya wastaafu na mambo yanayohusiana na mirathi kwa watumishi waliokufa kazini yamekuwa ni kero kubwa sana:-

Je, ni lini Serikali itaondoa kero hizi za muda mrefu ili wastaafu walipwe mafao yao mara wanapostaafu na mirathi kutolewa kwa wakati bila usumbufu kama ambao wanaoupata sasa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa anavyosema Mheshimiwa Mbunge, kwamba ucheleweshaji wa kupata mafao ya wastaafu na mambo yanayohusiana na mirathi kwa watumishi waliokufa kazini umekuwa ni mzigo usio wa lazima kwa wastaafu.

Mheshimiwa Spika, mafao ya wastaafu na mirathi ya Watumishi waliokufa kazini wa Serikali Kuu na wale wa Serikali za Mitaa yanasimamiwa na Mifuko mitano ambayo

ni: Mfuko wa pensheni kwa Watumishi wa Umma *(PSPF),* mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Serikali za Mitaa *(LAPF),* mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma *(PPF*), Mfuko wa Akiba ya Watumishi wa Serikali *(GEPF)* na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF).*

Mheshimiwa Spika, Mifuko hii ni mahsusi kwa malipo ya mafao na mirathi kwa wastaafu na watumishi waliokufa kazini kulingana na stahili zao. Mifuko hii ya pensheni ndiyo inayowajibika kutoa malipo stahili na kwa wakati. Mchakato wa malipo huanzia kwa mwajiri ambaye huandaa nyaraka za madai ya malipo na kuziwasilisha kwenye Mfuko husika. Mifuko huzipitia nyaraka na kukokotoa kiasi cha malipo na kisha kupeleka hundi kwa walengwa.

Mheshimiwa Spika, ucheleweshaji wa maandalizi ya mafao pamoja na mambo mengine unatokana na utunzaji wa kumbukumbu na mawasiliano hafifu miongomi mwa wadau. Hii inajumuisha malumbano ya kifamilia kuhusu uteuzi wa msimamizi wa mirathi husika.

Mheshimiwa Spika, endapo kumbukumbu za mstaafu zitakuwa kamilifu na michango yote itakuwa ikiwasilishwa katika Mfuko kama inavyotakiwa, mstaafu ataweza kupokea malipo yake ya kustaafu mara tu anapostaafu bila ya usumbufu usio wa lazima.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mirathi suala la utimilifu wa kumbukumbu zote za utumishi, pia makubaliano mahsusi ya kifamilia kuhusu uteuzi wa msimamizi wa mirathi ni muhimu sana. Kwa hiyo, endapo kutakuwa na kumbukumu zinazotakiwa pia na nyaraka zote za mirathi zitakuwa zimewasilishwa kama inavyotakiwa, warithi wataweza kulipwa mirathi yao kwa haraka bila ya usumbufu wowote. *(Makofi)*

**MHE. ANNA M. J. MALLAC:**Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Waziri nina swali la nyongeza.

Kwa kuwa, upatikanaji wa mirathi umekuwa wa kusuasua kwa baadhi ya familia, mpaka hivi leo kuna familia nyingi ambazo zinadai mirathi yao bila mafanikio mpaka imepelekea watoto kuacha shule kwa kukosa huduma.

Je, Serikali inalionaje hili ili kuhakikisha familia hizi zinapata haki zao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba mafao na mirathi inafikia walengwa kwa wakati, kuna matatizo mengi ambayo hujitokeza ambayo yapo nje ya Serikali. Pamoja na hivyo Mheshimiwa Mbunge nakushauri kwamba kama unawafahamu hawa ambao wana matatizo hususan ambao umewakusudia naomba tuwasiliane tuone tunaweza tukawasaidia vipi. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, bado wapo warithi ambao sasa ni muda mrefu wamekuwa wakizungushwa katika kupata haki wanazostahiki kutokana na marehemu ambaye alikuwa ni mzee wao.

Je, Waziri, endapo itathibitishwa kwamba Marehemu na vielelezo vyake vyote vimepatikana, unatoa kauli gani kwa warithi juu ya kuwapatia haki hizi kwa haraka na bila kuwageresha?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Mbunge aniletee hizo nyaraka ili nami nisaidie kulimaliza.

Na. 54

**Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto**

**MHE. AMINA N. MAKILAGI** aliuliza:-

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ni Wizara mtambuka kwa Maendeleo ya Watanzania lakini Wizara hiyo imekuwa ikitengewa fedha kidogo licha ya Wabunge wengi wanaochangia hoja za Wizara hiyo wakati wa Bajeti kuomba kuongeza Bajeti ya Wizara hiyo:-

Je, Serikali katika bajeti ya mwaka 2011/2012 itaongeza Bajeti ya Wizara hiyo kwa asilimia ngapi ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Nassor Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ni Wizara mtambuka kwa Maendeleo ya Watanzania. Aidha, kila Wizara, Mikoa na Halmashauri hutengewa fedha kulingana na majukumu ya msingi waliyopewa kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto katika mwaka wa fedha 2009/2010 ilitengewa kiasi cha shilingi Bilioni 17.1 na katika mwaka wa fedha 2010/2011 ilitengewa kiasi cha shilingi Bilioni 19.9 ikiwa ni ongezeko la asilimia 16.4. Mwaka wa fedha 2011/2012 imetengewa kiasi cha shilingi Bilioni 16.3 ikiwa ni pungufu ya kiasi cha shilingi Bilioni 3.6 sawa na asilimia 18 ikilinganishwa na Bajeti ya mwaka 2010/2011. Kati ya fedha hzi shilingi Bilioni 11.402 ni kwa matumizi mengineyo *(OC)* na shilingi Bilioni 4.853 ni kwa ajili ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, upungufu huu pamoja na mambo mengine, umechangiwa na Bajeti ya watumishi wapya wanaotarajiwa kuajiriwa katika mwaka wa fedha 2011/2012

kuhamishiwa kwenye Fungu 21 (HAZINA) ili kudhbiti malipo ya watumishi hewa wakati wa ajira mpya. Fedha hizi zitakuwa zinarejeshwa kwenye fungu husika kulingana na idadi halisi ya watumishi watakaoajiriwa na kuingizwa kwenye "*Payroll*" ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo pamoja na ufinyu wa Bajeti ya Serikali kwa ujumla, fedha zimetengwa kwenye Wizara na Halmashauri mbalimbali kwa ajili ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa vile mambo ya Maendeleo ya Jinsia ni mtambuka.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa bado kuna umuhimu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kutengewa fedha za kutosha na rasilimali watu ili iweze kufanya kazi zake kikamilifu? *(Makofi)*

(b) Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya Halmashauri za Wilaya na Halmashauri za Miji na Manispaa ambazo zimekuwa hazitengi fedha asilimia kumi ya Mfuko wa Maendeleo ya wanawake na Vijana kwa ajili ya kuimarisha vikundi vya uchumi vya kijamii?(*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Spika, suala la rasilimali fedha kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, Wizara imetengewa bilioni 16.

Pia nikasema kuna fedha ambazo zimetengwa kwenye Wizara tofauti za Serikali pamoja na Halmashauri nazo zinalenga kwenye maeneo ya jinsia na vijana, nina mfano wa shilingi bilioni 32.2 ambazo zimetengwa kwa ajili ya kazi za maendeleo kwenye Wizara tofauti nilizozitaja. Wizara ya Elimu, Wizara ya Afya na Wizara nyingine pamoja na Wizara ya Kazi. Kwa hiyo, suala la rasilimali fedha nafikiri limechukuliwa hatua za kufaa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la rasilimaliwatu, Wizara hii imeomba na kutengewa nafasi za ajira 252 ambazo zitagharimu jumla ya shilingi milioni 1.5. Kwa hiyo, kuna jumla ya wafanyakazi kama 252 wanaweza wakaajiri katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili kauli ya Serikali kwa sasa ni kuzikumbusha Halmashauri kwamba kuna agizo la kuwataka watoe asilimia kumi kwa ajili ya maendeleo ya vijana na wanawake. Hili ni muhimu kwa sababu hizi ni sehemu mbili au sekta na makundi ambayo ni muhimu katika maendeleo ya nchi yetu hasa uchumi. Kwa hiyo, ni vizuri kutekeleza hilo.

Lakini niwaombe pia Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ni sehemu ya uendeshaji wa Halmashauri hizi kwamba wawe mabalozi wetu kukumbushia kwenye Halmashauri kwamba kuna agizo hili na vizuri tukalitekeleza. (*Makofi*)

Na. 55

**Chuo cha Maendeleo ya Jamii Kihinga**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA** aliuliza:-

Chuo cha Maendeleo ya Jamii Kihinga hakifanyi kazi iliyokusudiwa kwa sababu kimetelekezwa na kimegeuzwa kuwa kumbi za mikutano, starehe, sehemu ya kuchomea matofali na kilimo:-

Je, kwa nini Serikali isilikubali ombi la Mkoa wa Kigoma la kukibadili Chuo hicho na kuwa Chuo cha Ualimu?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, Kihinga siyo Chuo cha Maendeleo ya Jamii bali ni Chuo cha Maendeleo ya Wananchi *FDC.*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, vilianzishwa mwaka 1975 kwa madhumuni ya kuwapatia Wananchi ujuzi, maarifa na stadi, zitakazowawezesha kujiajiri na kujiongezea kipato na kuondokana na umaskini. Mafunzo haya hutolewa kwa muda mrefu, mfupi au kozi nje ya chuo, kulingana na mahitaji ya jamii husika. Vyuo hivi vina umuhimu mkubwa zaidi kwa sasa kwani ni vyuo pekee vinavyotoa stadi kwa Wananchi wote bila kujali sifa za kielimu za mwombaji.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kihinga, kinatekeleza majukumu yaliyokusudiwa ya kutoa maarifa, ujuzi na stadi mbalimbali kwa Wananchi. Mafunzo ya fani yanayotolewa katika chuo hiki ni pamoja na ufundi wa magari, ushonaji, useremala, uashi, kilimo na ufugaji. Kwa kuzingatia taarifa zilizopo Wizarani, katika Mwaka wa Fedha wa 2009/2010, jumla ya Wananchi 159 walipata mafunzo hayo na mwaka huu wa 2010/2011, Chuo kina Wanachuo 68 wa kozi ndefu katika fani za ufundi wa magari, ushonaji, uashi na useremala. Kozi fupi zilizoendeshwa tangu mwezi Januari, 2011 zimewanufaisha jumla ya Wananchi 165 ambapo mafunzo nje ya Chuo yalitolewa kwa Wanachuo 29.

Mheshimiwa Spika, Vyuo hivi ni Vituo vya Maendeleo ya Jamii na kwa yale maeneo ambayo hayana Majumba ya Maendeleo, Vyuo hivi hutumika kama Majumba ya

Maendeleo, bila kuathiri shughuli ya msingi ya utoaji mafunzo. Shughuli hizo ni pamoja na kuendeshea mikutano na semina mbalimbali za jamii.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakusudia kuendelea kuviboresha vyuo hivi ili kuviwezesha kudahili Wananchi wengi zaidi hususan vijana na kutoa maarifa na stadi mbalimbali zitakazowawezesha kujiajiri/kuajiriwa na kukamilifu katika shughuli za uzalishaji mali.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, wakati ninaandika swali hili nilikuwa na uhakika na ninachokiandika. Hata kama ni Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, lakini hakifanyi kazi iliyokusudiwa na wala hakitengewi fedha ndiyo maana Mkuu wa Chuo pale amekuwa akiamua kukodisha maeneo watu waweze kulima na kuchoma matofali. Kikao cha RCC cha Mkoa wa Kigoma kikaamua kuomba Chuo hiki kibadilishwe kuwa Chuo cha Ualimu ili kukidhi haja ya matatizo ya uhaba wa walimu katika Mkoa wa Kigoma.

Je, kama Serikali haiwezi kukibadilisha Chuo hiki ili tukidhi haja ya uhaba wa Walimu kwa Mkoa wa Kigoma; kwa nini haikipatii fedha ili kiweze kufanya kazi iliyokusudiwa na tayari tunacho Chuo cha VETA ambacho Wanafunzi wanaweza kwenda kujifunza ushonaji na useremala na kile Chuo kikafanya kazi nyingine kwa sababu hakipatiwi fedha ya kuweza kukiendeleza? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ninaomba ujibu kwa kifupi sana muda wenyewe umeshakwisha.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kusisitiza kwamba, Kihinga ni Chuo cha Maendeleo ya Wananchi na kuna tofauti ya msingi sana kati ya Chuo cha Maendeleo ya Jamii, kwa sababu wao wanatoa Taaluma za Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vinatoa mafunzo, stadi za maisha na maarifa mbalimbali kwa jamii husika.

Mheshimiwa Spika, Serikali haijakitelekeza Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Kihenga kwa sababu kwa mwaka wa fedha huu tayari tumetuma shilingi milioni 4.6 kwa ajili ya uendeshaji wa Chuo. Katika mwaka huu wa fedha pia tumeweza kununua matrekta yanayokokotwa na ng’ombe, *power tiller*, mashine za kufyatulia matofali na mashine za kutotoa vifaranga.

Mheshimiwa Spika, huwezi kutelekeza kitu kama utakuwa hukitazami. Ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, tuna changamoto nyingi katika Vyuo vyetu vya Maendeleo ya Wananchi ambavyo viko 55, uchakavu wa miundombinu na majengo.

Mheshimiwa Spika, lakini ni jana tu Bunge lako Tukufu limepitisha Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge asome Mpango ule katika *chapter three, strategic intervention,* utaona kwamba, Serikali inakusudia kuviboresha vyuo hivi ili kuweza kudahili vijana wengi zaidi hasa wanaomaliza darasa la

saba na kukosa nafasi za kuendelea VETA au Sekondari ili wapate stadi za maisha na washiriki katika shughuli za uzalishaji mali. Ninakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zitto, *time*.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, Chuo hiki kiko katika jimbo langu, kwa hiyo, ninaomba unipe fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

**SPIKA:** Siyo sababu, ninaomba ukae.

Na. 56

**Shamba la Mitamba Kibaha**

**MHE. SILVESTRY F. KOKA** aliuliza:-

Wananchi wa Halmashauri ya Kibaha waliomba kupewa eneo la shamba la Mitamba kwa ajili ya kupanua makazi yao na biashara katika Mji mpya wa Kibaha bila mafanikio:-

(a) Je, Serikali ina mpango na eneo hilo ambalo sasa hivi liko mjini?

(b) Je, ni kwa nini baadhi ya Wananchi wameruhusiwa kuweka makazi kwenye eneo hilo na wengine wamekataliwa na kufukuzwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, lililokuwa Shamba la Mitamba Kibaha lilikuwa linazalisha Mitamba kwa ajili ya wafugaji wa ng'ombe wa maziwa nchini. Kutokana na eneo hilo kuzungukwa na makazi na udogo wa eneo kwa ufugaji mkubwa, Serikali ilibadilisha matumizi ya eneo hilo na sasa matumizi yake ni kwa ajili ya kuwa kituo cha uzalishaji na usambazaji wa kimiminika cha *Nitrogen* (*Liquid Nitrogen),* uzalishaji wa chanjo, pamoja na uchunguzi wa magonjwa ya mifugo katika Kanda ya Mashariki kwa lengo la kupeleka huduma karibu na wafugaji.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, kuna Wananchi ambao waliingia shambani na kujichukulia maeneo kabla ya shamba hilo kupimwa. Hata hivyo, kwa kutambua mahitaji ya kulitumia eneo hilo kwa makazi na matumizi mengine, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ilipima upya shamba hilo na kubakiza eneo la ekari 1,037 kwa shughuli za Serikali nilizozitaja hapo juu.

Eneo lililobaki lenye ukubwa wa ekari 2,963 litatolewa kwa Halmashauri ya Mji wa Kibaha kwa matumizi ya makazi na shughuli zingine za maendeleo. Hivyo, Wananchi ambao makazi yao yalikuwa ndani ya eneo lililotajwa, watapaswa kusubiri kumilikishwa maeneo hayo baada ya upimaji wa maeneo husika utakaofanywa kwa utaratibu wa Halmashauri ya Kibaha.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa wito kwa Wananchi waliojenga ndani ya eneo lililopimwa la ekari 1,037 kwamba, eneo hili litatumika sasa kwa shughuli nilizozitaja na ninawaomba wajaribu kuondoka na kutafuta maeneo sehemu nyingine. Aidha, ninaomba nitumie fursa hii kuomba Halmashauri ya Mji wa Kibaha, ione uwezekano wa kuwapatia Wananchi hao maeneo mengine.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuona kwamba, kuna umuhimu wa kutoa zile ekari 2,963 kwa ajili ya maendeleo wa Mji wa Kibaha. Kwa kuwa eneo lililobaki lina ekari 1,037 tayari liko ndani ya Mji Mpya wa Kibaha na linazungukwa na makazi ya watu na kama alivyokiri, tayari lilikwishavamiwa na baadhi ya Wananchi. Kwa kuwa liko kandokando ya kitovu cha Mji wa Kibaha, Mji ambao tunauona sasa kama ni *next destination* kutoka Dar es Salaam.

(a) Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kutoa eneo hili lote kwa ajili ya Maendeleo ya Mji wa Kibaha ili eneo hili liweze kuwa makazi na shughuli zingine za mji?

(b) Je, ni lini Serikali itatoa eneo nililolitaja la ekari 2,963 kwa Halmashauri ya Mji kwa Jimbo la Kibaha? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Silvestry Koka, Mbunge wa Kibaha, kama ifuatavyo:-

(a) Moja ya eneo hilo tayari limeshaendelezwa na Wizara, kuna miundombinu na kuna mipango inayoathiri taratibu zetu za kitaifa kuweza kujitosheleza kwa chanjo ya mifugo. Pia kuhakikisha kwamba, Mikoa ya Morogoro, Pwani na Dar es Salaam, wafugaji wanaokaa katika maeneo hayo waweze kupata huduma hii ya kuwa na kituo cha uchunguzi wa magonjwa kwa mifugo yao.

Kwa hiyo, ninaomba kwamba, pamoja na kuwa eneo hilo liko hapo, tayari mipango ipo, limeendelezwa na hivyo maadamu robo tatu ya shamba zima zimetolewa Kibaha na robo moja ndiyo Wizara imebaki nayo; ningewaomba Halmashauri ya Kibaha, Mbunge akiwepo kwamba, kinachofanyika kule ni kitu muhimu kitaifa, kwa hiyo, waachie Wizara iendelee na shughuli zilizopangwa katika eneo hilo.

(b) Kuhusiana na kwamba ni lini eneo lingine litakabidhiwa, ningemwomba Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa kutumia Halmashauri yake ya Kibaha, waharakishe tu utaratibu wa kuketi pamoja na Wizara, maana taratibu kwa upande wa Wizara

zimekamilika na hivyo Halmashauri ya Kibaha ikijipanga hata kesho hakutakuwepo na ugumu wa kukabidhiwa eneo hilo ambalo nimesema ni ekari 2,963. Ninashukuru.

Na. 57

**Uvuvi wa Bahari Kuu**

**MHE. THUWAYBA IDRISA MUHAMED** aliuliza:-

Tanzania ina Bahari Kuu yenye rasilimali nyingi ikiwemo samaki wakubwa ambao siyo rahisi kuvuliwa na wavuvi wadogo wadogo na hivyo uvuvi wa Bahari Kuu hufanywa na meli kubwa kutoka nje ya nchi:-

(a) Je, meli hizo za uvuvi huvua tani ngapi kwa siku?

(b) Je, Serikali inafaidika na uvuvi huo?

(c) Je, malipo ya leseni ya uvuvi wa Bahari Kuu ni kiasi gani kwa sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhamed, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, meli za uvuvi katika Bahari Kuu hulenga kuvua samaki aina ya jodari na samaki wengine wa aina hiyo. Upatikanaji wa samaki hao unategemea hali ya hewa, joto la maji, chakula, pamoja na mabadiliko ya tabia nchi. Katika maji ya Tanzania, samaki hao hupatikana kwa wingi kuanzia mwezi Julai hadi Novemba *(peak season).* Katika kipindi hicho wastani wa tani mbili hadi tani tano za samaki hupatikana kwa meli kwa siku. Aidha, kuanzia mwezi Desemba hadi Juni *(low season),* katika kipindi hicho wastani wa nusu tani za samaki hupatikana kwa meli kwa siku.

(b) Mheshimiwa Spika, uvuvi wa Bahari Kuu huliingizia Serikali mapato kutokana na ada za leseni za uvuvi na usajili wa meli zinazovua kwenye eneo husika. Katika mwaka 2010/2011, jumla ya meli 71 za uvuvi zilisajiliwa na kukatiwa leseni za kuvua katika Bahari Kuu. Mapato yaliyopatikana ni jumla ya Dola za Kimarekani 2,074,400. Hata hivyo, katika miaka ya hivi karibuni, uvuvi katika Bahari Kuu umeanza kuathiri kutokana na uharamia katika Bahari ya Hindi. Inakisiwa kuwa, bila kuwa na tishio hili la uharamia, jumla ya meli kati ya 120 na 150 zingesajiliwa na kukatiwa leseni ya kuvua katika Bahari Kuu na hivyo kiasi cha mapato ambacho tungelipata kama Taifa, ingekuwa ni mara mbili ya kiasi tulichopata hivi sasa.

(c) Mheshimiwa Spika, malipo ya leseni ya uvuvi kwenye Bahari Kuu hutofautiana kulingana na aina ya uvuvi, muda wa leseni na mahali inakotoka meli. Mfano, meli ya kigeni inayovua kwa uvuvi uitwao *purse seining* inatozwa ada ya leseni

ya Dola za Kimarekani 12,000 kwa miezi mitatu au 35,000 kwa mwaka na usajili wa meli ya kigeni unakuwa ni Dola za Kimarekani 2,000 kwa mwaka. Meli za Kitanzania zinazofanya kazi hiyo hiyo hutozwa Dola za Kimarekani 4,500 kwa miezi mitatu na Dola 18,000 kwa mwaka na usajili wa meli ya Kitanzania ni Dola za Kimarekani 300 kwa mwaka.

**MHE. THUWAYBA IDRISA MUHAMED:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti meli za nje zinazovua samaki ambazo hazina vibali?

(b) Je, Serikali itawasaidiaje wazawa na wavuvi wadogo wadogo ambao wanahitaji kuvua katika Bahari Kuu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Thuwayba Muhamed, ameuliza vizuri sana maswali ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Moja, hivi sasa kuanzia mwaka jana kumekuwepo na Mamlaka ya Uvuvi katika Bahari Kuu na Mkurugenzi wa Mamlaka tayari amechaguliwa, Ofisi yake iko Zanzibar na amekuwa akiratibu uthibiti wa anga kwa kutumia KMKM, lakini pia polisi na baadhi ya wanajeshi hasa wale wa majini, wajaribu kufuatia meli zinazovua. Katika eneo hilo la udhibiti pia kuna chombo maalum kilichofungwa katika ofisi Zanzibar, kinachoweza ku-*monitor* na kuona meli zinapoingia katika maeneo ya maji yetu na kuvua na chombo hicho kinafanya kazi. Teknolojia iliyopo ili iweze kufanya kazi, lazima meli inayovua iwe na chombo kama hicho. Mara nyingine kama hakipo siyo rahisi kuona. Kwa hiyo, ni eneo ambalo tunahitaji na tumejipanga Kiwizara na kama Serikali kuweza kuboresha eneo hilo la udhibiti.

Kuhusu kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo, kuna mipango kama mlivyoona juzi tukijadili hapa, kuna eneo zima kwa ajili ya uvuvi. Katika mifuko ya kuwezesha wavuvi wadogo wadogo na wao wana fursa sawa na watu wanaofanya shughuli nyingine kuweza kupata mikopo mle na kununua vyombo hasa vya kisasa watakavyotumia kwa ajili ya uvuvi.

Na. 58

**Fedha za Uhamisho wa Askari Polisi – Bahi**

**MHE. OMARY AHMAD BADWEL** aliuliza:-

Askari Polisi wa Wilaya ya Bahi walishahamia Makao Makuu ya Wilaya Mjini Bahi na kwamba fedha zao za uhamisho zilishatolewa na Serikali lakini mpaka sasa hawajalipwa:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kuwalipa askari polisi hao fedha zao kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha?

(b) Je, ikiwa fedha hizo hazikutolewa Serikali inaahidi kuwa katika Bajeti ya Mwaka 2011/2012 fedha hizo zitatengwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Omary Ahmad Badwel, Mbunge wa Bahi, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali iko tayari kulipa madeni ya askari hao kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha. Labda nirudie kutamka kwamba, Wizara yangu imekusudia kulipa madeni hayo kabla ya mwaka huu wa fedha kumalizika tarehe 30 Juni, 2011, kama alivyoeleza Waziri wa Fedha tarehe 07 Juni, 2011 katika Bunge lako Tukufu wakati alipokuwa akitoa maelezo ya ziada kwa swali la nyongeza lililoulizwa na Mheshimiwa Mohammad Ibrahim Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe kwamba, haya madeni yote yatakuwa yamelipwa mwisho wa mwezi huu, yaani mwezi wa sita.

**MHE. OMARY AHMAD BADWEL:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili pamoja na majibu mazuri na ya uhakika ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri na ya uhakika ya Mheshimiwa Naibu Waziri; Watumishi ambao Mheshimiwa Waziri ameahidi hivi punde kuwalipa malipo yao ya kuhamia Bahi wako 56 na tayari wote wameshahamia Bahi, lakini kama tunavyojua Wilaya ya Bahi ni mpya na Kijiji cha Bahi kimepandishwa hadhi hivi karibuni kuwa Makao Makuu ya Wilaya; na tunalo tatizo kubwa la makazi ya Watumishi; hivyo imewalazimu askari hao 14 kukaa katika nyumba moja kati ya nyumba nne zilizoko pale katika Wilaya ya Bahi:-

(i) Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuniahidi katika bajeti hii kwa uhakika kama alivyoahidi habari ya malipo yao kwamba watatupatia angalau nyumba chache katika Wilaya ya Bahi ili askari hao wapunguze matatizo ya makazi?

(ii) Kwa kuwa Wilaya ya Bahi kabla haijajenga kituo kipya cha polisi, tulikuwa na kituo cha zamani ambacho kilijengwa kabla ya uhuru katika Kijiji cha Kigwe. Kituo kile kimechakaa sana, lakini licha ya kuchakaa sana askari wanafanyia kazi humo, familia zao zinahishi humo na mahabusu wanawekwa humo. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kufuatana na mimi siku moja akajionee adha wanayoipata askari wale mpaka wanashindwa kutekeleza majukumu yao ya kila siku?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninaomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Omary Ahmad Badwel, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu nyumba, ninadhani hili tumekuwa tunalizungumzia sana; ni suala ambalo tunalitazama Kitaifa, yaani kinchi nzima na niseme tu kwamba, tunaweka Programu ambayo imekwishapitishwa katika Baraza la Mawaziri, Programu ya Maboresho ya Jeshi la Polisi. Kwa hiyo, siwezi nikamwahidi kwamba, hizo nyumba zitajengwa zote kwa Askari 56, lakini kile ambacho nimepanga kwamba tutafanya, tutaweza kukitekeleza.

Pili, kuhusu kutembelea hicho kituo, nimwambie kwamba, niliwahi kutembelea hicho kituo na nilikitembelea mwaka jana nilipofanya ziara pale na kutazama mahitaji yao na kutazama jengo la polisi ambalo tumeliweka pale. Ninamhakikishia kwamba, niko tayari, kwa kuwa tuko hapa na Bahi siyo mbali, kwa hiyo, tutaweza kupanga na tukaenda tena tuyatazame hayo matatizo ya Askari wetu.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, hatuwezi kuwa tunajibu maswali siku nzima na muda wetu ni saa moja tu kwa maswali kumi, hata hivyo tumechukua muda wa kuwasilisha zile taarifa ndiyo sababu tuko hapa.

Waheshimiwa Wabunge, nina wageni kwenye *Speaker's Gallery;* wa kwanza kabisa ni Bi. Shida Salum, huyu ni Mama Mzazi wa Mheshimiwa Zitto Kabwe, pia ni Mwenyekiti wa CHAWATA Tanzania, halafu ni dada yangu na amenikabidhi huyu Zitto Kabwe anapofanya ujeuri hapa simwelewi kabisa, ahsante. Ninaomba mumpe pongezi Mama Zitto Kabwe. *(Makofi*)

Tuna Ndugu Lulu Mangele, huyu ni Meneja Mahusiano ya PPF, amekuja hapa kwa lengo la kujaribu kufadhili shughuli za michezo ya Wabunge. Kwa hiyo, mazungumzo yataendelea, ninaomba usimame Bi. Lulu Magele, ahsante sana kwa kutoa *support* kwa *Bunge Sports Club,* tunashukuru sana. (*Makofi*)

Wengine wanatambulishwa tu kwa ajili ya umuhimu wao, yuko Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CHADEMA, Ndugu Henche Suguta na wenzie, ninaomba na wasimame walipo na wenzio; ahsante. *(Makofi)*

Matangazo ya kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa James Lembeli, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo tarehe 15 Juni, 2011, saa saba mchana, kutakuwa na mkutano, Chumba Namba 219. Ninadhani tuseme baada ya kikao chetu kitakachofanyika Ukumbi wa Msekwa, ndiyo Wajumbe wa Kamati hiyo watakutana. Tumekubaliana kwamba, baada ya kuwasilisha maelezo ya Kamati na maelezo ya Kambi ya Upinzani, tutaahirisha ili tukafanye kazi nyingine. Kwa hiyo, baada ya kikao hicho, Kamati ya Mazingira mtakutana Chumba Namba 219.

Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, Mheshimiwa January Makamba, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba, leo nao watakutana Chumba Namba 231, baada ya Mkutano huu kukamilika, alisema saa saba, lakini ninasema baada ya kikao kile kukamilika. Halafu tunatangaziwa na Ofisi kwamba, Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2011, utakuwa kwenye *pigeon hole*, baada ya kusomwa hapa kwa mara ya kwanza baada ya tangazo hili. Kwa hiyo, ni vizuri mkasome, kwa sababu utakuwa na *implications* nyingi sana za kodi mbalimbali ambazo Serikali itatangaza.

Mtaalamu wa *Computer* hapa Bungeni anasema kwamba, tunatarajia kufunga vitambulisho vya muda, *acess card,* mwishoni mwa wiki hii, kwa mantiki hiyo vitambulisho vya muda havitatumika tena, tunaomba virudishwe ili vitolewe vitambulisho vya kudumu. Hivyo, tunapenda kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote ambao hawajapiga picha kwa ajili ya vitambulisho, wafike ghorofa ya kwanza, Chumba Namba 128.

Zoezi hili ni la muda mfupi; hivyo, wote ambao hamkupiga picha, mnaombwa mkapige kwa sababu baada ya wiki ijayo kama huna hii *acess card* wewe utakuwa nje, labda ujibandikize kwa mwenzio, sasa uhuru wako utakuwa umekwisha; nenda ukapige picha ili uweze kupata kitambulisho cha kukuwezesha kuingia na kutambuliwa hapa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, mwisho wa matangazo. Katibu.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2011
***(The Finance Bill, 2011)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA**: Ahsante. Kama nilivyosema, Miswada yenyewe itagawiwa kwenye *pigeon hole,* Waheshimiwa Wabunge mkasome kwa sababu kazi yote hii inategemea huo Muswada. Kwa hiyo, tunaendelea; Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2011 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2011/2012 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha ili aweze kutoa maoni ya Kamati yake, kuhusu Bajeti ya Serikali, Mheshimiwa Dkt. Kigoda.

**MHE. DKT. ABDALLAH O. KIGODA – MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI :** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 96(6) cha Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, ninaomba kutoa maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2010 na Malengo ya Uchumi katika kipindi cha muda wa kati (2011/2012 -2015/2016), pamoja na Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Fedha na Uchumi ilipokea na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa ya Mwaka 2010 na Malengo ya Uchumi katika kipindi cha muda wa kati (2011/2012 – 2015/2016), ikifuatiwa na ile ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012. Kamati inapenda kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa H. Mkullo, kwa ushirikiano wake na Kamati, vilevile Wizara kuwa sikivu na kukubaliana na ushauri uliotolewa na Kamati katika kuboresha Bajeti hii. Aidha, Kamati inakiri kuwa na majadiliano ya tija na Naibu Mawaziri wa Fedha, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu, Kamishna wa TRA, Wataalamu wa Wizara, pamoja na wale wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, yanaendelea vizuri. Bajeti iliyowasilishwa inaweka msisitizo katika utekelezaji badala ya michakato; ni bajeti inayosisitiza vitendo badala ya nadharia, *blendind theory into practice.*

Mheshimiwa Spika, dhana ya kuwa uandaaji na maelezo ya Bajeti ya Nchi ni suala la Serikali pekee, hivi sasa ni dhana iliyopitwa na wakati. Kwa mantiki hii ni vigumu mihimili mingine ya Taifa hususan Bunge, kuepuka changamoto zitokanazo na upungufu wa utayarishaji na mawasilisho ya Bajeti ya Nchi. Katika nyakati hizi Bajeti siyo suala la Serikali pekee (*Domain of the Executive),* hasa tunapoendeleza na kujenga utaratibu katika mifumo yetu ya Uwazi na Uwajibikaji wa Bajeti (*Budget Transparency and Accountability),* ambao unahimiza hata kutoa taarifa kwa Wananchi wa kawaida kupitia Bajeti ya Wananchi *(Citizen's Budget)* ili nao waelewe mwelekeo wa Bajeti. Hata zoezi la Kambi ya Upinzani la kutoa Bajeti Mbadala siyo jambo la ajabu, kwani ni utaratibu ule ule wa kuboresha dhana ya Uwazi na Uwajibikaji wa Bajeti. (*Makofi)*

Bunge kama chombo cha kuwakilisha Wananchi, jukumu lake katika uandaaji na utayarishaji wa Bajeti ni suala lisilo na mjadala, hasa ikizingatiwa kuwa, unapotokea upungufu katika Bajeti ni lazima Wananchi watasikika wakitoa hoja zao kuwa Spika na Bunge lake limeshindwa kuishauri Serikali vizuri.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ni chombo muhimu cha kuendesha nchi na kuelekeza mwelekeo wa maendeleo ya nchi. Bajeti huandaliwa kitaalam na kiufundi *(technically prepared)* ili kufikia malengo, madhumuni, misingi na shabaha zilizowekwa. Pamoja na hali hii, lipo eneo moja ambalo ni muhimu kuzingatiwa wakati wa kuandaa Bajeti, linalohusu Umma unasemaje au Mawazo ya Umma juu ya Bajeti ni yapi *(Public Perception of the Budget).* Kwa sababu mara nyingi Bajeti huandaliwa kila mwaka, Umma ndiyo kipimo chao kikubwa cha mafanikio au kipimo cha maeneo yapi

yaliyojitokeza kama matatizo katika mwaka uliopita na hivyo Bajeti ya nchi kuwa ni ufumbuzi wa matatizo hayo katika kipindi kijacho.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hii, Bajeti pamoja na changamoto nyingi zilizopo ni lazima ijielekeze na kuangalia mafanikio au matatizo yaliyojitokeza, ambayo yanagusa masuala ya Kitaifa (*Issues of National Interest)*. Masuala hayo ya Kitaifa ndiyo yanayopaswa kuzingatiwa na Bunge katika kuitafakari Bajeti hasa katika muda mfupi na wa sasa *(Immediate or Short Term),* Muda wa Kati na Muda Mrefu. Kamati ya Fedha na Uchumi kutokana na uzoefu ilioupata, imetoa ushauri kwa Serikali kushughulikia masuala ya *National Interest* yaliyojiri ili kuhamasisha Wadau kujishughulisha katika kujenga Uchumi wa Nchi.

Mheshimiwa *Spika*, Serikali imekwishatoa kwa kina maelezo juu ya Hali ya Uchumi wa Taifa na Mapendekezo ya Bajeti katika kipindi kijacho cha 2011/12 hadi 2015/16, pamoja na kuelezea Mpango wa Maendeleo Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16). Aidha, Sera ya Mapato na Matumizi pamoja na mfumo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, nao umeelezwa katika Hotuba ya Waziri wa Fedha. Taswira ya Hali ya Uchumi wa Nchi inaonesha kuwa, ukuaji wa Uchumi Jumla kupitia Pato la Taifa umeongezeka kwa asilimia 7.0 mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 6.0 mwaka 2009, ukuaji wa rasilimali umeongezeka kwa asilimia 26.5 ikilinganishwa na mwaka 2009, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje imeongezeka kwa asilimia 22.9 kutoka Dola za Kimarekani 4780.4 mwaka 2009 hadi Dola za Kimarekani 5876.5 mwaka 2010. Ukuaji wa baadhi ya sekta pia umeongezeka: kilimo asilimia 4.2 ikilinganishwa na 3.2 mwaka 2009, ujenzi asilimia 10.2 ikilinganishwa na asilimia 7.2 mwaka 2009 na kadhalika. Hata hivyo, pamoja na taaswira hii bado changamoto kubwa inayojitokeza ni jinsi gani mafanikio haya ya Uchumi Mkubwa – Jumla yanapunguza viwango vya umaskini vya Wananchi walio wengi, hasa kutokana na kupunguza umaskini wa kipato *(linking the macro and micro level).*

Mheshimiwa Spika, tumejifunza sasa, hili linawezekana tu pale ambapo rasilimali za Taifa zitaelekezwa kwenye maeneo ambayo yanawagusa Wananchi wengi katika shughuli zao za kila siku. Takwimu zinaonesha kuwa, sekta zinazochangia kwa kiwango kikubwa ni Ujenzi asilimia 10.2, Mawasiliano asilimia 22.1 na zile zinazotoa Huduma. Sekta hizi hugusa idadi chache ya watu katika Taifa na vilevile haziongezi katika ukuaji wa uchumi unaowagusa wengi ikilinganishwa na Sekta ya Kilimo, Uvuvi, Ufugaji na Sekta za Wananchi, ambazo zinaajiri Wananchi wengi, lakini mchango wake katika Pato la Taifa haujakua kwa kasi kubwa.

Hali hii inaashiria kuwa, bado Serikali ina changamoto kubwa ya kuendeleza Sekta hizi kupitia hatua za makusudi za kuongeza rasilimali na vivutio ili kuendeleza maeneo haya na kupunguza umaskini wa watu hasa wa kipato. Kwa ulazima maeneo haya yatapiga hatua za maendeleo zikihusishwa na uendelezaji na uboreshaji wa huduma za jamii; afya, elimu na maji, kwa maana ya uwekezaji katika rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika, Kamati imezingatia misingi na shabaha ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2011/12, zinazolenga kupunguza umaskini. Kamati imeridhika na hatua na

uamuzi wa Serikali wa kuweka msisitizo katika vipaumbele vikuu vya jumla vitano katika miaka mitano ijayo. Vipaumbele hivi ni vichache na vinazingatia hali halisi ya uchumi wa Nchi pamoja na uwezo wetu wa kuamsha rasilimali za kugharamia vipaumbele hivyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa, uwekaji wa vipaumbele hivi hauna maana ya kuwa Sekta nyingine ziathirike. Badala yake kuendeleza vipaumbele hivi, ndivyo vitakuwa vyanzo vya nguvu ya kuibua uchumi na hatimaye kupunguza viwango vya umaskini. Hata hivyo, kama msingi wa vipaumbele unavyodai ni kuwa rasilimali zinazohitajika hazitoshelezi. Lazima kuchagua nini kianze na nini kisubiri kama alivyosema Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Nyerere "kupanga ni kuchagua." Hivyo, baadhi ya Sekta ni lazima *(necessarily)* zitakosa fedha za kutosha. Vipaumbele vichache vilivyooneshwa ni hivi vifuatavyo:-

(i) Nishati: Kuendeleza umeme, gesi, nishati ya jua na upepo;

(ii) Miundombinu: Kuendeleza reli, bandari, barabara na usafiri wa anga pamoja na uendelezaji wa Mkongo wa Taifa wa TEHAMA;

(iii) Kilimo, Mifugo na Uvuvi;

(iv) Kuendeleza huduma za maji kwa matumizi ya nyumbani, mifugo viwandam pamoja na huduma za Maji Taka Mijini na Vijijini; na

(v) Kuendeleza Rasilimali Watu *(Human Resource Development).*

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2011/12 imefanikiwa kulenga katika zile hatua za kupunguza kwa kiasi fulani makali ya maisha, hasa kwa kurekebisha na kudhibiti ongezeko la bei ya mafuta, ongezeko la bei za bidhaa na huduma, nia ya kuimarisha hifadhi ya Taifa ya Chakula, azma ya kuongeza ajira na kudhibiti matumizi ya Serikali. Kamati inaamini kuwa, hatua hizi zitafanikiwa kwa kuhusisha Serikali yenyewe (Sekta ya Umma), sekta binafsi na Wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Bajeti iliyowasilishwa, tukizingatia Sera za Mapato na Matumizi, inatuonesha kuwa, Uchumi una changamoto kubwa katika eneo la kukuza mapato ili kuhimili mahitaji yetu yanayohitajika kugharamiwa. Kamati inaishauri Serikali ichukue hatua madhubuti za kusimamia uchumi ukizingatia kuwa kikwazo kikubwa ni uwezo wake wa kuongeza mapato yatakayokidhi matumizi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Fedha na Uchumi inakubaliana na uamuzi wa Serikali kuingilia kati hali halisi ya sasa Kitaifa inayoletwa na kupanda sana kwa gharama za maisha na hatimaye kujitokeza kwa malalamiko mengi kutoka makundi mbalimbali ya Wananchi hususan Mijini na Vijijini. Makali ya maisha yanajionesha katika upatikanaji wa mahitaji muhimu na ya lazima hasa chakula, yanayochangiwa na bei za juu na umaskini wa kipato. Kwa kawaida athari za kupanda kwa gharama za maisha zinawaathiri sana Wananchi wenye kipato cha chini ikilinganishwa na wale

wenye uwezo. Hawa wenye uwezo wanaweza kujirekebisha/kuji-*adjust* haraka na hivyo athari hizo kuwa ndogo.

Mheshimiwa Spika, bei za vyakula kama unga wa sembe, maharage na sukari ambavyo hutumiwa na watu wengi Mjini na Vijijini, hasa wenye kipato cha chini zimeongezeka. Kamati inaisisitiza na kuishauri Serikali katika kipindi kifupi itekeleze mkakati wa makusudi wa kupunguza makali ya maisha (*reduction of high cost of living)* kama ilivyoainishwa kwenye Bajeti. Pamoja na kuwa hali hii imetokana na kuongezeka kwa bei za mafuta katika soko la dunia, upungufu wa umeme nchini na upungufu wa chakula; Serikali haina budi kuchukua mapema hatua za kiutawala *(administrative intervention)* kurekebisha hali hii.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Hifadhi ya Chakula, Kamati inakubaliana na hatua za Serikali za kuendeleza na kuimarisha matumizi ya Hifadhi ya Taifa ya Chakula *(SGR).* Kamati inaipongeza Serikali kwa kuuza mahindi kwa bei ya chini hasa katika maeneo ya mjini ili kupunguza viwango vya bei ya unga. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuwa makini katika viwango vya bei ya mahindi inayowekwa, isiwe na tofauti sana na bei ya wasindikaji hasa ikizingatiwa maeneo mengi mjini hutumia unga wa sembe badala ya dona. Zoezi la kusafirisha chakula toka maeneo yenye ziada na yale pungufu, yanasisitiza umuhimu wa mikakati ya kuboresha barabara pamoja na kupunguza gharama za nishati ya dizeli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza Serikali kuendeleza haraka mpango wake wa kuongeza Hifadhi ya Chakula kwa ujenzi wa maghala ya tani 20,000 Shinyanga, tani 40,000 Dodoma na tani 20,000 Morogoro ili kusogeza huduma hii kwenye maeneo ya upungufu wa chakula wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa bei ya mafuta pamoja na tozo za mafuta; Kamati inakubaliana na hatua ya Serikali ya kupunguza tozo zilizopo katika bei za mafuta na zoezi hili lifanyike kwa haraka. Tozo hizi zinazokaribia 21 ni mzigo mkubwa kwa watumiaji. Utitiri wa tozo hizi inazipa hadhi ya kuwa Tozo Kero *(Nuisance Levies).* Tozo hizi zinazotozwa na taasisi mbalimbali; TRA, TPA, SUMATRA, TBS, Tipper, EWURA na kadhalika, zikihusisha bei ya mafuta ya soko la dunia *(FOB na CIF)*, wingi wa mafuta na Dola ya Marekani. Taasisi hizi bado hazijazingatia gharama halisi zinazotumika katika kutoa huduma kwa wateja. Tozo zinapanda wakati bei za mafuta zinapanda na wakati shilingi yetu inaposhuka thamani, ikilinganishwa na dola hata pale ambapo gharama halisi za utoaji huduma hizo hazikupanda, bado gharama zinakuwa kubwa. Kamati inaishauri Serikali kupunguza au kufuta tozo hizi haraka iwezekanavyo na viwango vikadiriwe kwa kutumia Shilingi ya Tanzania badala ya Dola ya Marekani katika kipindi hiki cha Bajeti. Kamati inasisitiza kuwa, hata kama tozo hizi ni za kisheria (*statutory),* Serikali itumie Sheria Mama, *Public Finance Act 2009/10,* kukamilisha zoezi hili. Bei za mafuta kwa miaka mitatu iliyopita zimepanda mara tatu. *(Mkaofi)*

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili, Kamati vilevile inaishauri Serikali ising'ang'anie tu katika kufuta tozo, maana hizi ni sita tu kati ya maeneo 21. Ipo haja ya

Serikali kuangalia pia *Excise Duty* na *Import Duty* ili punguzo la gharama za mafuta liwe endelevu hata bei zikipanda. Aidha, *Road Toll* isipunguzwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa hatua hii na ufuatiliaji wake utapunguza kwa kiwango kikubwa gharama za maisha. Aidha, utaratibu huu vilevile utapunguza tatizo la uchakachuaji wa mafuta ambao umekithiri. Tatizo hili, takwimu zinaonesha linaipotezea Serikali mabilioni ya shilingi kama mapato yake. Zoezi hili pia lilenge kuondoa tofauti kubwa ya bei ya dizeli na mafuta ya taa, ambayo ndiyo chanzo cha uchakachuaji ingawa Hotuba ya Serikali imekuwa kimya kuzungumzia tatizo hili linaloendelea kupunguza mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati vilevile inakubaliana na Serikali kuanza sasa utaratibu wa ununuzi wa mafuta kwa wingi *(Bulk Procurement)*, eneo ambalo limekuwa likiongelewa na Kamati pamoja na kushauri kwa kipindi cha muda mrefu. Kamati inajua kuwa uagizaji wa mafuta katika shehena ndogo ndogo huongeza gharama za usafirishaji, bima na msongamano wa meli bandarini na hivyo kupandisha gharama za matumizi ya bidhaa husika. Changamoto mbele ya Serikali sasa ni muda wa utekelezaji wa hatua hii. *Bulk Procurement* itapunguza makali ya tozo na hivyo kupunguza gharama za mafuta kwa asilimia 20 hadi 30. *Kurasini Oil Jetty* na *Single Point Mooring* ziimarishwe kuwezesha upatikanaji wa mafuta hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua kadhaa za kibajeti *(Budgetary Measures),* ilizochukua kupitia maboresho ya mfumo wa kodi, ada, tozo na hatua nyingine za mapato. Eneo hili kwa kiasi kikubwa limepunguza gharama kwa uchumi, vilevile hata katika maeneo yanayogusa Sekta za Wananchi; kilimo, mifugo na uvuvi. Marekebisho yamegusa Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT),* Sheria ya Kodi ya Mapato, Sheria ya Elimu, Sheria ya Ushuru wa Mafuta ya Petroli, Sheria ya Leseni za Biashara, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Marekebisho ya Ada na Tozo. Marekebisho haya yatasaidia kupunguza ukali wa maisha kama ilivyooneshwa kwenye Kitabu cha Hotuba ya Waziri.

Mheshimiwa Spika, ili bajeti hii iwe tendaji, Serikali haina budi kutekeleza maamuzi yote yaliyofikiwa kwenye bajeti ya kupunguza ukali wa maisha mapema iwezekanavyo ili kuwapa ari Wananchi kuwa Serikali inajali na iko makini. Hali ya uzalishaji wa umeme nchini bado haijakidhi mahitaji na hivyo kusababisha mgao wa umeme nchini. Upatikanaji wa umeme kwenye Gridi ya Taifa kwa sasa ni megawati 470 tu ikilinganishwa na mahitaji ya juu ya megawati 833. Tatizo la mgao wa umeme lisipotatuliwa haraka, litapunguza kasi ya ukuaji wa uchumi.

Kwa mfano, Ukuaji halisi wa Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2001, Sekta ya Viwanda na Ujenzi imeshuka kutoka asilimia 10.4 mwaka 2005 hadi asilimia 8.2 mwaka 2010. Tafiti zinaonesha kuwa, gharama za upungufu wa umeme viwandani zinaongeza gharama ya uzalishaji kwa asilimia mbili hadi 15, hatimaye kuwa mzigo kwa watumiaji.

Mheshimiwa Spika, wakati sasa umefika Serikali kutoa maamuzi na utaratibu wa makusudi kwenye eneo la Nishati ya Umeme wa kuachia Sekta Binafsi shughuli za

uzalishaji. Serikali iendelee kuwekeza kwenye usafirishaji wa umeme *(transmission)* na usambazaji *(distribution)* wa umeme. Ni vyema Serikali ikafikiria kuchukua maamuzi ya kutenganisha majukumu haya matatu. Wazalishaji hawa Binafsi wapewe uhuru na mamlaka ya nani wawe ni wateja wao, kufuatana na viwango vitakavyowekwa kwa njia ya ushindani, sheria na taratibu zinazokubalika.

Katika Bajeti hii umeme umetengewa shilingi 539.3 bilioni, ikilinganishwa na shilingi 327.2 bilioni, mwaka uliopita ongezeko la asilimia 65. Hili ni ongezeko kubwa likilinganishwa na maongezeko mengine katika bajeti za kisekta.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha uchimbaji wa madini kwa mwaka 2005 ulichangia asilimia 16.1 ya ukuaji halisi wa Pato la Taifa *(GDP),* ikilinganishwa na asilimia 2.7 kufikia 2010. Hali hii inaonesha Serikali imekuwa ikipata mapato madogo kadiri miaka inavyoongezeka, tofauti na mategemeo hasa ikizingatiwa kuwa idadi ya migodi imeongezeka. Kamati inaishauri Serikali kuwa, sasa umefika wakati wa kuwabana wawekezaji kwenye Sekta ya Madini ili kuchangia Pato la Taifa.

Serikali ichukue hatua ya kuipatia migodi ya umeme au kuwaruhusu wenye migodi kuwekeza kwenye umeme kwa utaratibu maalum na hivyo kuweza kufuta misamaha ya kodi wanayoipata migodi hii ili kuongeza mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, wawekezaji wasaidie kuhifadhi mazingira na kuwezesha Miradi ya Maendeleo kwenye maeneo ya migodi. Serikali Mwaka 2010/2011 ilifanya marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT),* Sura 148 ili kupunguza kodi kilimo. Matokeo yamejionesha kuwa, shughuli za kilimo zinazojumuisha mifugo; zimechangia asilimia nukta mbili ya Pato la Taifa katika mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 3.2 mwaka 2009. Mwelekeo huu, pamoja na uimarishaji mikakati ya Kilimo Kwanza, unaashiria Sekta ya Kilimo kufanya vizuri itakapowekewa mazingira bora na hatimaye kuongeza vipato vya wakulima. Uwekezaji mkubwa katika kilimo cha umwagiliaji, vivutio vya makusudi na kurahisisha huduma zinazosaidia kilimo, hususan usafiri na bei za mafuta zitaimarisha sana wadau wa sekta hii.

Mheshimiwa Spika, mfano ulio hai ni Sekta ya Usafirishaji inayosafirisha asilimia 75 ya shehena yote nchini, pamoja na mazao ya kilimo, hutozwa asilimia 25 kama kodi ya betri za muundo wa *maintenance free,* hutozwa ushuru wa matairi asilimia 25, hutozwa utitiri wa kodi kama vile alama za zimamoto (*fire stickers),* leseni ya EWURA, gharama za ukaguzi wa magari, leseni za barabara, hutozwa tozo za huduma za Miji na kadhalika. Ni dhahiri kwamba, kodi, tozo na gharama zote hizi anayezibeba ni mkulima.

Nchi jirani wao wanatumia viwango vya asilimia O vya COMESA kama ushuru wa matairi na betri, zinatumia asilimia 20 ya viwango vya COMESA kwa ushuru wa matairi na betri; hivyo, kupunguza gharama za usafirishaji kuliko zilivyo hapa nchini, ikimaanisha kudumaza ushindani. Kamati inaishauri Serikali kufuta kodi na tozo hizi au kuzipunguza hadi asilimia kumi ili kuwapa nafuu wakulima. Hotuba ya Bajeti ya Serikali

imekuwa kimya katika eneo hili muhimu linalogusa wazalishaji ambao ndiyo wazalishaji wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mikakati ya kuongeza mapato ya ndani: Kamati inaamini kuwa Bajeti imara na endelevu kwa nchi inayoendelea kama Tanzania ni ile itakayokuwa na shabaha, mikakati sahihi na inayotekelezeka, inayolenga kupanua wigo wa kodi. Bado Kamati inaendelea kuishauri Serikali kujikita zaidi katika kutengeneza fursa za mapato na ajira katika Sekta ya Uvuvi hususan wa baharini, kuingiza sekta isiyo rasmi katika mfumo wa kodi, pamoja na kuondoa vikwazo kwa shughuli wanazofanya wajasiriamali wadogo *(SMEs)* na kujenga ujuzi na uwezo, kujikita katika kufuatilia kodi za majengo *(Property Tax),* hasa ikizingatiwa kuwa hivi sasa kuna mwamko *(boom)* ya ujenzi wa majumba makubwa hasa katika Miji Mikuu. Ujenzi huu bado haujasimamiwa (haujawa *regulated),* hasa ikizingatiwa kuwa uwekezaji wake unatumia fedha nyingi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ni lazima kuweka msisitizo mkubwa katika ukusanyaji wa mapato katika maeneo yasiyo ya kodi (*Non Tax Revenue).* Bado Serikali haijafanya kazi kubwa katika eneo hili. Shughuli za Maliasili na Utalii, shughuli za bidhaa za misitu (magogo) na kadhalika ni maeneo ya kuibua fursa. Serikali itakapofanikiwa katika eneo hili litapunguza tozo nyingi za kero ambazo wanashikwa Wananchi na hatimaye kupoteza ari ya kuchangia katika kuzalisha uchumi.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Nchi ikitegemea sana mapato yake ya ndani kutokana na vyanzo vya kodi bila ya kupanua fursa ya mapato yasiyo ya kodi (*Non Tax Revenue*), matokeo yake ni kuwa na kodi nyingi na hasa zile za kero na hivyo kudumaza uwekezaji katika uchumi pamoja na kudhoofisha hali ya kuibua fursa zilizopo. Mapato yasiyo ya kodi yatawafanya Wananchi kutambua kuwa wao pia ni Wadau wa Maendeleo. Lengo ni kuendelea kupunguza utegemezi wa Bajeti ya Serikali wa misaada ambao sasa umefikia asilimia 17 ikilinganishwa na asilimia 28 mwaka 2007/08.

Mheshimiwa Spika, Kamati inarudia kuishauri Serikali kudhibiti eneo la mapato na matumizi ya Serikali. Eneo hili bado ni changamoto; Matumizi ya Serikali bado yanaendelea kuwa makubwa kuliko mapato. Mwaka 2009/2010 mapato ya ndani ya Serikali yalikuwa Sh. 3,490.3 milioni na matumizi yalikuwa Sh. 6143.9 milioni.

Kwa kipindi cha Julai 2010 hadi Machi 2011, mapato ya Serikali yalifikia Sh. 4256.3 bilioni na matumizi yalikuwa Sh. 7169.3 bilioni. Katika kipindi cha 2011 – 2012 mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa Sh. 6775.2 bilioni wakati matumizi ya kawaida ni Sh. 8, 600.3 bilioni.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wetu wa Kibajeti unaonesha kuwa wa matumizi zaidi badala ya kuzalisha. Mfano, uwiano wa mapato na matumizi katika Mwaka 2007/08, Pato la Taifa lilikuwa asilimia 15.9 wakati matumizi yalikuwa asilimia 22.8; mwaka 2008/09 hali ilikuwa asilimia 16.2 ikilinganishwa na asilimia 25.7 ya matumizi; mwaka 2009/10 ilikuwa asilimia 16.4 ikilinganishwa na asilimia 24.6 ya matumizi; na mwaka 2010/11 hali inatarajiwa kuwa asilimia 17.3 ikilinganishwa na asilimia 26.4 ya matumizi. Kwa Mwaka 2011/12 mapato ya ndani ni asilimia 18.1 ya Pato la Taifa wakati

ikilinganishwa na asilimia ya matumizi, uchumi wetu unaashiria utumiaji mkubwa badala ya uzalishaji *(Net Consumer Nation).* Hali hii ni tofauti kwa nchi jirani zetu, yaani Uganda na Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kama ilivyoelezwa katika Bajeti kutekeleza mapema mikakati ya makusudi ya kupunguza matumizi ya Serikali yasiyo ya lazima *(Cost Cutting Measures – Expenditure Cuts)*. Katika Bajeti ya Mwaka 2011/12, vipo viashiria vinavyoonesha upungufu wa mapato, upungufu wa misaada na malipo kutoka nje. Hatua ya kupunguza matumizi itasaidia Bajeti ya Serikali kuwa endelevu na vilevile kuepuka *deficit financing* ambayo inaweza kuongeza athari za mfumko wa bei katika uchumi.

Serikali, kama moja ya eneo lililooneshwa katika Rasimu ya Mpango, ukurasa wa 17, imetambua kuwa posho za vikao na usafiri, zinajenga mfumo mbaya wa vivutio Serikalini na kwa hiyo basi, Serikali inatarajia kuzirekebisha au kuzifuta kabisa. Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua maalum za kuangalia eneo hili liwe njia ya kuongeza mapato. Aidha, Kamati inasisitiza Serikali kukamilisha haraka Muswada wa Sheria ya Manunuzi ya Umma, 2010 ili kudhibiti matumizi mabaya ya Fedha za Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado kuna tatizo kubwa la watumishi hewa katika Serikali Kuu, Mikoa, Wilaya pamoja na Taasisi zake. Kwa mujibu wa Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali, inaonesha kuwa, kiasi cha shilingi bilioni moja kilitumika kuwalipa watumishi hewa. Kamati inaishauri Serikali kuhakiki watumishi wake iliyowaajiriwa na kufuatilia maeneo mengine yanayoendeleza upotevu wa fedha za Serikali, kwa mfano, maduhuli yasiyokusanywa kwa wakati, malipo yasiyokuwa na stakabadhi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na uamuzi wa Serikali wa kuhuisha utaratibu wa kutoa misamaha ya kodi katika uchumi. Misamaha ya Kodi kwa makundi mbalimbali imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka na hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa, mapato ya Serikali yatokanayo na kodi. Misamaha iliongezeka kutoka asilimia 2.1 ya Pato la Taifa mwaka 2009/10 hadi kufikia asilimia 2.5 ya Pato la Taifa mwaka 2010/2011. Kiwango hiki ni kikubwa (kutoka Sh. 653.7 bilioni – mwaka 2009/2010 hadi kufikia Sh. 869.6 bilioni; Machi 2011); ni kiwango kikubwa kuliko kile cha *Government Budget Support (GBS)*, iliyotolewa na Wafadhili kwa Serikali kwa mwaka 2011/12. Nchi ya Kenya na Uganda hutoa Misamaha kwa kikomo cha asilimia moja ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1997 bidhaa tatu zilisamehewa kodi chini ya Jedwali la Kwanza *(Zero Rated),* bidhaa 11 chini ya Jedwali la Pili *(Exempted)* na makundi matatu yalisamehewa chini ya jedwali la tatu *(Relieved).*

Hivi sasa Jedwali la Kwanza lina bidhaa 14, bidhaa 29 kwa Jedwali la Pili na bidhaa 29 kwa Jedwali la Tatu. Bidhaa za walaji kama fenicha, nguo, vifaa vya elektroniki huchangia takriban asilimia 41 ya misamaha yote.

Athari ya misamaha hii ni kama zifuatazo: Ushawishi kwa biashara kujihusisha na mbinu za kukwepa kodi; kufanya usimamiaji wa kodi kuwa mgumu na hivyo kuathiri

utawala wa kodi; kuelekeza rasilimali kwenye tija hafifu; na hatimaye kupunguza mapato ya Serikali

Mheshimiwa Spika, kutokana na athari hizi, Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuhakikisha kuwa, misamaha ya Kodi isizidi asilimia moja ya Pato la Taifa. Aidha, Serikali iangalie misamaha ya kodi iliyopo sasa na itathmini gharama yake inavyoshabihiana na Pato la Taifa, iangalie faida na hasara za misamaha hiyo kwenye uchumi na hatimaye ijifunze nini kinafanyika katika nchi nyingine katika eneo hili. Hatua hizi zifanyike haraka kwa utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kuwa, uwekezaji nchini hautaongezeka kwa kuongezeka kwa misamaha ya kodi. Uwekezaji utaongezeka tutakapoondoa urasimu, rushwa na ubinafsi. Pili, uboreshaji wa miundombinu; barabara, reli, umeme na maji. Tatu, tuwe na sheria na taratibu zinazotabirika na endelevu.

Utaratibu wa *PPP* uanze haraka baada ya kanuni kukamilika ili kusaidia Bajeti ya Serikali katika Miradi ya Maendeleo. Fedha za Sekta Binafsi zitakuwa na mchango mkubwa hasa katika uwekezaji wa miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la uwekezaji bado lina changamoto. Pamoja na jitihada za Serikali, bado msukumo wa uwekezaji haujawa wa kutosha *(Investment Drive).* Licha ya maazimio ya kupunguza urasimu, rushwa na ucheleweshaji wa maamuzi, jitihada za kuboresha mazingira ya uwekezaji, Programu za *BEST*, kuanzishwa kwa Baraza la Uwezeshaji Wananchi ki-uchumi, mkakati wa utekelezaji wa sera ya Ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi *(PPP)* na kadhalika, msukumo wa uwekezaji nchini unasuasua *(investment drive).*

Bado mazingira yetu ya uwekezaji hayajaboreshwa vya kutosha hasa katika eneo la miundombinu, barabara, umeme, maji na kadhalika, bado tunahitaji kuendeleza umakini katika eneo hili. Thamani ya mitaji ya kigeni ya moja kwa moja *Foreign Direct Investiment (FDI)* ya dola milioni 573 kwa Tanzania yenye fursa nyingi, bado ni ndogo. Ipo haja kubwa ya msukumo wa uwekezaji *(investment drive)*. Kuendelea kutoa taarifa juu ya makaa ya mawe ya Mchuchuma, chuma cha Liganga, *SAGCOT* na kadhalika, bila ya utekelezaji kwa muda mrefu uliopita ni ishara ya kutokuwa makini. Haya ndio maeneo ya uhakika ya kuongeza mapato katika uchumi na kuanzisha viwanda mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Uvuvi ikipewa umuhimu stahiki ina nafasi kubwa ya kutoa mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi na ajira nchini. Hadi sasa bado sekta hii haijatumika ipasavyo na imeendelea kudorora na hazijafanyika jitihada za kutosha za kuikuza sekta hii na kuvutia uwekezaji. Katika kipindi cha miaka sita tangu 2005 hadi 2010, ukuaji halisi wa pato la Taifa kwa Sekta ya Uvuvi umeendelea kushuka kutoka 6% mwaka 2005 hadi asilimia 1.4 mwaka 2010 (Ofisi ya Taifa ya Takwimu - Ukuaji halisi wa Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2001). Hapa inaonyesha dhahiri Serikali haijaipa kipaumbele sekta hii ya uvuvi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuingia ubia na Serikali nyingine na kuihusisha kikamilifu sekta binafsi. Ukanda mkubwa wa Pwani yetu pamoja na wananchi wengi kujihusisha na uvuvi itasaidia kukuza mchango wa uvuvi katika uchumi pamoja na kuwa chanzo cha ajira.

Mheshimiwa Spika, kwa hali ilivyo sasa, uvuvi unafanyika kwa kutumia zana duni, hivyo Serikali inapaswa kuelekeza nguvu zake katika kuvutia uwekezaji wa ndani na nje. Kwa upande wa uwekezaji wa ndani, Serikali ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa mitaji ya kununulia zana za kisasa. Aidha, programu kama *Small Entrepreneurs Loan Facility (SELF)*, zitumike kuwezesha wananchi hususan vijana na wahitimu wa Vyuo vya Uvuvi kujiingiza katika Sekta ya Uvuvi kwa ufanisi. Wakati umefika kwa Serikali kuweka mazingira mazuri yatakayoshawishi uwekezaji mkubwa wa ufugaji wa samaki katika mabwawa, bahari na nchi kavu pamoja na ununuzi wa zana bora za uvuvi zikiwemo boti za kisasa *(fiber boats)*. Serikali ihamasishe wawekezaji wa Kitanzania kuwekeza katika kuanzisha karakana za kutengeneza boti za uvuvi hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa vile Muswada wa Sheria ya *PPP* tayari umekamilika pamoja na Kanuni zake, utekelezaji wake uanze mara moja, ili kuiwezesha Serikali kupata fedha za kuendeleza miradi yake, hususan ile ya miundombinu ya barabara, reli, bandari, nishati ya umeme na kadhalika. Zoezi hili halitakuwa na tija kama litatawaliwa na urasimu, rushwa na ucheleweshaji wa kutoa maamuzi. Maamuzi ya kuruhusu sekta binafsi kujiingiza katika uzalishaji wa nishati ya umeme, ujenzi wa barabara, ujenzi wa bandari utekelezwe ili Serikali ipate raslimali za ziada za kujenga uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Vyuo vyetu Vikuu vinatoa kila mwaka karibu vijana 700,000, sekta rasmi ya umma inayotoa ajira, inaajiri watu 40,000 tu. Ipo haja ya kutumia nguvu kazi hii kupitia mipango ya uwezeshaji, kuboresha huduma za fedha kama mabenki, vyama vya kuweka na kukopa, *VICOBA* na mifuko mbalimbali ili kuwapa vijana fursa ya kujiajiri na kujenga Uchumi wetu. Ingawa jitihada mbalimbali zimeshafanyika katika eneo hili, tatizo limeendelea kuwa lile la kuwasaidia walengwa wahusika *(targeting).*

Changamoto hii ni endelevu hasa ikizingatiwa kuwa idadi yetu inaongezeka kwa kasi ya asilimia 2.9 hadi tatu. Wanawake vijijini na mijini wanazaa wastani wa watoto 5.4 hadi sita. Kwa kasi ndogo ya ukuaji wa pato la Taifa kila mwaka la chini ya asilimia mbili, pamoja na tija ndogo katika kilimo, utegemezi ni wa hali ya juu. Hali hii inaashiria Mipango ya Elimu ijielekeze kwa wasichana ili wapate fursa kubwa ya kusoma zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa uchumi mkuu umeendelea kufanya vizuri pamoja na changamoto ya uhaba wa umeme, ukosefu wa mvua na matatizo mengine ya kimiundombinu, Serikali inatakiwa ibuni na iweke hatua ya kutafsiri mafanikio hayo na jinsi ya kuwagusa wananchi walio wengi vijijini ambao wengi ni masikini *(linking the Macro level with the micro level).* Maeneo ambayo yataweza kupunguza umasikini wa walio wengi na kwa uhakika, kwanza ni kuharakisha maendeleo ya kilimo; pili, kujenga

uwezo na ujuzi wenye umasikini; tatu, ni lazima kuondoa vipingamizi na vikwazo katika shughuli ndogo ndogo wanazofanya masikini pamoja na shughuli za kijasiriamali *(small and medium scale enterprises)*; nne, ni usawa wa kijinsia kwa fursa za uchumi na tano, lazima sera na mipango yetu itengeneze fursa za kuibua ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu suala la umasikini ndio ajenda ya sasa hivi, maendeleo ya raslimali watu *(human resource development)* ni muhimu. Kamati inaishauri Serikali kuongeza stadi *(skill)* za vijana wengi. Takwimu zinaonyesha kuwa kwa wastani nchi zinazoendelea zimefikia wastani wa asilimia 15 ya watu wenye stadi *(average skilled labour)* wakati Tanzania wastani ni asilimia tatu. Hali hii ni changamoto ambayo Serikali iifanyie kazi ili kupunguza umasikini. Kenya na Uganda, sekta isiyo rasmi inachangia takriban asilimia 50 ya Pato la Taifa wakati Tanzania mchango wake ni asilimia 15.

Mheshimiwa Spika, hatua ya Serikali ya kupeleka madaraka Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inahitaji ufuatiliaji wa karibu (*Decentralization by Devolution).* Serikali imekuwa ikitenga fedha nyingi kwa Halmashauri za Wilaya lakini bado ipo changamoto kubwa ya kujenga uwezo wa kiufundi na kitaalam (*capacity building).*

Halmashauri zinatakiwa ziwe bunifu *(innovative)* katika kutekeleza mipango yao ya kuibua uchumi, ajira, uwekezaji na kadhalika ili kuongeza mapato na kupunguza umasikini. Hatua ya Serikali ya kuanzisha *Expenditure Track Unit* pamoja na Ofisi ya Mkaguzi wa Ndani wa Fedha za Serikali (*Internal auditor)* ziwe ni hatua endelevu za kupunguza matumizi mabaya ya fedha, upotevu wa fedha na hatimaye kupima thamani ya fedha inayopelekwa huko *(value for money).* Utaratibu wa *decentralization by devolution* usizifanye Halmashauri kudumaa na kujenga utamaduni na utegemezi kutoka Serikali Kuu.

Kimsingi, utaratibu wa *D by D* uimarishwe ili kufaidi ukubwa wa nchi yetu na umiliki wa mpango wa wananchi wenyewe. Halmashauri ziwe na uwezo wa kufikiria zenyewe maeneo ya uwekezaji ajira na mipango Wilayani mwao. Mapato ya ndani yanayoibuliwa na Halmashauri za Wilaya ni kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua utaratibu wa *Cash Budget* katika kugharamia miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida. Utaratibu huu unaweza kupunguza *predictability of the budget.* Utaratibu wa sasa wa kupeleka fedha hizi Halmashauri kwa robo mwaka unapongezwa na Kamati. Lakini utaratibu huu unahitaji upatikanaji wa fedha kwa wakati *(timely delivery).* Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kwamba fedha zikichelewa kufika kwenye Halmashauri hasa mwishoni mwa mwaka, fedha ambazo hazitatumika zisirudishwe Hazina ili kukamilisha mipango iliyopangwa na kupunguza viporo vya miradi katika nyingi ya Halmashauri ya Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, riba za mikopo katika soko la fedha bado ni za juu na hivyo kupunguza matumizi ya mkopo, hasa kwa wananchi walio wengi. Serikali ifanye mambo yafutayo:-

- Kuendelea kuboresha muundo *(structure)* wa Sekta ya Fedha ili kuhakikisha uwepo wa mazingira mazuri ya ushindani wa vyombo vya fedha ambavyo vitawezesha taratibu kushuka kwa riba za mikopo na wakati huo huo kupanda riba za amana.

- Uwepo wa soko la fedha pamoja na uwepo wa ufanisi wa utendaji wa soko huwezesha upatikanaji wa riba nzuri katika soko. Historia inaonyesha kwamba mara baada ya Serikali kuruhusu uanzishaji wa Soko la fedha *(Financial Market),* Tanzania na vyombo vyake *DMS* na *DSE* bei na riba za fedha ziliboreka na kuelekea kwenye utulivu. Hata hivyo, Serikali inahitajika kuendelea na juhudi za uboreshaji wa mazingira na mfumo wa soko hili ili ulete manufaa zaidi.

- Kuboresha mazingira yanayosaidia kupunguza athari *(risks)* za ukopeshaji na zinazoweza kuathiri usalama wa mabenki *(Financial Risks)*. Kwa kawaida uwepo wa athari katika shughuli za ukopeshaji hujitokeza katika maeneo yafuatayo:-

  (i) Upungufu wa Sheria ya kumbana mkopaji ili awajibike kulipa kama alivyokubaliana na benki;

  (ii) Ulegevu wa dhamira ya mkopaji kulipa deni *(Credit culture)*; na

  (iii) Ukosekano wa taarifa muhimu kuhusu mkopaji ambazo zinasaidia benki kufanya maamuzi sahihi yenye uhakika wa kulipwa fedha baada ya kukopesha.

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu *(BOT)* inaendelea na utayarishaji wa mfumo *(Credit Reference Data Bank)* itakayosaidia Benki zinazokopesha ili kuwa na ufahamu sahihi wa historia ya mkopaji kabla ya kuamua kutoa mikopo hiyo. Kamati inashauri Serikali kwa upande wake kuendelea kuchunga matumizi/mahitaji yake na kuwa waangalifu kuhusu kukopa katika soko la ndani na hivyo kupunguza uwezekano wa kuathiri viwango vya riba ndani ya soko la fedha.

Mheshimiwa Spika, *Mortage Finance* kama utaratibu, bado haujawa wazi. Taratibu hazijajulikana kwa walengwa kuwezesha uelewa na matumizi ya fursa hii kuwa ya faida. Chombo chenye wajibu wa kutoa elimu kwa wananchi kifanye hivyo ili kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine la kuboresha ni lile la pensheni ya wazee. Wapo wazee milioni 2.4 nchini waliostaafu na wengi wanaishi vijijini, ni 4% tu ndio wanaopata huduma hii. Takwimu zinaonyesha kuwa kiwango cha umasikini cha wazee kinafikia 22% na karibu 53% ya yatima wanatunzwa na wazee. Mipango mizuri ya pensheni itasaidia kupunguza umasikini wa wazee na vile vile Serikali itakuwa inazingatia *areas of social protection;* hatua za uzalishaji mali na taratibu za kugawana kupitia kukua kwa uchumi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inabaini kuwa ipo haja ya kuweka sawa mtazamo wetu *(mind set)* na kubadilisha tabia mtazamo *(change of attitude)* jinsi tunavyowaona na

kukubali wawekezaji. Imejengeka tabia kwa baadhi ya wengi wetu kuwaona wawekezaji wa nje na wa ndani kama watu wasio waaminifu wala waadilifu au kuwachukia. Tabia hii inadumaza msukumo wa uwekezaji Tanzania. Serikali iweke utaratibu mzuri pamoja na vivutio vyenye tija kwa nchi na wawekezaji *(win – win situation)* ili kukuza uwezeshaji. Hakuna nchi duniani inayoweza kuendelea bila ya msukumo wa uwekezaji *(investment drive).*

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumalizia kwa kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya na ushirikiano wao walionipa katika kujadili na kupitia Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2010/2011. Naomba nitumie fursa hii kuwatambua Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mheshimiwa Eustace Osler Katagira, Mheshimiwa Maulidah Anna Valerian Komu, Mheshimiwa Dr. Binilith Satano Mahenge, Mheshimiwa Devotha Mkuwa Likokola, Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mheshimiwa William Augustao Mgimwa, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mheshimiwa Rosemary Kasimbi Kirigini, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Rostam A. Aziz, Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, Mheshimiwa Andrew John Chenge na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Victor Mwambalaswa - Makamu Mwenyekiti kwa kunisaidia kuiongoza Kamati, Mheshimiwa Mustafa Mkullo - Waziri wa Fedha na Uchumi na Manaibu Waziri wa Fedha - Mheshimiwa Gregory G. Teu na Mheshimiwa Pereira A. Silima. Aidha, naomba niwashukuru Watendaji Wakuu wa Wizara, Benki Kuu, Mashirika, Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa kuandaa bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana wewe mwenyewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kutupatia miongozo na maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Katibu wa Bunge Dr. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Ndugu Michael Kadebe kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, naomba niendelee kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Handeni, kwa sapoti kubwa wanayonipa katika kushughulikia matatizo ya Jimbo letu. Ujumbe wangu bado ni ule ule, mambo mazuri hayataki haraka.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha mwaka 2011/2012 kama alivyowasilisha mtoa hoja hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nitamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kuhusu hoja hii. Mheshimiwa Kabwe zitto. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani Bungeni, naomba kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Hali ya Uchumi na Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012. Kabla ya kuanza kutoa maoni, napenda kwanza nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Dr. Abdallah Kigoda, kwa uwasilishaji mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba radhi kwa lililotokea asubuhi wakati Mheshimiwa Magufuli anajibu swali kuhusu Kigoma, haikustahili kufanya hivyo na ninakuomba radhi sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Bunge hili, kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kambi ya Upinzani kuhusu hali ya uchumi wa nchi yetu na bajeti kwa mwaka 2011/2012 kwa mujibu wa kanuni za Bunge ya 96(6).

Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya Waheshimwa Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani ambao hawakupata nafasi ya kushiriki au kutoa rambirambi zao kwako kwa msiba mkubwa uliokupata wa kuondokewa na mama yako mpenzi, nifanye hivyo kwa niaba yao. Pole sana.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza kutoa mtazamo wetu, naomba nikishukuru Chama changu cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Viongozi wangu Wakuu wote, kwa juhudi kubwa tunazozifanya ili kuhakikisha Watanzania wanaelewa maana halisi ya wananchi kuwa na mamlaka kwa Serikali waliyoiweka madarakani kwa njia ya kura.

Vile vile na kwa umuhimu wa kipekee namshukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni - Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, kwa kuniteua kuwa Waziri Kivuli wa Wizara hii nyeti katika uchumi na maendeleo ya nchi. Kama ilivyo ada yangu, nitaifanya kazi hii kwa uaminifu, uadilifu na umakini mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, namshukuru Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai - Naibu Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Fedha, kwa ushirikiano wake pamoja na timu nzima ya Kambi ya Upinzani kwa kazi yao kubwa waliyoifanya katika maandalizi ya hotuba hii. Napenda kuwashukuru kwa dhati kabisa Watanzania waliotupatia maoni mbalimbali kupitia *social media* kama *facebook, twitter* na hata wengine kwa kupitia ujumbe mfupi wa *sms*. Maoni yao yamesaidia kuboresha hotuba hii na pia kuimarisha ushiriki wa wananchi katika kutengeneza sera za nchi.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sijatenda haki kwa wananchi wa Jimbo la Kigoma Kaskazini, kama sitawashukuru kwa imani kubwa waliyonayo kwangu, nami nawaahidi kuwa nitaitunza na kuiheshimu imani yao kwangu, kuendelea kushirikiana nao kuleta maendeleo katika Jimbo na Mkoa wetu na mwisho kukifanya Chama cha Demokrasia na Maendeleo *(CHADEMA)* kuwa chama tawala ifikapo mwaka 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, kwa mapenzi ya hali ya juu kabisa, napenda kumshukuru mama yangu mzazi ambaye yupo pale na anamwangalia mtoto wake kipenzi leo akiwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti. Nashukuru sana mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti ya nchi ni nyenzo *(instrument)* ya maendeleo. Sio suala la Urari wa Mapato na Matumizi tu, ni namna ya kutumia raslimali chache tulizonazo kwa ajili ya kutengeneza raslimali nyingi zaidi na hatimaye kuboresha maisha ya wananchi na kujenga Taifa imara. Hata hivyo, bajeti inahusu namna ya kukusanya na kutumia pesa za wananchi kwa manufaa yao ya pamoja.

Kwa bahati mbaya, mchakato wa kuamua namna ya kuzitumia, kuzisimamia na kuhakikisha kuwa pesa hizo zinakwenda zinakotakiwa kwenda ni mgumu kwa wananchi wa kawaida kuweza kushiriki. Hii inatokana na ukweli kuwa sehemu kubwa ya taarifa zinazohusiana na bajeti huwa haziwekwi wazi kwa umma, na hata zile zinazopatikana huwa katika namna iliyo ngumu kueleweka. Hivyo, wananchi wengi huwa hawana fursa ya kushiriki katika michakato ya bajeti. Kwa ujumla, michakato mingi rasmi huwa haiko wazi kwa wananchi. Hata hivyo, juhudi zilizoanza sasa za kutaka kuanzisha Ofisi ya Bajeti ya Bunge zitasaidia sana kuweka uwazi katika bajeti ya nchi na hivyo kuweka urahisi wa wananchi kushiriki katika mchakato.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imekuwa ikiitaka Serikali kuweka vitabu vya bajeti katika mfumo rahisi unaoweza kueleweka na kufuatiliwa na wananchi wengi, lakini suala hilo limekuwa gumu kufanyika. Nina matumaini kuwa kwa miaka ijayo na hasa baada ya kuanzisha Ofisi ya Bajeti ya Bunge, vitabu vya bajeti vitakuwa vinapatikana mapema na kwa njia rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaamini kuwa ushiriki mkubwa zaidi wa umma na uchunguzaji wa utungaji na utekelezaji wa bajeti utaboresha uwajibikaji na kuziba mianya zaidi ya ufisadi na matumizi mabaya ya raslimali za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mahatma Gandhi aliwahi kusema: "Mabadiliko ya kidemokrasia hayawezekani iwapo hatupo tayari kusikiliza upande mwingine. Tunafunga milango ya kufikiri wakati tunapokataa kuwasikiliza wapinzani wetu, au baada ya kuwasikiliza, tunawafanyia mzaha. Kutokuvumiliana kunapokuwa ndiyo mazoea, tunajiweka katika hatari ya kutokujua ukweli." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani ilitoa maoni yake ya mwelekeo wa Bajeti na kuainisha mambo kadhaa itakayoyapendekeza katika bajeti yake mbadala. Mambo hayo ni pamoja na:-

(i) Kupunguza misamaha ya Kodi isizidi 1% ya pato la Taifa;

(ii) Kupunguza kodi na tozo kwenye mafuta ya petroli na dizeli ili kupunguza mfumko wa bei na ukali wa maisha kwa wananchi;

(iii) Kufanya marekebisho makubwa katika mfumo wa malipo Serikalini hususan kuondoa posho za vikao (*sitting allowances*) kwa watumishi na viongozi wote wa Umma; na

(iv) Kuelekeza sehemu ya tozo ya kuendeleza ujuzi (*Skills Development levy*) kwenye Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, baadhi ya mambo haya yalizingatiwa na kupewa kipaumbele. Nachukua fursa hii kumpongeza Waziri mwenzangu kwa kusikiliza maoni yetu kwenye baadhi ya mambo hayo na hivyo kuonyesha kwa umma moja ya faida ya mfumo wa Vyama Vingi. Tunatarajia kuwa Serikali itaendelea kusikiliza maoni yetu na kuyafanyia kazi. Changamoto hii na kwa uzito ule ule ipo pia kwetu sisi wa Kambi ya Upinzani kusikiliza pia maoni ya Serikali. Ni kwa namna hii ndiyo tutajenga Taifa la watu walio huru, lenye demokrasia, usawa na haki, na lenye kutoa fursa kwa wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapopitia hali ya uchumi ili kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani Bungeni ni vyema tulijue Taifa letu kwa takwimu chache.

Mheshimiwa Spika, pato la Taifa limefikia shilingi trilioni 32 na hivyo pato la wastani la kila mtu kuwa shilingi 770,000. Tanzania ina takriban wananchi milioni 42 na kati ya hao milioni 11 wapo kwenye Taasisi za Elimu kwa maana ya Shule za Msingi, Sekondari, Vyuo vya Ufundi na Vyuo vya Elimu ya Juu. Kwa hiyo, robo ya Watanzania wanasoma hivi sasa na wakimaliza wanatarajia kupata ajira kwa kuajiriwa au kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, kushuka huku kwa thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni, kunatokana na kukosekana kwa mikakati thabiti ya kuhakikisha kuwa shilingi inaimarika kwenye soko na hasa kutokana na sera mbovu za kiuchumi na usimamizi usio makini.

Mheshimiwa Spika, deni la Taifa nalo linaonekana kuongezeka kwa kasi ya ajabu sana na hivyo kupelekea Taifa kuwa na mzigo mkubwa sana wa madeni. Ninapopitia hali ya uchumi ili kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani Bungeni, ni vyema tulijue Taifa letu kwa takwimu chache.

Mheshimiwa Spika, pato la Taifa limefikia shilingi trilioni 32 na hivyo pato la wastani la kila mtu kuwa Sh. 770,000/=. Tanzania ina takribani wananchi milioni 42 na kati ya hao milioni 11 wapo kwenye Taasisi za Elimu kwa maana ya Shule za Msingi, Sekondari, Vyuo vya Ufundi na Vyuo vya Elimu ya Juu. Kwa hiyo, robo ya Watanzania wanasoma hivi sasa na wakimaliza wanataraji kupata ajira kwa kuajiriwa au kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010 Watanzania milioni 19 walikuwa wanatumia simu za mkononi na hivyo kufanya asilimia 45 ya Watanzania kuwa na simu na kuliweka Taifa katika nafasi ya juu kabisa duniani ya matumizi ya simu. Asilimia 64 ya Watanzania wanapata maji safi na salama mijini na asilimia 57.8 hupata huduma hii vijijini. Asilimia 14 ya Watanzania wanapata huduma ya umeme na kwa vijijini ni 2% tu.

Mheshimiwa Spika, Asilimia 33.4 ya Watanzania wanaishi chini ya mstari wa umasikini na kwa waishio vijijini ni asilimia 37.4 wakati asilimia 16.2 tu ya Watanzania waishio Dar es Salaam wanaishi chini ya mstari wa umasikini. Wakati tofauti ya kipato kwa Watanzania ni asilimia 35, matajiri wa juu asilimia 20 wanamiliki asilimia 42 ya pato la Taifa *(consumption expenditure)* na masikini wa chini kabisa asilimia 20 wanamiliki 7% tu ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2010/2011 iliyosomwa hapa Bungeni, inaonyesha kuwa katika mwaka 2010/2011 pato halisi la Taifa lilikuwa kwa kiwango cha asilimia 7.0 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.0 mwaka 2009/2010. Taarifa inaonyesha kuwa ukuaji huu wa uchumi ulitokana na kuchangiwa zaidi na kuongezeka kwa viwango vya ukuaji katika shughuli za kiuchumi zenye mchango mkubwa katika pato la Taifa na hasa kilimo, biashara na matengenezo na ujenzi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na taarifa hiyo, ukweli ni kuwa ukuaji wa viwango vya juu ulionekana zaidi kwenye Sekta za Mawasiliano 22.1%, ujenzi 10.2%, umeme na gesi 10.2%, fedha 10.1% na uzalishaji viwandani 7.9%. Hata hivyo, pamoja na ukuaji wa sekta hizi, mchango wake katika pato la Taifa ni mdogo kulingana na kiwango cha ukuaji wa sekta husika kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya hali ya uchumi inaonyesha kuwa pamoja na sekta kadhaa kukua, lakini bado hazijaongeza mchango wake katika ukuaji wa pato la Taifa ukilinganisha na ukuaji wa sekta husika. Kwa mfano, Sekta ya Mawasiliano imekua kwa 22.1% ila mchango wake katika pato la Taifa ni 2.1% tu. Shughuli ndogo za hoteli na migahawa ukuaji wake ulikuwa 6.1%, lakini mchango wake katika ukuaji wa pato la Taifa ni 2.3% tu. Hii ina maana kuwa sekta hizi hazina uhusiano wa moja kwa moja

*(strong linkages)* katika ukuaji wa uchumi na katika kukuza pato la Taifa na hivyo kushindwa kupunguza hali ngumu ya maisha kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya hali ya uchumi inaonyesha kuwa mchango wa shughuli za kiuchumi za kilimo umeendelea kushuka, hii ni pamoja na ukweli kuwa Serikali katika mwaka husika ilijikita kwenye Kilimo Kwanza, jambo ambalo halionyeshi kama ni kilimo kwa kauli tu ama ni kweli tunawekeza kwenye kilimo katika kukuza uchumi wa wananchi takribani asilimia 71 ambao wanategemea kilimo kama msingi mkuu wa maisha yao. Pia mauzo ya mazao nje ya nchi yalipungua kama ifuatavyo: kahawa 36.4%, pamba 24.3%, chai 39.0%, karafuu 47.0%. Hii ni pamoja na ukweli kuwa bei za mazao husika iliongezeka ukilinganisha na mwaka 2009/2010, ila sisi tulishindwa kuitumia fursa hiyo katika kukuza uchumi wa wananchi wetu ambao ni wakulima wa mazao haya kwa kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, ukisoma Taarifa ya Hali ya Uchumi utaona kuwa ni sekta mbili za utoaji huduma na viwanda na ujenzi ndizo zinachangia pato la Taifa kwa asilimia 66.3. Hii maana yake ni kuwa sekta mama ya kilimo ambayo ndiyo inaweza kuwaondolea Watanzania umasikini kwa sasa ina mchango mdogo katika pato la Taifa. Mabadiliko haya ya kimuundo wa uchumi wetu ndiyo sababu kubwa tunakuwa na uchumi unaokua bila kupunguza umasikini.

Narejea kusema kuwa, kwa sasa ukilinganisha na tulipotoka, licha ya kwamba tunahitaji ukuaji wa kasi zaidi wa uchumi, ukuaji siyo changamoto kubwa. Changamoto sasa ni namna gani ukuaji huu wa uchumi unawafikia wananchi. Sekta zinazokuwa kwa kasi ni zile zinazoshawishi uwekezaji wa sekta binafsi kwa urahisi. Sekta ya Kilimo inahitaji uwekezaji mkubwa wa kimiundombinu wa Serikali.

Nchi yetu itaendelea na changamoto ya kupunguza umasikini hadi hapo tutakapoamua kwa dhati kuwekeza katika kukuza uchumi wa vijijini. Kambi ya Upinzani inapendekeza katika bajeti hii mbadala, mikakati maalumu ya kukuza uchumi wa vijijini kwa kuwekeza kwenye miundombinu ya vijijini, umeme vijijini na maji vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011 ukuaji katika shughuli za kiuchumi za madini na uchimbaji mawe uliongezeka na kufikia asilimia 2.7. Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na kuongezeka kwa uzalishaji wa dhahabu na kuongezeka kwa bei ya dhahabu katika Soko la Dunia. Hata hivyo, mchango wa sekta hii pamoja na kuongezeka uzalishaji na bei kuwa kubwa zaidi ya mwaka 2009/2010 bado uliendelea kuwa ule ule wa mwaka 2009/2010 wa asilimia 3.3 pamoja na kuuza nje dhahabu yenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 1,516.6 mwaka 2010/2011. Mauzo haya ya dhahabu nje, kwa mwaka 2010/2011 ni sawa na asilimia 7.1 ya pato la Taifa kwa hesabu za mwaka husika.

Ukiangalia mchango wa Sekta ya Madini kwenye pato la Taifa, mchango kwenye Mapato ya Serikali na Mchango wa sekta katika Mauzo ya nje unaona dhahiri kabisa kuwa bado tunahitaji kufanya kazi ya ziada kuhakikisha Sekta ya Madini inakuwa na mahusiano na sekta nyingine za uchumi *(linkages).* Masuala haya yanahitaji kusimika sera madhubuti *(policy interventions)* ili kulifanya Taifa lifaidike na utajiri wa madini.

Kuboresha sera za kikodi ikiwemo kujenga uwezo wa Wakandarasi wa ndani katika Sekta ya Madini na kuhusisha Sekta ndogo ya Umeme na Sekta ya Madini ni masuala ambayo tunapaswa kuyaamulia wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Hali ya Uchumi inaonyesha kuwa mwenendo wa mfumko wa bei umekuwa ukiongezeka tangu mwezi Oktoba, 2010 kutoka asilimia 4.2 na kufikia asilimia 5.6 mwezi Desemba, 2010, mwezi Januari, 2011 ulikuwa asilimia 6.4 na hadi kufikia mwezi Aprili, 2011 mfumko wa bei ulikuwa umefikia asilimia 8.6. Hii ina maana yake kuwa mfumko wa bei unaongezeka kwa wastani wa asilimia 0.8 kila mwezi. Hali hii inaelezwa kuwa ni kutokana na ongezeko la bei za umeme, gesi na chakula.

Jambo hili ni la hatari katika ukuaji wa uchumi kama hatua za haraka na dharura hazitachukuliwa ili kuweza kukabiliana na jambo hili, kwani kama hali itaendelea kuwa hivyo kwa miezi mitano tu ijayo, mfumko wa bei utakuwa umefikia asilimia 12.6. Serikali imekubaliana na hoja ya Kambi ya Upinzani kwamba itaangalia tozo katika bei za mafuta ili kudhibiti hali hii. Hata hivyo, suluhisho la muda mrefu la kudhibiti mfumko wa bei ni kuzalisha chakula cha kutosha, kwani chakula ni sehemu kubwa ya kikapu cha bidhaa na huduma ambazo Mtanzania anatumia. Ikitokea kuwa bei za mafuta katika Soko la Dunia zikapanda tena na kuyafanya maamuzi yetu ya kikodi hayana maana, kuna haja ya Serikali kuangalia jinsi ya kufidia kupanda kwa bei za umeme kwa asilimia 18 ili kupunguza ukali wa maisha kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, thamani ya Shilingi ya Tanzania imeendelea kushuka ukilinganisha na fedha za kigeni na hii inatokana na kukosekana kwa mikakati thabiti ya kuhakikisha kuwa shilingi inaimarika kwenye soko na hasa kutokana na sera mbovu za kiuchumi na usimamizi usio makini.

Mheshimiwa Spika, thamani ya shilingi ya Tanzania imeendelea kushuka. Leo nilikuwa nasoma gazeti la *Daily News* habari kubwa kabisa ilikuwa *Shilling tumbles to record low.* Naomba kunukuu: *"Hardly a week after the government read its 13.5 trillion budget for 2011/2012 the Tanzanian Shilling has tumbled to the lowest value, we need 25 years history".* Kushuka kwa thamani ya Shilingi licha ya kupanda kwa mauzo yetu nje kwa sekta zote mbili tunazotegemea sana (Madini na Utalii) kunaacha maswali mengi kuhusiana na chaguo letu kuhusu hifadhi ya fedha za kigeni.

Kambi ya Upinzani inaunga mkono ushauri uliotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma kwamba sasa Benki Kuu ya Tanzania ianze kutunza sehemu ya hifadhi ya nchi katika dhahabu. Benki Kuu inunue dhahabu kutoka kwa wachimbaji wadogo na pia tuangalie uwezekano wa kutoza sehemu ya mrahaba katika madini kama dhahabu safi *(pure gold). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, deni la Taifa nalo linaonekana kuongezeka kwa kasi ya ajabu sana na hivyo kupelekea Taifa kuwa na mzigo mkubwa sana wa madeni. Kwa mujibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, deni la Taifa limeongezeka kwa asilimia 38 kutoka shilingi trilioni 7.6 mwaka 2008 mpaka shilingi trilioni 10.5 mwaka 2009 na sasa kwa mujibu wa hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, deni limefikia dola

za Kimarekani bilioni 11.4 ambazo ni sawa na shilingi trilioni 17.1 kwa bei ya dola ya Kimarekani ya Desemba, 2010. Jedwali hapa chini linaonyesha deni la Taifa na malipo ya deni hilo.

Mheshimiwa Spika, Mataifa yote duniani hukopa, sembuse sisi Taifa linaloendelea! Hata hivyo, kasi ya ukopaji wetu sio endelevu hata kidogo na kwa kweli ni mzigo mkubwa kwa kizazi kijacho. Kwa mfano, tunapoangalia bajeti ya mwaka huu, utaona kuwa asilimia 50 ya bajeti itagharamiwa na kodi zetu, lakini asilimia 30 itagharamiwa na mikopo ya ndani, ya nje na ya kibiashara, asilimia 17 misaada na asilimia tatu Makusanyo ya Halmashauri. Hii maana yake ni kwamba asilimia 30 ya gharama za sasa za Serikali itabebwa na kizazi kijacho kwani madeni haya yatalipwa na kizazi kijacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni inapendekeza ufanyike uchunguzi maalumu kwenye deni la Taifa ili Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atuambie madeni haya tunayokopa kwa kasi ya namna hii tunayapeleka kwenye miradi gani (Matumizi ya Madeni) na namna gani tunaweza kudhibiti deni la Taifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, udhaifu katika matumizi ya Serikali, ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mwaka 2009 inaonyesha kwamba katika bajeti iliyopitishwa mwaka 2008/2009 asilimia 25 ya bajeti yote ilitumika vibaya, maana yake ni kwamba katika kila shilingi mia moja ambapo Bunge hili Tukufu linapitisha, shilingi 25 zinakwenda kwenye mifuko ya wezi na wabadhirifu. Hali hii haiwezi kuendelea hata kidogo na ni lazima tuidhibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mifano ya fedha zilizopotea au kutumiwa vibaya katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 ni manunuzi yaliyofanywa nje ya mpango wa mwaka ya jumla ya shilingi bilioni 50.6, malipo yenye shaka ya jumla ya shilingi bilioni 15.5, upotevu wa fedha na mali za Serikali wa jumla ya shilingi bilioni 11.1 na malipo ya mishahara kwa watumishi waliostaafu, waliokufa na watoro kazini ya jumla ya shilingi bilioni 1.8.

Aidha, Mkaguzi hakukabidhiwa nyaraka na orodha ya walionufaika na kiasi cha jumla ya shilingi bilioni 48 *(Stimulus package)* kilichotolewa kwa ajili ya kuchochea ukuaji wa uchumi toka Benki Kuu ya Tanzania katika juhudi za kukabiliana na msukosuko wa uchumi ulioikumba dunia. Katika Mkutano wa Tatu wa Bunge la Kumi, nilimwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu suala la Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kunyimwa nyaraka ili kukagua jumla ya shilingi bilioni 48 zilizotajwa hapo juu.

Natumaini sasa Serikali itakuwa na majibu juu ya suala hili. Kambi inaendelea kusisitiza ombi lililotolewa na aliyekuwa Waziri Kivuli wa Fedha na Uchumi - Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwamba fedha zote zilizotolewa kwa ajili ya *Stimulus Package* zikaguliwe na *CAG* na kuwasilisha taarifa hiyo maalumu Bungeni. Serikali ilikubaliana na ombi hili, hivyo tunaomba taarifa hiyo mara moja.

Mheshimiwa Spika, tunalisema hili la *Stimulus Package* kwa kuwa kuna ushahidi wa barua kutoka kwa Katibu Mkuu Hazina akiwaandikia Mameneja wa Vyama vya Ushirika vya Mikoa ya Kilimanjaro na Kagera akiwaeleza kuwa Serikali pamoja na kuidhinisha kulipwa kwa Vyama hivyo, kwa sasa hakuna fedha kwa ajili ya kufanya malipo hayo.

Barua iliyoandikwa kwa Meneja wa Kagera *Cooperative Union* (1990) *Limited* ya tarehe 16 Septemba, 2010 yenye kumb. Na TYC/B/40/143 ilikuwa ikimweleza Meneja kuhusiana na Serikali kulipa kiasi cha Sh. 734,369,379.49. Ila ilipofika tarehe 27 Aprili, 2011 Katibu Mkuu wa Hazina aliandika barua nyingine kwa Meneja husika yenye kumb.Na.TYC/B/40/143/45 kwa ajili ya kusitisha malipo ya fidia kutokana na mdororo wa uchumi kwa kuwa Serikali haina fedha na pia muda wa kulipa fidia hizo ulikwisha tangu mwaka 2010.

Kuhusiana na Chama cha Ushirika cha Mkoa wa Kilimanjaro *(Kilimanjaro Native Cooperation Union (1984)*, Katibu Mkuu Hazina - Ndugu Ramadhan Kijjah mnamo tarehe 16 Septemba aliandika barua yenye kumb.Na TYC/B/40/143 iliyowajulisha kuwa Serikali imeridhika kuwa wanastahili kupewa fidia ya Sh. 255,107,570.17 waliyopata kutokana na mdororo wa uchumi duniani. Ila ilipofika tarehe 27 Aprili, 2011 Katibu Mkuu huyo huyo aliandika barua nyingine yenye kumb.Na.TYC/B/40/143/43 akiwajulisha kuwa Serikali haina fedha kwa ajili ya kulipa fidia hiyo na kuwa muda wa kulipa fidia ulikuwa umekwisha tangu mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, kupatikana kwa barua hizi ni uthibitisho wa wazi kuwa kuna tatizo kubwa kuhusiana na fedha zilizotolewa na Serikali kwani wakati Naibu Waziri wa Fedha - Mheshimiwa Omar Yusuph Mzee akiwa anajibu swali la msingi la Mheshimiwa Mhonga Saidi Ruhanywa wakati wa Bunge la Bajeti la mwaka 2010/2011 alisema kuwa mpango ulikuwa unakwenda vizuri. Pia wakati Waziri wa Fedha - Mheshimiwa Mkullo akiwa anahitimisha hotuba ya bajeti ya mwaka 2010/2011 alilieleza Bunge hili kuwa Mpango ulikuwa unakwenda vizuri. Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa tunaitaka Serikali ifanye ukaguzi maalum kwenye Mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka wa fedha wa 2011/2012 inapendekezwa kufikia shilingi trillioni 13.5 kutoka shilingi trillioni 11.2 ya mwaka wa fedha unaokwisha wa 2010/2011. Kwa maana ya Shilingi za Kitanzania bajeti inaonekana kukua. Hata hivyo, ukiondoa mfumko wa bei kwa wastani wa 7%, ambao unapunguza uwezo wa kimanunuzi, utaona thamani halisi ya bajeti ni kama shilingi trillioni 12.5 hivi. Ukiibadilisha bajeti kwa dola za Kimarekani ambapo mwaka 2010 ilikuwa ni wastani wa shilingi takribani 1,400 kwa dola moja ya Kimarekani na sasa siku Waziri anasoma bajeti, thamani ya Shilingi ilikuwa na thamani ya Sh. 1,581/= kwa dola moja ya Kimarekani. Utaona kuwa kwa uhalisia *(in real terms)* hakuna nyongeza ya Bajeti. Hivyo, kuna haja kubwa ya kuimarisha sarafu yetu na kudhibiti mfumko wa bei.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 08 Juni, 2011 Waziri wa Fedha - Mheshimiwa Mustafa Mkullo aliwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya

Mapato na Matumizi kwa mwaka 2011/2012. Aliwaeleza Watanzania kuwa bajeti ya mwaka huu ni mahsusi kwa ajili ya masuala yalioyoorodheshwa hapa chini. Nanukuu: "Bajeti ya mwaka 2011/2012 itazingatia vipaumbele vifuatavyo:-

(i) Umeme;

(ii) Maji;

(iii) Miundombinu ya usafiri na usafirishaji (reli, bandari, barabara, viwanja vya ndege, Mkongo wa Taifa);

(iv) Kilimo na umwagiliaji; na

(v) Kupanua ajira kwa sekta binafsi na ya umma.

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri akitaja kuwa kipaumbele cha kwanza ni umeme ukiangalia kwenye vitabu vya bajeti vya Serikali, Wizara ya Nishati na Madini imetengewa jumla ya shilingi bilioni 402.4 kwa mujibu wa Fungu la 58. Fedha hizo zimegawanywa katika mafungu ya matumizi Sh. 76,953,934,000/= na kwa upande wa Bajeti ya Maendeleo zimetengwa Sh. 325,448,137,000/=. Katika hali hii, tunaona kuwa umeme hauwezi kuwa kipaumbele katika bajeti hii kwa kuwa haujapewa uzito unaostahili.

Mheshimiwa Spika, wakati Wizara ya Nishati na Madini inatengewa kiasi hicho cha fedha, ukiangalia fungu lililotengwa kwa ajili ya Hazina *(the treasury)* Fungu 21 zimetengwa jumla ya Sh. 1,054,411,138,000/=. Fedha zilizotengwa kwa Hazina Fungu 21 ni sawa na 8% ya bajeti yote ya Serikali. Wakati Wizara ya Nishati na Madini, *Vote 58* yote imepangiwa fedha za maendeleo shilingi bilioni 325.4, Hazina imepangiwa shilingi bilioni 129 kwa ajili ya matumizi mengine ya kiutendaji *(other operating expenses)* na shilingi bilioni 314 kwa ajili ya matumizi mengine ila yasiyo ya dharura *(contingencies-non emergence).*

Nimemsikia Mheshimiwa Mkullo anasema kuwa Fedha nyingine ya umeme ipo Wizara ya Fedha kupitia *MCC*. Hata hivyo, ukiangalia Fungu 50, fedha za Maendeleo *MCC* zimetengwa shilingi bilioni 111 ambazo hazifikii jumla anayosema Waziri. Zaidi ya hapo, fedha za *MCC* siyo za miradi ya umeme peke yake, ni pamoja na barabara na kadhalika. Ningependa kupata ufafanuzi zaidi ambao unathibitishwa na vitabu vya bajeti na siyo maneno matupu katika hotuba.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya Serikali iliyosomwa na Waziri alisema kwamba na nanukuu Wakati Waziri akisema Bungeni kuwa bajeti ya mwaka 2011/2012 itapunguza posho kama sehemu ya mkakati wa Serikali wa kudhibiti matumizi, nanukuu: "Kupunguza malipo ya posho mbalimbali yasiyokuwa na tija (uk.53), lakini ukweli ni kuwa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2011/2012 zimetenga jumla ya shilingi trilioni 0.987, yaani bilioni 889 ambazo ni sawa na 13% ya bajeti yote ya matumizi ya kawaida ya Serikali na 6% ya bajeti nzima yote kwa ajili ya kulipa posho. Kambi ya Upinzani

inahoji: Je, Waziri atapunguza posho zipi na kwa kiasi gani wakati bajeti inaongezeka mwaka hata mwaka? Tayari ametenga kiasi cha shilingi trilioni 0.987 kwa ajili ya posho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri wa Fedha akisema kuwa ili kudhibiti matumizi, watapunguza posho mbalimbali; wakati huo huo katika hotuba yake uk. 66, anapendekeza kufanywa kwa marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato sura ya 332 na anasema kwenye (i) "Kusamehe kodi ya mapato kwenye posho wanazolipwa wafanyakazi wa Serikali na wanaofanya kazi kwenye Taasisi zinazopata ruzuku kutoka kwenye bajeti ya Serikali." Sasa tumeanza kusikia vilio kutoka sekta binafsi kwamba na wao wapate unafuu huu wa kodi kwenye posho. Kambi ya Upinzani inapendekeza mfumo mzima wa kulipana posho za vikao (*sitting allowances)* uondoke katika utumishi wa umma na jambo hili siyo la CHADEMA, jambo hili siyo jambo la Zitto Kabwe, jambo hili ni jambo la Serikali kwenye Mpango wa Maendeleo wa Serikali ambalo Bunge zima limepitisha jana. Sasa nashangaa sana hoja imekuwa ni kubwa sana imekuwa ni hoja ya Zitto imekuwa ni hoja ya CHADEMA. Hii ni hoja ya Taifa iko kwenye Mpango wa Maendeleo ambao umepitishwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zitto, naomba usome hotuba yako na siyo mawazo yako.

**MHE. KABWE Z. ZITTO - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI WIZARA YA FEDHA:** Ninaomba ieleweke kuwa hatupingi posho za kujikimu ambazo viongozi au maafisa wa umma hulipwa wanaposafiri nje ya vituo vyao vya kazi. Posho hizi zirekebishwe kuendana na gharama za maisha za sasa. Lakini posho za vikao zifutwe mara moja. Ili kuonyesha kuwa Viongozi wa kisiasa tunaelewa kilio cha wananchi kuhusiana na gharama za maisha na kupunguza matumizi ya Serikali, waheshimiwa Wabunge tunaanza na posho za vikao vya Bunge.

Iwapo sisi tukiendelea kujilipa posho za kukaa humu ndani na kwenye Kamati zetu, tunakuwa tunatoa ruhusa kwa Watumishi wa Serikali kulipana posho hizi na hatutakuwa na mamlaka ya kuwahoji na kuwawajibisha. Mfumo wa posho za vikao ni rushwa ya kitaasisi wanaojipa watu wenye mamlaka. Wakati kiongozi wa umma anapolipwa posho kwa kikao cha kufanya maamuzi yanayohusiana na majukumu yake ya kazi ambayo analipwa mshahara, Polisi halipwi posho kwa kulinda, Mwalimu halipwi posho kwa kuingia darasani na wala Nesi halipwi posho kwa kusafisha vidonda vya wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kufanya marejeo ya mfumo wa posho na mfumo wa mishahara kwa watumishi wa umma. Suala hili ni lazima tulianze sasa na katika bajeti hii tunayoijadili. Lazima kuwaonyesha Watanzania kuwa tunajali hali zao ili kurejesha imani ya umma kwa Wanasiasa na viongozi wao.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele sita vilivyotolewa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni:-

Mheshimiwa Spika, fedha zimewekwa katika Shilingi ya Kitanzania shilingi bilioni. Shilingi trilioni 8.361 ni kwa ajili ya sekta sita tu ambayo ni sawa na asilimia 62 ya bajeti nzima. Katika kufanya uchambuzi katika vitabu vya bajeti imeonyesha kuwa hizo sekta sita zimo kati ya mafungu 15 ambayo yamepangiwa fedha nyingi ambayo ni pamoja na deni la Taifa ambalo ni shilingi trilioni 1.9. Hivyo basi, ukiongeza mafungu mengine sita ambayo ni fungu 21, 28, 30, 37, 38 na 57) unapata jumla ya shilingi trilioni.12, 586.11.

Mheshimiwa Spika, jumla ya bajeti nzima kwa mwaka huu ni shilingi trilioni 13, 525.90. Kwa mahesabu ya kawaida ni kwamba kuna tofauti ya shilingi bilioni 939.8 kati ya matumizi kwa sekta za vipaumbele pamoja na Idara nyingine zilizopewa fedha nyingi na bajeti kuu. Mgao wa fedha za Serikali kwa mafungu 15 ya juu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa bajeti hii ni ya nadharia zaidi kwani kwa hali ya kawaida Wizara na Idara za Serikali zilizobakia haziwezi kutumia shilingi bilioni 939.8 tu. Hapa inaonyesha bajeti iliyosomwa na Mheshimiwa Waziri ilikuwa na lengo la kuwafumba macho Watanzania na kuwapa matumaini tu. Hili ni jambo la hatari, kwani mara zote ukweli uliofichwa pindi utakapofichuliwa kwa njia yoyote madhara yake yanakuwa ni makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, licha ya uchambuzi hapo juu utagundua kirahisi kabisa kuwa Waziri wa Fedha amelundika fedha za miundombinu kwa pamoja ili kuhadaa umma. Ukiangalia vitabu vya bajeti utaona kuwa katika shilingi trilioni 2.8 zilizotengwa kwa miundombinu, shilingi trilioni 1.5 ni kwa Wizara ya Ujenzi peke yake na kuacha fedha nyingine kwa Wizara zilizobakia. Utaona kuwa Wizara ya Uchukuzi inayosimamia sekta nyeti kama reli, bandari, usafiri wa majini na Shirika la Ndege la Taifa imetengewa fedha kidogo sana ambazo ni shilingi bilioni 69 kwa matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 167 kwa maendeleo. Shirika la Ndege, Shirika la Reli na Shirika la Usafiri Majini *(MSCL)* hayajatengewa fedha za kuweza kuyafanya mashirika haya yaanze kazi mara moja kwa ufanisi na kutengeneza faida miaka ya usoni.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikali ya mwaka 2011/2012 imewaongezea mzigo mkubwa sana wananchi na hasa wajasiriamali wadogo na vijana ambao wamejiajiri ama kuajiriwa kwenye biashara ya usafiri na usafirishaji. Kwani Serikali inapendekeza kufanyika kwa marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani Sura 168 ili kuongeza ukomo wa kiwango cha faini inayotozwa kwa kufanya makosa wakati akiwa anaendesha gari, yaani *(Traffic Notification Fee)* kutoka Sh. 20,000/= hadi Sh. 300,000/=. Ingawa Waziri alitamka kwa maneno kuwa faini itakuwa Sh. 50,000/=, kwenye kitabu cha hotuba yake ni Sh. 300,000/=. Kambi ya Upinzani haipingi adhabu kwa wakosaji wa makosa barabarani isipokuwa tuna wasiwasi kuwa adhabu hii itasababasha rushwa kuongezeka. Ila ikisimamiwa vizuri itapelekea kupunguza ajali barabarani.

Mheshimiwa spika, ongezeko hili la faini ni kubwa sana na litawaangamiza kabisa kibiashara vijana ambao wamejiajiri kwenye biashara ya usafirishaji kama vile daladala, taxi, bajaji na pikipiki. Kambi ya Upinzani inapinga marekebisho haya ya sheria

kwani yataathiri maisha ya Watanzania wengi ambao watakuwa sasa kila mara wanafanya kazi kwa ajili ya kulipia faini Polisi badala ya kuweza kukuza uchumi wao. Kwa mfano, kama dereva wa pikipiki atakutwa na makosa matatu, mathalani la kusahau leseni, kutovaa helmenti na kutovaa vazi maalum kwa ajili ya kuendesha pikipiki, atapaswa kutozwa faini ya Sh. 900,000/= ambazo ni sawa na gharama ya kununua pikipiki nyingine mpya.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikali ya mwaka 2011/2012 haijalenga katika kuimarisha uchumi kwani fedha zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo ni kiasi cha shilingi trilioni 4,925 tu na kati ya fedha hizo shilingi trilioni 1,871 ni fedha za ndani na nyingine zilizobakia kiasi cha shilingi trilioni 3,054 ni fedha za nje. Hivyo basi, kama wahisani hawatatoa fedha kama ambavyo hali hiyo imekuwa ikitokea mara kwa mara ni kuwa maendeleo hayataweza kupatikana, kwani hakuna fedha kwa ajili ya kuendesha miradi mbalimbali ya kimaendeleo.

Kambi ya Upinzani, inaona kuwa Serikali bado haijaamua kuliondoa Taifa hili katika lindi la umasikini kwani hatutengi fedha zetu za ndani kwa ajili ya maendeleo, badala yake fedha za ndani tunatenga kwa ajili ya shughuli za kawaida ambazo siyo za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, bajeti mbadala ya Kambi ya Upinzani, zifuatazo ni dondoo za Bajeti Kivuli inayotolewa na Kambi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Spika, zifuatazo ni dondoo za Bajeti Mbadala za Kambi ya Upinzani:-

- Kuongeza mapato hadi kufikia Shilingi trilioni 14.160 kutoka trilioni 13.525 za Serikali;

- Tumeongeza mapato ya ndani hadi shilingi trilioni 8.68 kutoka shilingi trilioni 6.7 za Serikali;

- Tumeondoa kukopa mikopo ya kibiashara na hii inatokana na ukweli kwamba kufanya hivyo ni kuliongezea Taifa gharama za kulipa madeni yenye riba kubwa na pia hili linafanya uchumi;

- Kuathirika kwani Serikali inakuwa ikishindana na sekta binafsi katika kuchukua mikopo kwenye Taasisi za Fedha na hivyo kuathiri uchumi;

- Tumeondoa posho mbalimbali ambazo ni shilingi trilioni 0.987 na kuzipeleka kwenye kuboresha mishahara ya Watumishi wa Umma na katika bajeti ya maendeleo;

- Tumepunguza matumizi ya kawaida ya Serikali kutoka shilingi trilioni 8,600,286 na kuwa shilingi 7.913;

- Tunapendekeza kuwekeza fedha za kutosha kwenye sekta ya umeme na gesi ili kumaliza kabisa tatizo la nishati ya umeme. Vilevile kuchochea matumizi ya gesi majumbani; *(Makofi)*

- Tutakusanya mapato ya ndani kwa 22.84% ya pato la Taifa ukilinganisha na Serikali ambao watakusanya 17%;

- Tutapunguza misaada na mikopo kutoka nje na kuwa 27.54 % ya bajeti wakati ya Serikali ni 29%, Waziri wa Fedha amesema asilimia 17, lakini mikopo na misaada ni asilimia 29 ya bajeti, misaada peke yake ndiyo asilimia 17;

- Kutoka vyanzo vipya vya mapato, tumeongeza shilingi trilioni 1.905 ambavyo ni vyanzo havikusanywi na Serikali na kupanua wigo wa kodi na kurekebisha sheria za kuzuia ukwepaji wa kodi (*anti tax avoidance measures)* na kuboresha mfumo wa kodi; na

- Tunapendekeza kurahisisha mfumo wa Kodi ya Mapato *(Personal Income Tax)* na kwamba sasa kila Mtanzania ajaze fomu za kodi *(tax returns)* kwa mujibu wa sheria hata kama hana kipato.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza mapato ya nchi kutoka katika bidhaa za misitu, tunapendekeza kwamba tudhibiti mfumo wetu wa bidhaa za misitu zinazouzwa nje. Wizara ya Maliasili na Utalii inabidi iliangalie suala hili na Waziri kivuli wa Maliasili na Utalii atalitolea ufafanuzi zaidi na katika kuhakikisha kuwa bidhaa mbalimbali zitokanazo na misitu kama vile mbao, madawa, magogo na asali zinatumika kikamilifu katika kuliongezea Taifa kipato, hatua zifuatazo zitachukuliwa:-

(i) Kuhakikisha kuwa magogo yote yanayosafirishwa nje ya nchi yanalipiwa kodi. Tunashauri kuimarisha usimamizi bora wa uvunaji wa bidhaa hizi za misitu na kuifanya Idara ya Misitu na Nyuki kuwa Wakala wa Serikali. Juhudi zitawekwa katika kuhakikisha kwamba bidhaa nyingi za misitu zinatumika hapa nchini kuzalisha Fenicha kufuatia amri ya kutonunua Fenicha kutoka ughaibuni.

(ii) Kutafuta soko la uhakika la asali kwa ajili ya kupata fedha za kigeni kwenye masoko ya Ulaya na Marekani kwani yametawaliwa na asali kutoka nchi za Amerika ya Kusini kama Brazili na Argentina. Lengo la kuongeza juhudi katika eneo hili ni kusaidia jamii za warina asali kupata soko na nchi kufaidika na kodi na pia mauzo nje na hivyo kupata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi amezungumza suala la kupunguza misamaha ya kodi kwa undani kabisa na wala sina sababu ya kuliongelea tena kwa sababu nitakuwa ninapunguza uzito wa Kamati ya Fedha na Uchumi jinsi ilivyolipendekeza. Kiwango cha misamaha ya kodi zinazotolewa na Tanzania ni kikubwa mno. Hii inaonekana wazi kwa kulinganisha kiwango cha

misamaha ya kodi kinachotolewa Tanzania na kile kinachotolewa katika nchi za Uganda na Kenya.

Nchini Tanzania kati ya miaka ya 2005/2006 na 2007/2008 misamaha ya kodi ilikadiriwa kuwa wastani wa asilimia 3.9 ya pato la Taifa. Mwaka 2008/2009 misamaha ya kodi ilikuwa asilimia 2.8 ya pato la Taifa na mwaka 2009/2010 asilimia 2.3. Ukilinganisha na Kenya na Uganda misamaha ilifikia asilimia moja na 0.4 ya pato la Taifa la kila nchi husika kwa mtiririko huo.

Mheshimiwa Spika, kama Tanzania ingerekebisha viwango vya misamaha ya kodi ili kulingana na kiwango kilichofikiwa na Kenya, zaidi ya shilingi bilioni 600 zingeokolewa kwa mwaka 2007/2008 peke yake. Ukubwa wa kiwango cha misamaha inayotolewa unaweza kuelezewa kwa kukilinganisha na malengo ya ukusanyaji wa mapato ya kodi ambayo Tanzania inashindwa kuyafikia. Katika mwaka 2008/2009 na 2009/2010 Serikali haikutimiza lengo lake la mapato kwa wastani wa shilingi bilioni 453 kila mwaka. Katika kipindi hicho hicho, misamaha ya kodi iliyotolewa ilifikia wastani wa shilingi bilioni 724 kwa mwaka. Mpaka mwaka 2011 mwezi Juni, msamaha wa kodi unakadiriwa kuwa shilingi bilioni 930 kwa mujibu wa Taarifa ya *TRA* kwa Kamati ya Fedha na Uchumi.

Kama misamaha ya kodi ingetolewa katika kiwango kinachofanana na kiwango cha misamaha ya kodi inayotolewa Kenya, shilingi bilioni 484 zingeokolewa mwaka 2008/2009 na shilingi bilioni 302 mwaka 2009/2010. Kwa maneno mengine, upungufu katika ukusanyaji wa mapato ungepunguzwa kwa kiasi kikubwa. Kambi ya Upinzani inaipongeza Serikali kwa kukubali wazo la kupunguza misamaha ya Kodi mpaka kufikia asilimia moja ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kambi ya Upinzani inapendekeza kupitia upya vivutio vinavyotolewa na *TIC* kwa wawekezaji kwa kupiga marufuku msamaha wowote wa kodi kwa bidhaa zinazozalishwa nchini ili kulinda viwanda vya ndani, hiyo iwe ni marufuku kabisa bidhaa yoyote ambayo inazalishwa Tanzania kutolewa msamaha wa kodi kuagizwa kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini na Makampuni ya kimataifa *(multinationals)* katika tathmini ya Hali ya Uchumi ya mwaka 2010 tumeonyesha ni namna gani ambavyo Sekta ya Madini imekuwa haichangii mapato ya ndani. Katika Mwaka huu wa Fedha, Taifa letu litakusanya shilingi bilioni 99.5 kutoka katika mrahaba kwenye Madini yanayochimbwa nchini kwetu. Mapato haya ya mrahaba kwa mwaka ujao wa Fedha ni asilimia 4.5 tu ya mauzo ya dhahabu peke yake nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kodi nyingine zinazokusanywa kutoka katika Sekta ya Madini inakuwa ni vigumu kuweza kujua kiasi gani tunakusanya, kwani Kampuni zote zinalundikwa katika kapu moja la Idara ya walipa kodi wakubwa. Kwa takwimu za mwaka 2009/2010 mapato yote ya kikodi pamoja na mrahaba na malipo kwa mifuko ya pensheni (ambayo siyo kodi) katika Sekta ya ya Madini yalikuwa takribani

shilingi bilioni 256 ambazo zilikuwa sawa na asilimia 16 ya thamani ya mauzo ya madini nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya kuhakikisha Taifa linakusanya mapato ya kutosha katika Sekta ya Madini ili kuleta maendeleo ya wananchi wetu. Katika kuhakikisha kuwa tunaongeza ukusanyaji wa mapato ya kutosha kutokana na Sekta ya Madini na makampuni ya kimataifa, tutachukua hatua kadhaa.

Mheshimiwa Spika, Makampuni makubwa ya kimataifa *(MNC)* hutumia mbinu mbalimbali kupunguza kodi wanazolipa kwenye nchi zinazoendelea. Nchi yetu imekuwa ikikaribisha wawekezaji wakubwa kwenye maeneo mbalimbali hasa sekta za Madini na Mawasiliano. Hata hivyo, kwa muda mrefu wa uwekezaji, wao wamekuwa wakipata misamaha ya kodi na pia kutolipa kodi ya makampuni ama kodi ya *capital gains* wanapouziana makampuni hayo.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri ni wa kampuni za madini ambazo hutumia sehemu kubwa ya uwekezaji wao kama mkopo *(debt financing).* Njia hii huwezesha wawekezaji *(shareholders)* kupata faida *(return)* mapema zaidi kuliko kuweka mtaji *(share holders equity).* Hii inatokana na ukweli kwamba riba huondolewa katika kukokotoa kodi ambayo kampuni hulipa. Katika kipindi cha kati ya mwaka 2001-2009 kiwango cha kodi ambacho kingelipwa Serikalini iwapo makampuni ya madini yangewekeza mtaji wa angalau 30% ya uwekezaji wao wote kwenye migodi yao kingelikuwa takribani dola za Kimarekani milioni 830. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mifano ya asilimia ya mikopo katika mitaji ya makampuni ya madini hapa nchini ni kama ifuatavyo (Chanzo *Masha Mining Review Report*):-

*(i)* *Geita Gold mine* – 12,597,000 %

*(ii)* *Bulyanhulu Gold mine* – 791%

*(iii)* *Resolute Gold mine* – 5088%

Mheshimiwa Spika, utaona kuwa kwa muundo huo wa mitaji ya Makampuni haya matatu tu ni namna gani ambavyo sehemu kubwa ya fedha zinazotokana na faida wanayopata kwenye mauzo ya dhahabu huishia kulipia madeni na riba na hivyo kukosesha Serikali mapato. Hii kwa wataalamu wa kodi inaitwa '*tax planning measures'*. Muundo huu wa mitaji ya uwekezaji itapelekea makampuni haya kutangaza hasara kila mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kwenye Sekta ya Mawasiliano, kampuni ya *Celtel International* ilifungua kampuni huko *Netherlands* (Celtel Tanzania BV) ambayo ndio inamiliki *Celtel* Tanzania *Limited*.

Hivyo, uuzaji wa *Celtel* kwenda *Zain* na baadaye kwenda *Airtel* haukulazimisha kubadilishwa kwa mmiliki wa *Celtel Tanzania limited* na hivyo kwa kutumia mikakati ya

kiumiliki *(ownership structure)* kila mara kampuni hii ilipouzwa Serikali haikuweza kukusanya kodi yake. Kwa mfano, kwenye mauzo ya *Zain* kwenda *Airtel* Serikali ingeweza kukusanya dola za Kimarekani milioni 312, ambazo hazikukusanywa.

Mheshimiwa Spika, kwenye Sekta ya Viwanda, Kampuni ya Bia Tanzania ambayo inamilikiwa na *SABMILLER* nayo pia imeripotiwa kutumia njia ya kimkakati kukwepa kodi ikiwemo kusajili hatimiliki na hivyo kupata mrahaba ambao hautozwi kodi. Mfano ni kwenye pombe aina ya CHIBUKU ambapo jina hilo limesajiliwa huko *Netherlands* na kampuni tanzu ya *TBL*. Inasemekana Tanzania imepoteza karibu dola milioni mili kila mwaka kutokana na mpango huo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni tunapendekeza hatua zifuatazo ili kuweza kukabiliana na ukwepaji huu wa kodi na hatimaye kuliongezea Taifa mapato:-

(i) Kutunga sheria kwa kuimarisha zaidi Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 kwamba, mikopo ya makampuni kwenye uwekezaji, kwa sababu za kikodi, isizidi asilimia 70 ya mtaji wote uliowekezwa na hii ianze mara moja bila kujali mikataba iliyopo;

(ii) Kutunga sheria kuhakikisha kwamba riba kwenye mikopo kutoka Makampuni yanayohusiana haitaondolewa kwenye kutoza kodi; na

(iii) Kuhakikisha kwamba mauziano ya Kampuni yoyote ambayo mali zake zipo Tanzania tunakusanya kodi ya 30 % kama ongezeko la mtaji (*capital gains*). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapongeza hatua ya Serikali kuchukua wazo la Kambi ya Upinzani la kupunguza Kodi na tozo kwenye bidhaa za mafuta ili kupunguza bei ya bidhaa hizi na hivyo kupunguza ukali wa maisha kwa wananchi. Ingawa Serikali haijasema kiwango cha kodi kitakachoondolewa, tunapendekeza kuwa ushuru wa barabara *(road toll)* usipunguzwe ili kubakia na Fedha za kutosha kukarabati barabara ambazo tunazijenga kwa kasi. Tunapendekeza ushuru wa bidhaa za mafuta upunguzwe kwa asilimia 40 na tozo nyingine zote kwenye mafuta zipunguzwe kwa asilimia 40 pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapendekeza pia kufuta kabisa msamaha wa kodi kwenye mafuta kwa Kampuni za Madini na Kampuni za Ujenzi kwani imethibitika kuwa msamaha huu unapelekea upotevu mkubwa wa fedha za umma. Takwimu zinaonyesha kuwa kupitia misamaha hii, jumla ya lita milioni 133 za dizeli ambazo ni sawa na asilimia 20 ya dizeli yote iliyoingizwa nchini, ziliingizwa nchini na Kampuni tano za Migodi ya Dhahabu na Kampuni hizi zililipa dola 200,000 tu kama ushuru. Mafuta mengi yanayoingia kupitia msamaha huu hurudi kwenye soko na kuuzwa reja reja. Misamaha hii ifutwe bila kujali mikataba iliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni inapinga pendekezo la sasa la kuondoa msamaha wa kodi ya mafuta kwa kampuni za utafutaji ya mafuta na gesi.

Msamaha huu hauna mantiki kwani Kampuni za utafutaji mafuta na gesi kwa mujibu wa mikataba yao *(Production Sharing Agreements)* wataweza kurejeshewa gharama hizi mara baada ya mafuta na gesi kupatikana *(Cost Oil).* Mfumo wa mikataba ya mafuta na gesi ni tofauti na mfumo wa mikataba ya madini na *risk* ya wao kuja kuwekeza, nchi ndiyo *risk* kubeba pamoja na kulipia kodi hizi.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema hapo juu, hatua hii ya kikodi ni ya dharura tu, kwani bado inaweza kufanywa haina maana yeyote kwa kitendo cha bei za mafuta kupanda katika Soko la Dunia. Hivyo, tunahitaji njia endelevu nayo ni kuhakikisha mafuta yanaagizwa kwa wingi na hivyo kupunguza gharama za usafirishaji. Mpango wa *Bulk Procurement* umekuwa ukisemwa bila kutekelezwa kwa muda mrefu kutokana na nguvu kubwa ya rushwa waliyonayo matajiri katika Sekta ya Mafuta. Ni lazima tuishinde nguvu hii hata kama itakuwa ni kwa baadhi yetu kupoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni inapendekeza Serikali kupitia Shirika la Umma la Mafuta (baada ya kurekebisha *TPDC* na kuwa na Mamlaka ya Udhibiti katika kutafuta na kuchimba mafuta na gesi na Shirika la Kibiashara la Mafuta na Gesi), inunue hisa asilimia 50 zilizobakia za *BP (T) Limited,* kuweka mtaji wa kutosha na kufanya biashara ya Mafuta. Nchi nyingi duniani hutumia mashirika yake ya umma kwenye Sekta ya Mafuta kudhibiti bei. Ukienda Dubai leo, Vituo vingi vya Mafuta vinamilikiwa na Shirika la Umma. Vilevile Malaysia licha ya *Petronas* kushirikia katika kuchimba mafuta, lakini pia inamiliki Vituo vya Mafuta vya reja reja.

Hii ndiyo hatua muafaka ya kuchukua, ipo ndani ya uwezo wetu na itaongeza ushindani katika soko na hivyo kudhibiti upandaji wa bei holela wa bidhaa za mafuta. Kwa ufupi, tunashauri *BP (T) Limited* imilikiwe na Serikali kupitia Shirika la Umma kwa asilimia 100 badala ya asilimia 50 ya sasa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni inapendekeza pia kuwianisha viwango vya bei ya Mafuta ya Taa na bei ya mafuta ya diseli na petroli ili kudhibiti uchakachuaji wa mafuta ambao unaligharimu Taifa fedha nyingi sana na kuleta uharibifu mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kupanda kwa gharama za maisha kwa wananchi kumepunguza uwezo wa matumizi wa wananchi walioajiriwa na kulipwa mishahara ambayo inakatwa kodi (*PAYE).* Tunatambua kuwa kodi hii ni chanzo kikubwa cha Mapato kwa Serikali ambapo kwa mwaka huu wa fedha kinatarajiwa kuingiza takribani shilingi bilioni 450 kutoka Idara ya Kodi za Ndani na Idara ya Walipa kodi Wakubwa. Hata hivyo, kuna haja ya kuangalia upya *(tax brackets)* na kuzirahisisha kwa kuzipunguza na hata kuanza kufikiria kama kuna haja ya kuwa na Kodi Mfuto, yaani *flat tax.*

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu wa fedha tunapendekeza Sheria ya Kodi ya Mapato ifanyiwe marekebisho na kushusha kiwango cha chini kabisa cha *PAYE* mpaka 9% na kiwango cha juu mpaka 27%. Uamuzi huu utawezesha wananchi kubakia na fedha

na hivyo kutumia katika uchumi na kukuza uzalishaji. Uamuzi huu utapunguza mapato ya Serikali kwa takribani shilingi bilioni 23 (4% ya matarajio ya makusanyo ya kodi hii).

Mheshimiwa Spika, vile vile Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa mchakato uanze ili kila Mtanzania awe anajaza fomu za kodi *(tax returns)* kila mwaka. Kuna watu wengi sana ambao wanapata mapato makubwa lakini hawalipi kodi. Mfano, watu wenye nyumba za kupangisha mijini wanapata fedha nyingi sana na wengine hutoza kodi za pango kwa kutumia dola za Marekani lakini hawalipi kodi ya Mapato. Watu hawa hutumia barabara na huduma nyingine za umma ambazo gharama zake zinatokana na kodi ilhali hawalipi kodi. Kambi ya Upinzani inapendekeza kuanzishwa kwa *Real Estate Regulatory Authority* na kwamba kila mwenye nyumba ya kupangisha lazima atambuliwe na kulipa kodi inavyostahili.

Kambi ya Upinzani Bungeni inataka kila Mtanzania mwenye kipato alipie kodi ya kipato chake. Kulipa kodi ndiyo ishara ya Uzalendo na ili raia aweze kuinyooshea kidole Serikali yake lazima awe na uchungu na uchungu unapatikana kwa kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya hatua ambayo imekuwa ikizungumzwa siku zote ni kupanua wigo wa kodi. Waheshimiwa Wabunge wa Kambi zote mbili na hata wataalamu mbalimbali wanarejea sana jambo hili. Imefikia wakati sasa kutekeleza jambo hili kwa vitendo kwa kuondoa vikwazo vinavyofanya biashara ndogo na za kati (*SMEs)* zisiandikishwe. Biashara ndogo na za kati zinaunda sehemu kubwa ya shughuli za kiuchumi nchini na hivyo kuwa moja ya chanzo kikubwa cha mapato ya Serikali.

Katika utafiti uliofanywa na Shirika la *Serengeti Advisers Limited* imeonekana kuwa licha ya maboresho yanayofanywa na *TRA,* bado wafanyabiashara wadogo na wa kati wanakutana na vikwazo vingi sana. Baadhi ya vikwazo ni pamoja na vitisho kutoka kwa Maafisa wa *TRA*, urasimu na hata rushwa. Pamoja na vikwazo hivyo, bado wafanyabiashara wadogo wadogo wamekuwa wakichangia kwa kiasi kikubwa kupitia kodi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba ushauri wa Mradi wa kuboresha mfumo wa kodi *(Tax Modernisation Project)* ambao ulishauri kwamba kuna haja ya kuainisha Kodi ya *VAT* na *Presumptive Tax* utekelezwe. Tungeshauri kuwa kodi anayotozwa mfanyabiashara ndogo ndogo kabla hajaanza kufanya biashara ifutwe kabisa. Uamuzi huu utapunguza mapato ya Serikali (Shilingi bilioni 18 kwa mujibu wa kitabu cha Bajeti Vol. I) katika kipindi cha muda mfupi lakini itakuwa ni chanzo kikubwa sana cha mapato katika kipindi cha muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni inaona kurejeshwa kwa ada ya leseni kwa biashara ndogo ndogo licha ya kuongeza mapato ya Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji kutarejesha ugumu wa kufanya biashara. Madhumuni ya kuondoa leseni yaliyofanywa mwaka 2003 bado yana maana. Tunashauri uamuzi huu uangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza kufutwa kwa msamaha wa kodi kwenye orodha ya misamaha kwa nyaya za umeme *(removal of duty remission on electric wires and cables (as deemed capital goods) through Tanzania Certificate of Incentive scheme administered by TIC).* Uamuzi huu utalinda viwanda vya ndani na kulinda ajira za Watanzania walioajiriwa kwenye viwanda vinavyotengeneza nyaya za umeme.

Mheshimiwa Spika, katika sera ya mapato, viwango hivyo vikirekebishwa tutakusanya shilingi trilioni 1.9 zaidi ya fedha ambazo zimekusanywa mwaka huu.

Muhtasari wa vyanzo nyongeza vya mapato kwa bajeti mbadala ya mwaka 2011/2012:-

(1) Kurekebisha Kodi katika Misitu shilingi bilioni 100;

(2) Kurekebisha misamaha ya kodi shilingi bilioni 658;

(3) Mauzo ya hisa za Serikali shilingi bilioni 550;

(4) Kurekebisha Kodi Sekta ya Madini shilingi bilioni 240;

(5) Kuimarisha usimamizi wa mapato ya Wanyamapori shilingi bilioni 81;

(6) Kuondoa msamaha wa ushuru wa mafuta Kampuni za Madini shilingi bilioni 59;
(7) Usimamizi wa Mapato katika Utalii shilingi bilioni 68; na

(8) Kuimarika kwa Biashara na *EAC* shilingi bilioni 150.

Mheshimiwa Spika, jumla ni shilingi bilioni 1,905.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele vya bajeti ya Matumizi ni:-

(i) Ukuaji wa uchumi vijijini *(rural growth)* kwa kuboresha miundombinu ya umeme, barabara na maji. Tunapendekeza kutumia shilingi bilioni 450 kila mwaka (shilingi bilioni 150 kwa kila sekta) kwa miaka mitano mfululizo katika sekta hizi vijijini, tunataka ku-*pump* fedha kwenye uchumi wa vijijini. Ujenzi wa barabara za vijijini utatumia kwa kiasi kikubwa nguvukazi watu *(labour intensive)* ili kuongeza kipato na kukuza matumizi ya kaya vijijini kufikia lengo la kupunguza umasikini wa vijijini mpaka asilimia 20 kutoka asilimia 37 ifikapo mwaka 2015.

(ii) Tunatenga shilingi trilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa barabara na madaraja. Fedha hizi na miradi hii ikifanywa na makampuni ya kigeni zote zinakwenda nje. Tunataka zibaki ndani ya uchumi wetu.

(iii) Nishati (umeme na gesi asilia) kuhakikisha tunazalisha 360MW za umeme kila mwaka ili kufikia malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Pia kuwekeza katika bomba la gesi kutoka Mtwara, matumizi ya gesi kwenye nyumba za Dar es Salaam na mtambo wa kutengeneza gesi *(LPG extraction Plant).*

(iv) Raslimali watu (kuboresha Elimu na afya).

(v) Kuongeza kima cha chini cha mshahara kwa wafanyakazi wa umma mpaka Sh. 315,000/= kwa mwezi na kutoa motisha kwa Walimu wanaofundisha vijijini kwa kuwapa mshahara mara moja na nusu ya wenzao wanaofundisha mijini. Tunapendekeza kupunguza matumizi ya Serikali kwa kuhakikisha kwamba Mawaziri, Wakurugenzi na makatibu Wakuu wanatumia magari yao binafsi, wakopeshwe kila miaka mitano wasitumie magari ya Serikali na magari ya Serikali yote yaliyopo hivi sasa wanayotumia viongozi wanaostahili magari, yapigwe mnada, yauzwe.

(vi) Uchukuzi (reli, bandari na Shirika la ndege).

(vii) Kujenga uwezo wa wakandarasi wa ndani kwa kurekebisha sheria mbalimbali ili kuhakikisha kuwa: (i) Miradi yote ya ujenzi nchini isiyozidi shilingi bilioni 30 iwe ni kwa ajili ya Watanzania tu na kama Mtanzania hana uwezo ataalika mgeni kwa mapenzi yake mwenyewe; (ii)Miradi yote ya ujenzi inayozidi shilingi bilioni 30 itakuwa wazi kwa zabuni za ndani na nje, hata hivyo Kampuni ya kigeni itakayopata zabuni ni lazima iwe na ushiriki wa Mtanzania kwa angalau asilimia 30; na (iii) Vifaa vyote vya ujenzi na hasa vile vinavyozalishwa nchini vinunuliwe nchini na itakuwa ni marufuku kwa Kituo cha Uwekezaji kutoa ruhusa ya msamaha wa kodi kwa makampuni ya uwekezaji kwa bidhaa zinazozalishwa nchini na itakuwa ni marufuku kwa Kituo cha Uwekezaji kutoa ruhusa ya msamaha wa kodi kwa makampuni ya uwekezaji wa bidhaa zinazozalishwa nchini na hasa saruji.

Lengo la hatua hii ni kuhakikisha fedha za miradi mikubwa ya maendeleo ya ujenzi zinabaki nchini na kuchochea ukuaji wa uchumi wa Watanzania, kuongeza ajira na uzalishaji viwandani.

(viii) Pensheni ya uzeeni.

(ix) Tunapendekeza kuondoa ada kwa wanafunzi wa Shule za Sekondari za kutwa na kupunguza ada kwa Sekondari za bweni kwa kiwango cha asilimia 50 kwa wavulana na bure kwa wasichana. Kwa kuwa kuna wanafunzi 1.6m katika Shule za Sekondari nchini, gharama za shilingi bilioni 32 zitakazopotea zitalipwa na Serikali kutoka vyanzo vipya vya mapato.

(x) Kuuza nje bidhaa za kilimo na mifugo zilizoongezewa ubora.

(xi) Kupunguza mzigo wa matumizi ya magari ya Serikali kwa kuweka mfumo wa viongozi na watumishi ambao stahili zao zinapaswa kupewa magari watakopeshwa magari na kupewa posho ya mafuta. Magari kadhaa yatawekwa *pool* na mengine yote

yatapigwa mnada. Benki Kuu ya Tanzania tayari inatumia mfumo huu ambapo hata Gavana wa Benki Kuu sasa amekopeshwa gari. Tunatumia uzoefu wa Taasisi hii ya Serikali kwa Idara zote za Serikali, Mawizara, Mikoa, Mashirika ya Umma yanayopata ruzuku ya Serikali na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kama Taifa tumezindua Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano 2011/2012 – 2015/2016 na jana Bunge lako Tukufu limeupitisha pamoja na mapendekezo yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Mpango unahitaji wastani wa Shilingi Trilioni 8.6 kila mwaka ili kuutekeleza, na fedha zote hizi za utekelezaji wa Mpango huu ni fedha za bajeti ya maendeleo. Katika bajeti iliyosomwa na Waziri wa Fedha - Mheshimiwa Mkullo bajeti ya maendeleo ni shilingi trilioni 4.9 tu ambayo ni sawa na asilimia 36.3 ya bajeti yote ya Serikali kwa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, ili kuanza kutekeleza Mpango wa Maendeleo kuanzia mwaka huu wa fedha, na iwapo tungesema fedha zote za maendeleo mwaka huu zitekeleze Mpango huu, ingekuwa ni asilimia 56.9 ya fedha zinazohitajika kuutekeleza Mpango kwa mwaka. Hii inaonyesha kuwa Serikali haina nia ya dhati ya kuutekeleza Mpango huu wa kitaifa. Kushindwa kutenga fedha za kutekeleza Mpango huu kwa mwaka huu, kutapeleka mzigo mkubwa wa bajeti ya Mpango huu katika mwaka ujao wa fedha. Kambi ya Upinzani inaona kuwa kuna ulazima wa kuanza kutekeleza baadhi ya miradi ya maendeleo katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri wa fedha Mheshimiwa Mustafa Mkullo akitaja kuwa kipaumbele cha kwanza cha bajeti ya mwaka huu ni kumaliza tatizo la Umeme na hivyo kutamka kwamba ametenga shilingi bilioni 537, upembuzi uliofanywa na Kambi ya Upinzani kwenye vitabu vya bajeti (Kitabu Namba II na IV fungu la 58) vilivyotolewa na Serikali, umebaini kuwa Wizara ya Nishati na Madini imetengewa jumla ya shilingi bilioni 402.4 tu. Fedha hizo zimegawanywa katika mafungu ya matumizi ya kawaida shilingi bilioni 76.95 na kwa upande wa bajeti ya maendeleo zimetengwa shilingi bilioni 325.4. Shilingi bilioni 325 zilizotengwa katika Bajeti ya Maendeleo ya Wizara ya Nishati na Madini zinatosha kwa mradi mmoja tu wa umeme wa 160MW, 100 Dar es Salaam na 60 Mwanza. Hakuna mradi wowote mpya wa umeme unaoonekana katika Bajeti hii. Waziri wa Fedha amesema kwamba fedha nyingine ziko *MCC*.

Tumeangalia *Vote* 50 *MCC* tumekuta kuna shilingi bilioni 111 tu na *MCC* siyo fedha za umeme peke yake ni pamoja na barabara, maji na kadhalika. Kwa hiyo, taarifa ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameitoa tunaomba aifanyie marekebisho. Tunahitaji fedha za kutosha kwenye umeme.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia malengo ya Mpango wa kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano, katika uzalishaji umeme ambapo kama Taifa tumepanga kuzalisha megawati 1788 za ziada kutoka MW 1034 *(installed capacity)* zilizopo sasa, tunahitaji kuzalisha wastani wa MW 358 kila mwaka kwa miaka mitano. Hivyo basi, ukiondoa mradi wa MW 160 ambao tayari umeanza na umetengewa fedha katika bajeti ya mwaka huu, tunahitaji mradi mwingine wa angalau MW 200 ndani ya mwaka huu wa fedha.

Mradi ambao unaweza ukatekelezwa kwa haraka ni mradi wa Kiwira awamu ya kwanza MW 200.

Taasisi za *NSSF* na *STAMICO* zimeonyesha nia ya kutekeleza mradi huo bila kutegemea fedha ya bajeti ya Serikali. Kambi ya Upinzani inapendekeza mradi huu kuingizwa katika utekelezaji ndani ya mwaka huu wa fedha. Kambi ya Upinzani pia inapendekeza kutenga fedha za ndani kutekeleza mradi wa njia za kusafirisha umeme kutoka Kiwira mpaka Mbeya na usambazaji huu utekelezwe na *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, miradi iliyosalia ya Mchuchuma na Ngaka (Makaa ya Mawe), Mtwara – Somanga Fungu na Kinyerezi (gesi asilia) na Ruhudji (Maji) ielekezwe kwa Taasisi zilizoainishwa kwa ajili ya utekelezaji na Serikali kuingia makubaliano na taasisi hizo ili kuhakikisha utekelezaji wake unafanyika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, madhara ya ukosefu wa umeme kwenye Uchumi wa Taifa ni makubwa sana. Mamlaka ya Mapato Tanzania ilinukuliwa kusema kuwa Mgawo wa umeme uliotokea mwanzoni mwa mwaka huu, unaweza kuikosesha mapato Serikali ya zaidi ya shilingi bilioni 840. Tumeona juhudi za Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini katika kutafuta ufumbuzi wa tatizo la umeme, lakini juhudi hizi hazionekani upande wa Serikali na hasa Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, imefikia wakati sasa kutangaza kuwa umeme ni janga la Taifa na kwamba Bunge lipitishe Azimio la uzalishaji wa umeme kwa viwango vya Mpango wa Maendeleo na kuweka adhabu ya kumfukuza kazi Waziri iwapo miradi hiyo haitakuwa imekamilika kila mwaka. Kamati ya Bunge na Nishati na Madini iwe inatoa taarifa mara mbili kwa mwaka (Bunge la Mwezi wa Novemba na Bunge la Mwezi Februari) kuhusu maendeleo ya miradi ya umeme na kama malengo hayajafikiwa, Kamati itoe Azimio la kutokuwa na imani na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inafahamika kuwa nchi yetu imejaaliwa kuwa na gesi asilia nyingi sana. Tafiti zinaonyesha kuwa hivi sasa kuna zaidi ya *12 trillion cubic feet* ya gesi na utafutaji bado unaendelea. Ndani ya miaka michache ijayo nchi yetu itakuwa moja ya Mataifa makubwa yenye gesi asilia hapa duniani. Hata hivyo, hali hii haionekani katika Mipango ya Serikali na viongozi wa kisiasa na hata wataalamu hawaliandai Taifa kwa hali hii. Madhara yake ni kuwa itakapofika siku ya siku tutaingia kwenye migogoro kama tuliyoshuhudia katika Sekta ya Madini. Kambi ya Upinzani inashangazwa na habari kwamba toka gesi ya Mkuranga igunduliwe mwaka 2007, mpaka sasa hakuna mradi wowote umeanzishwa kunyonya gesi hii na kuitumia kuzalisha utajiri kwa Taifa. Tunapendekeza kuwa mradi wa ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara ambalo pia litapita Mkuranga uwe ni kipaumbele cha juu kabisa cha nchi. Mradi huu utekelezwe kwa nguvu kama ilivyokuwa kwa Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria. Bomba hili lijengwe kwa kushirikiana na sekta binafsi na lifike Tanga na Mwanza ndani ya kipindi cha miaka mitano ijayo. Ni lazima tuamue mambo makubwa na tuyafanye. Hili tunaweza kulifanya na tulifanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika suala hili la kuandaa Taifa kwa ajili ya kuwa Taifa lenye kuzalisha gesi na bidhaa zitokanazo na gesi, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa tuanzishe Chuo Kikuu cha Mtwara. Chuo hiki kijikite kuwaandaa Watanzania katika utaalam wa utafutaji, uchimbaji na usimamizi wa Sekta ya Mafuta na gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya njia ya kupunguza matumizi ya umeme majumbani na hivyo kuhakikisha umeme wa kutosha unabakia kwa ajili ya matumizi ya uzalishaji viwandani, Kambi ya Upinzani inapendekeza kwamba miradi miwili muhimu ya gesi kwa ajili ya matumizi ya majumbani ianze ndani ya mwaka huu wa fedha. Nayo ni mradi wa gesi ya *LPG* kwa ajili kujaza gesi kwenye mitungi na mradi wa kusambaza gesi majumbani katika jiji la Dar es salaam. Miradi yote hii itatekelezwa na Shirika la Maendeleo ya Gesi na Mafuta Nchini, *TPDC*. Hata hivyo, Kambi ya Upinzani inakumbushia pendekezo la Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma kuhusu kuifanyia marekebisho *TPDC* kwa kuigawa na kuunda Mamlaka ya Mafuta na Gesi ambayo itahusika na kutoa vibali na leseni na kusimamia utafutaji na uchimbaji mafuta na gesi *(upstream regulator)* na kampuni itakayohusika na biashara ya mafuta na gesi.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa uchumi wa nchi yetu umekuwa ukikua kwa kasi ya kuridhisha katika kipindi cha miaka kumi iliyopita. Hata hivyo, ukuaji huu wa uchumi haujaweza kupunguza umasikini wa Watanzania kwa kiwango cha kuridhisha na cha kujivunia. Mara mbili viongozi wetu wakuu wa nchi (Rais na Waziri Mkuu) wamehojiwa na vyombo vya habari na kukiri kuwa hawajui kwa nini Watanzania ni masikini. Kwa wachumi wengi na kwa kasi hii ya ukuaji wa uchumi jibu ni hilo hilo, kwamba unakuwaje na Uchumi unaokua kwa wastani wa asilimia saba kwa miaka kumi bila kupunguza umasikini? Ni kitendawili na chemsha Bongo. Nina imani kubwa kutokana na tafiti mbalimbali kwamba kwa miaka kumi hatujawekeza vya kutosha katika uchumi wa vijijini na ndio maana hatuoni faida za uchumi wetu kukua. Uwekezaji mkubwa na hasa uliofanywa na sekta binafsi umekuwa ukifanywa katika uchumi wa mijini. Serikali inapaswa kufanya uamuzi wa makusudi kuwekeza katika miundombinu ya uchumi wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani kupitia bajeti hii mbadala, imeleta mapendekezo ambayo inaamini kuwa kwa kiasi kikubwa kwa kipindi cha miaka mitano ijayo itasaidia kujibu kitendawili hiki na itaondoa matatizo makubwa yanayotukabili ya umasikini uliokithiri vijijini na kusababisha vijana wengi kukimbilia mijini.

Mheshimiwa Spika, Katika mkakati wetu wa kufanikisha mpango wa kuondoa umasikini ni kuzifanya Halmashauri zetu za Wilaya kutayarisha kitu kinachoitwa "*District Economic Development Master Plan*", yaani Mpango Mama wa Maendeleo ya Kiuchumi wa Wilaya ambapo kila Halmashauri kupitia Mpango wake kutengeneza ajira zisizopungua 2000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Mpango huu utasaidia kuondoa dhana ambayo imeenea kwa watendaji ngazi za Mikoa na Wilaya kukaa mkao wa kupokea fedha na kutumia tu toka Serikali kuu. Mikoa na Wilaya zitatumia fursa zilizopo katika maeneo yao ili kuondoa

matatizo yanayowakabili wananchi wao kuliko kusubiri kupelekewa wawekezaji toka kituo cha uwekezaji, ambapo Halmashauri zingeweza kuingia ubia na mwekezaji husika.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani katika kufanikisha Mpango huo, tumeleta vipaumbele sita (6) na kila kipaumbele kitasaidia kuinua uchumi wa wananchi waishio vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa baadhi ya vipaumbele ambavyo tumevipanga na Serikali imeleta hivyo hivyo, tofauti iliyopo ni jinsi ya kuvitekeleza ili viweze kuleta tofauti kwa uchumi wa nchi hii. Mheshimiwa Spika, kipaumbele chetu cha muhimu ni kuwezesha ukuaji wa sekta za uzalishaji na hasa ukuaji wa uchumi wa vijijini *(rural growth).* Kambi ya Upinzani inakichukulia kipaumbele hiki kama tiba halisi ya kuwaondolea umasikini Watanzania waishio vijijini kwa kuwa asilimia kubwa ya Watanzania wanaoishi vijijini maisha yao yanaendeshwa na shughuli zinazohusiana na kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika kutimiza azma ya kuinua maisha yao, miundombinu ya barabara na umeme itasababisha ujenzi wa viwanda vidogo vidogo vya kuongeza thamani za bidhaa zizalishwazo vijijini. Ni dhahiri pia asasi za fedha zitakwenda zenyewe na pia itasaidia kupunguza uhamiaji wa kutoka vijijini kwenda mijini *(rural urban migration)* kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kwa njia hii tutafanikiwa kuondoa umasikini uliokithiri na pia kuiondoa nchi yetu kwenye hatari ya kuwa Taifa la Wachuuzi. Pendekezo kubwa katika kuchochea ukuaji wa uchumi wa Vijijini ni la kupeleka vijijini shilingi bilioni 450 kila mwaka kwa miaka mitano mfululizo katika sekta za barabara za vijijini, umeme vijijini na maji vijijini. Fedha hizi zitagawiwa kwa Halmashauri za Wilaya (sio Miji, Manispaa na Majiji) kulingana mahitaji ya sekta husika kwa Wilaya husika ya Vijijini. Tunaweza kufikiria kuanzisha Mamlaka ya Maendeleo Vijijini *(Rural Development Authority)* ambayo itasimamia Mpango huu utakaotekelezwa na Halmashauri za Wilaya chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Tanzania inatumia vizuri fursa ya jiografia yake ya kuwa na ukanda mrefu wa bahari, Kambi ya Upinzani itahakikisha upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam na Tanga kwa kutumia Ushirikiano wa Sekta Binafsi na ya Umma, yaani *Private Public Partnership (PPP*) unakamilika haraka ikiwa ni pamoja na kuimarisha bandari ya Mtwara. Kwa njia hii tutawavutia wafanyabiashara wa nchi ambazo hazina bandari kupitisha mizigo yao katika bandari yetu.

Mheshimiwa Spika, reli ya kati ni kichocheo kikubwa sana cha uchumi kwa wananchi wanaoishi Mikoa iliyopo kando kando ya reli hiyo, pia kuwa kiunganishi kikubwa kati ya bandari na nchi ambazo hazina bandari. Hivyo basi, jambo la kwanza ni kuiboresha reli ya sasa ili ifanye kazi kwa uwezo mkubwa kusafirisha abiria na mizigo mpaka hapo fedha za kujenga reli mpya yenye mataruma ya kisasa itakapopatikana. Ili kutimiza adhima hiyo, tumetenga kiasi cha shilingi bilioni 100 kuliwezesha Shirika la Reli Tanzania kufanya kazi yake ya msingi ya kusafirisha mizigo na abiria. Hata hivyo, uendelezaji wa Mradi wa Mchuchuma na Liganga unataka kuwepo kwa reli itakayounganisha Wilaya ya Ludewa na Bandari ya Mtwara. Kambi ya Upinzani

inapendekeza kuwa upembuzi yakinifu wa reli hii kama ulivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa uanze kufanyika mwaka huu na mchakato wa ujenzi wa reli hii uanze sambasamba na kuanza kwa mradi wa kuchimba chuma na makaa ya mawe.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha usafiri wa anga ambao ni kiunganishi kikubwa kati ya Watanzania na wale wa-ughaibuni na kichocheo kikubwa cha utalii, hivyo basi, Kambi ya Upinzani itahakikisha Shirika letu la Ndege linarudi tena kwenye biashara. Tumeweka shilingi bilioni 200. Kulifufua upya Shirika la Ndege la *ATC*. Hata hivyo, tunashauri kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kurekebisha umiliki wa Shirika la Ndege la Taifa kwa kuhusisha Taasisi za Umma ambazo zinafaidika na kuwepo kwa Shirika mara moja. Kwa mfano, Shirika la Ndege linatarajiwa kukuza utalii wa nchi hivyo Mashirika kama *TANAPA* na *NCAA* yanaweza kuelekezwa kuwekeza mtaji katika Shirika la *ATCL* na kumiliki asilimia zisizozidi 30 za Shirika. Badala ya Mashirika haya kupeleka tozo ya asilimia 10 ya mapato yao Hazina ambayo yanatumika kulipa posho, fedha hizi zinaweza kuwekezwa katika *ATCL* kwa kipindi cha miaka kadhaa na hivyo kulirejesha Shirika katika biashara. Tunashauri wazo hili liangaliwe kiufundi kama linaweza kuleta tija.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni inakubaliana na Serikali katika hatua za kuiimarisha Ofisi ya Msajili wa Hazina ili iweze kusimamia vyema Mashirika ya Umma. Ni wazi kwamba kuna Mashirika ya Umma ambayo iwapo yakisimamiwa vizuri yataweza kufanya kazi kwa faida na hivyo kuondoa mzigo wa ruzuku za Serikali kwenda kwa Mashirika ya Umma. Vilevile Kambi ya Upinzani Bungeni inapongeza pendekezo la Kuanzisha Mfuko wa Uwekezaji wa Taifa kwa ajili ya kutoa Mitaji kwa Mashirika ya Umma. Hatua hii itasaidia sana.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kufanya Marekebisho ya Sheria zifuatazo katika *Finance Bill, 2001* kwa ajili ya kuboresha ufanisi wa Mashirika ya Umma. Sheria ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1992 ifanyiwe marekebisho ili kuiboresha na kutamka wazi kuwa mamlaka ya Ofisi ya Msajili wa Hazina katika kusimamia Mashirika ya Umma ambayo Serikali ina hisa zaidi ya 50% ikiwemo kutoa Mamlaka kwa Msajili wa Hazina kusimamia Waraka anazotoa siku mbalimbali kwa Mashirika na pia kutungwa kanuni zitakazopelekea kuwepo kwa Mfumo wa Maadili ya Utawala Bora *(Code of Corporate Governance for Public Corporations).*

Mheshimiwa Spika, tunashauri sheria iliyounda *Consolidated Holdings* ifanyiwe marekebisho kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2011 ili kulipa uhai wa moja kwa moja Shirika hili na vile vile kupewa Majukumu ya Kusimamia Mashirika ya Umma ambayo Serikali ina hisa chini ya asilimia 50. Lengo la pendekezo hili ni kuhakikisha kuwa hisa za Serikali katika Makampuni binafsi zinasimiwa ipasavyo na kwamba *CHC* iwe kweli ni *Holding Company* ya Serikali kwa hisa hizi. Kwa sasa hisa hizi zinasimamiwa na Msajili wa Hazina. Pendekezo letu ni kutenganisha majukumu haya ili kuleta ufanisi na hasa ukizingatia kuwa *CHC* bado itakuwa inamilikiwa na Msajili wa Hazina kwa kwa asilimia mia moja. Uamuzi huu ukitekelezwa, utarahisisha sana Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma kuwa na jicho la kiusimamizi kwa mitaji ya Serikali kwenye Kampuni binafsi kwani *CHC* hutokea mbele ya Kamati ya *POAC* baada ya kukaguliwa na *CAG*.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina mfumo mzuri wa pensheni kwa wastaafu ambao unasimamiwa na Mifuko kadhaa ya pensheni hapa nchini. Hata hivyo, kuna changamoto kubwa kwamba Serikali inadaiwa fedha nyingi na mifuko hii, hali ambayo tunadhani inahatarisha maisha ya wastaafu. Kwa mfano, Serikali inadaiwa na Shirika la *PSPF* na iliahidi kuanza kulipa deni la shilingi bilioni 700, lakini bado haijalipa. Vile vile Serikali bado haijasaini mkataba wake na Shirika la *NSSF* kuhusu ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Tunashauri Serikali itimize wajibu wake huu ili kuifanya mifuko iendelee kutumikia Taifa na kuwekeza kwenye miradi mikubwa kwa maendeleo ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunashauri pia kuwa Serikali iangalie uwezekano wa kufanya marekebisho katika Mfumo wa Pensheni na kuunganisha mifuko iliyopo na kubakia na mifuko miwili tu, mmoja kwa ajili ya sekta ya umma na mwingine kwa ajili ya sekta binafsi na sekta isiyo rasmi. Hivi sasa nchini kuna jumla ya wanachama takribani 1,073,444 kwenye mifuko ya Pensheni (*NSSF* – 506,218, *PSPF* – 298,046, *PPF* – 160,068, *LAPF* – 73,833 na *GEPF* 35,279) ambayo ni sawa na asilimia 2.4 tu ya Watanzania wote. Hiki ni kiwango kidogo sana kuhudumiwa na mifuko mitano ya hifadhi ya jamii. Vilevile tunapendekeza kiwango cha chini cha pensheni kifikie Sh. 50,000/= na kwa maana hiyo, Shirika la *PSPF* lipandishe pensheni kutoka Sh. 20,000/= za sasa. Tunawapongeza *NSSF* kwa kulipa Sh. 80,000/= na *PPF* kwa kulipa Sh. 50,000/=.

Mheshimiwa Spika, licha ya udhaifu huu wa pesheni kwa wazee wetu waliotumikia utumishi wa umma kuwa kidogo, pia Tanzania haina mfumo wa pensheni kwa wazee bila kujali kama walikuwa waajiriwa kwenye Serikali au Mashirika ya Umma. Wazee wakulima ambao wamechangia kwa kiwango kikubwa katika uchumi kupitia kilimo hawamo kwenye mfumo wa pensheni na hivyo kusababisha kero kubwa kwa wazee wengi ambao ndio wanalea wajukuu huko vijijini kufuatia vijana wao wengi kupoteza maisha kwa magonjwa kama Ukimwi. Kambi ya Upinzani Bungeni, inapendekeza kuanzishwa kwa pensheni kwa wazee wote nchini walio na umri wa zaidi ya miaka 65 na ambao hawamo katika mfumo wa pensheni.

Kuna jumla ya wazee 1,362,435 ambao ni sawa na asilimi 3.2 ya Watanzania wote. Wengi wa Wazee hawa wapo vijijini na ndio walezi wa wajukuu zao kufuatia janga la Ukimwi. Itatakiwa kutenga shilingi bilioni 280 kila mwaka kwa ajili hii. Ni fedha nyingi, lakini muhimu kulinda wazee wetu ambao wamelitumikia Taifa letu ama kwa kulima, kufuga, kuvua au hata kwa kutulea tu. Maelezo ya ziada kuhusiana na mfumo huu wa Pensheni atayatoa Waziri Kivuli wa Kazi na Ajira atakapokuwa anawasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara husika. Maelezo ya ziada kuhusiana na mfumo huu wa pensheni atayatoa Waziri Kivuli wa Kazi na Ajira atakapokuwa anawasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa, napendekeza sura ya bajeti ya nchi iwe kama inavyoonekana katika Jedwali hili hapa chini. Naomba Bunge lako Tukufu lijadili Hoja ya Waziri wa Fedha kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa kuzingatia maoni haya ya Kambi ya Upinzani Bungeni. Sura ya Bajeti

Mbadala kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012, Mapato ya ndani shilingi bilioni 8,681. Mapato ya Halmashauri shilingi bilioni 351, tumebakiza kama jinsi ambavyo Serikali imependekeza. Mikopo na misaada ya nje shilingi 3,924 tumebakiza jinsi ambavyo Serikali imependekeza, lakini tumeondoa mikopo ya kibiashara ili kuweza kupunguza deni la Taifa. Mikopo ya ndani ni shilingi bilioni 1,204; jumla ya Mapato ni shilingi bilioni 14,160; matumizi ya kawaida ni shilingi bilioni 7,913; matumizi ya maendeleo kwa fedha za ndani shilingi bilioni 3,193 na fedha za nje shilingi bilioni 3,054 ambayo ni trilioni sita na ukijumlisha hapo unapata jumla ya matumizi shilingi bilioni 14,160.

Mheshimiwa Spika, mmoja wa viongozi duniani ninaowaheshimu sana ni pamoja na Dr. Mahathir Mohamad - Waziri Mkuu Mkuu wa zamani wa nchi ya Malaysia na rafiki mkubwa wa Mwalimu Nyerere. Ninapenda kumaliza hotuba yangu kwa kunukuu maneno yaliyopo ukurasa wa nyuma wa Kitabu chake, *A Doctor in the House*. Nanukuu: "Viongozi wachache wameweza kubadili uchumi wa nchi zao kutoka uchumi unaotegemea kilimo tu mpaka kuwa na uchumi wa viwanda. Wachache zaidi wameweza kufanya hivi katika kipindi cha miongo miwili tu." Dr. Mahathir aliposhika madaraka ya nchi yake mwaka 1981, Malaysia ilikuwa ni nchi ambayo zaidi ya nusu ya raia wake (asilimia 56) wakiishi katika dimbwi la umasikini. Alipoachia madaraka mwaka 2003 Malaysia ikawa na 3% tu ya raia wake wanaoishi katika dimbwi la umasikini.

Mheshimiwa Spika, Malaysia iliweza kwa sababu viongozi waliweza kuwa na mwono wa mbali, kufanya maamuzi na kuyasimamia maamuzi hayo. Ninaamini kuwa Tanzania inaweza kufanya vizuri zaidi ya Malaysia kama sisi sote viongozi tukiamua kuweka maslahi ya nchi mbele, kuweka malengo makubwa, kufanya maamuzi na kutekeleza maamuzi hayo kwa dhati na kwa makini

Mheshimiwa Spika, kila mtu akitimiza wajibu wake, Tunaweza. Tukiacha kuwa Taifa la walalamikaji, Tunaweza. Tukiendeleza umoja wa Kitaifa, mshikamano na kulinda haki za raia, tunaweza. Ninaamini, Tunaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Kuhusu bajeti mmewasilisha vizuri, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyoeleza jana, kwa sababu hii kazi ya kujadili hotuba ya bajeti ndiyo tutaianza jioni, lakini kwa sababu kuna mila na desturi zake ndiyo maana naahirisha kikao sasa hivi ili kusudi twende kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa tukazungumze baadhi ya hatua zitakazokuwa zinatumika wakati tunaendelea kujadili hotuba nzima ya bajeti pamoja na Wizara zinazohusika. Kwa hiyo, tukirudi mchana atakayechangia wa kwanza ni Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, atafuatiwa na Cynthia Hilda Ngoye, atafuatiwa na Mheshimiwa Rishard M. Ndassa, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. Hawa nimewataja kwa kuanzia, lakini wengine watatajwa zaidi wakati ukifika. Kwa hiyo, mchana nitamwomba Mwenyekiti wa Bunge Mheshimiwa Simbachawene aendelee na mjadala.

## T A A R I F A

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni ya 68(8), asubuhi wakati nilitaka kutoa taarifa, lakini kwa sababu shughuli bado zilikuwa zinaendelea, nimeona nisubiri mpaka wakati huu ili niweze kutoa taarifa. Asubuhi wakati limeuliza swali kwa Wizara ya Ujenzi kuhusu barabara ya Kigoma - Nyakanazi, jambo moja lililosemwa ambalo nimeona ni vizuri tuliseme na tuliweke wazi. Ni kwamba, barabara hii inajengwa kuunganisha Kigoma na Tanzania...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ngoja kwanza, ni kuhusu kanuni hizi hizi. Kanuni hizi kwa taarifa unayotaka kusema wewe na unatumia kifungu cha 28(8) ambapo hicho kinakupa nafasi wewe ya kuweza kueleza na hicho utakachokieleza utakiandika, kwa sababu ukitoa taarifa sasa hivi unamtolea nani? Kwa sababu hakuna mtu aliyefanya jambo lolote isipokuwa kifungu cha 28(8) kinasema hivi: *"Endapo Spika atakuwa amepokea taarifa ya Mbunge yeyote anayetaka kutoa maelezo binafsi, basi Spika hataliahirisha Bunge bali ataongeza muda usiozidi dakika 30 bila kulihoji Bunge ili kutoa nafasi kwa Mbunge huyo aweze kutoa maelezo yake, isipokuwa kwamba maelezo hayo sharti yawe yameandikwa…."*

Sasa maana yake, hii taarifa unayotaka kutuambia, kama kungekuwa na kitu kinaendelea ingekuwa sawa. Nilikataa asubuni wakati wa maswali. Wakati wa maswali swali moja ni dakika tano, sasa ukianza tena na taarifa unakuwa unapunguza muda wa maswali. Kwa hiyo, kama una hoja, hiki kifungu tumia na kama unataka, nipe taarifa jioni baada ya kuahirisha, tutakupa nafasi ueleze hicho unachotaka kueleza.

Kwa sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.00 mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. George B. Simbachawene) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, mchangiaji wetu wa kwanza jioni hii atakuwa Mheshimiwa Freeman Mbowe, simuoni, atafuatiwa na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika jambo hili zito linalohusu mustakabali wa wananchi na Taifa letu. Nianze kwa maneno machache ya kuwapongeza viongozi wetu wote waliopata madaraka ya kutuongoza, watuongoze vizuri ili tuweze kupiga hatua. Pili, niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Gandu kwa kunirudisha tena hapa kuwawakilisha katika chombo hiki muhimu ambacho kinaangalia mwenendo mzima wa mustakabali wao katika maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuangalia bajeti na niseme tu kuwa inasikitisha bajeti yetu mfumo mzima tunaokwenda nao ni bajeti tegemezi na haina mwendelezo yaani ni bajeti ambayo Kiingereza wanasema '*not sustainable*' kwa nini nasema hivyo? Tukiangalia bajeti iliyopita kwa mfano Serikali ilipanga kutumia shilingi trilioni 7.79 wakati makusanyo yalitegemewa kuwa shilingi trilioni 6.18, hapa pana ziada ya shilingi trilioni 1.61 hali kama hiyo inaleta matatizo kwa sababu ukiangalia unapanga kutumia kitu kingi lakini unakusanya kidogo. Hali hiyo inapelekea nakisi, katika bajeti ile iliyopita ilikuwa ni shilingi trilioni 5.4 sawa na 15.7%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuje katika matumizi halisi. Bajeti kwa hali ile ilivyokuwa haikuweza kuwa na makusanyo ya kawaida, yaani lile pato la Taifa halikuweza kuchangia kabisa katika maendeleo na matokeo yake Serikali ikalazimika kutumia mikopo na misaada ili kukidhi matumizi ya kawaida, sasa hiyo ni hali ya kutisha. Hali hiyo kana kwamba haikutosha na safari hii tuna hali hiyohiyo. Ukitazama bajeti, makusanyo yanategemewa kuwa shilingi trilioni 7.13 wakati matumizi yatakwenda mpaka shilingi trilioni 8.6, hii inaonesha kuwa matumizi yatazidi makusanyo kwa karibu shilingi trilioni mbili, mwenendo huu si mzuri kwa sababu unaifanya nchi inakuwa haina uhakika itatumia nini,  kile ambacho kinaletwa kwa ajili ya kusaidia maendeleo hakiendi kwenye maendeleo, matokeo yake kinarudi kwenye matumizi ya kawaida. Kwa mfano, mara hii imesema watakopa ndani, ukikopa ndani, vitu viwili vinatokea, kwanza unaweza ukasababisha mfumuko wa bei, lakini zile pesa ambazo walikuwa watumie wananchi, wazalishaji wa kawaida kukopa, zilishachukuliwa na Serikali, sasa kitu kama hiki kina matatizo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nini tufanye? Nadhani kuna tatizo katika makusanyo na tatizo liko kwa wakusanyaji wetu hasa *TRA*. Mimi binafsi na watu wengi wana imani kubwa na *Commissioner General* wa *TRA*, Bwana Kitilya, amefanya kazi kubwa katika Taifa hili na kila mtu asiyeweza kuona anachokifanya labda kwa sababu hampendi, lakini kwa kweli anafanya kazi nzuri sana. Tatizo liko kwa Watendaji na wakikaza nguvu hapa tutapata pesa hizi ambazo zinaonekana kuwa zinapungua. Mfano, leo ukienda bandarini pale, kontena, mlipishaji kodi anapatana na mteja, hali hiyo haiwezekani, kontena labda liwe na futi 40 anamwambia *okay* hapa utalipa milioni 100, ni *bargaining* mpaka tuseme inafikia milioni 30, akilipa milioni 30 siyo milioni 100 mzozo unaanzia hapohapo, ataambiwa atapewa *location* aliyolipa, hela ile haiendi kunakotakiwa, kwa nini hatuweki utaratibu wa kuaminika? Kwa mfano, unaleta kontena la vyombo vya nyumbani la futi 40 unajua ushuru wako ni *flat rate* hakuna kuzunguka. Unaleta kontena la *spares,* unajua bei yake ni hii, huzunguki sana, Serikali itaweza kukusanya pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unawakuta watu wa *TRA* wako Kariakoo wanapita duka moja moja kukusanya kodi, hivyo kweli wale wanakwenda kukusanya kodi au wanakwenda kutafuta hela za kutia mfukoni? Kwa sababu akifikia hatua ile ya kwenda kwenye duka la mtu, akafunga mlango, ni rahisi sana kuwa–*compromised* mahali pa kulipwa shilingi mlioni moja atapewa laki tatu, atatia mfukoni atamwambia akija mwenzangu usimwambie, mwenendo unakwenda huohuo na *in fact* inarudi kwa yule mlaji, yule muuzaji wa duka ndiye anaumia maana huyu leo kampa laki tatu

anamwambia usimwambie mwenzangu, kesho atakwenda mwingine atamwambia usimwambie mwenzangu, pengine alipaswa alipe laki nane ukishtukia amelipa milioni moja na nusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa utaratibu huu si mzuri, lazima wakusanyaji wa kodi wawe makini na waweke utaratibu ambao hauna usumbufu, kwa nini unafika hadi unapatana na mtu katika masuala ya kazi? Mahali pengi tunajua watu hawa wanakwenda, wanaona, wanasoma kwa wenzetu wanaokusanya kodi mambo yanakwenda wala hufikii hatua ya kuzungumza na mtu, unajua unadaiwa unatakiwa ulipe unalipa. Kuhusu *TRA* nilitaka niseme hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze sasa kuhusu kero ambazo zinatokea kulingana na hali halisi ya bajeti na mwenendo mzima wa nchi yetu. Kuna kitu wanaita misamaha ya kodi, misamaha ya kodi hii iko katika makundi mengi, Wabunge wanayo misamaha, wanapoleta magari yao wanapata misamaha ya kodi, lakini Serikali kipindi kilichopita walisema Walimu, Madaktari na Wanajeshi wanapewa misamaha ya kodi wanapoagiza magari, ni wazo zuri kabisa lakini haionekani kuwa wamepewa kwa nia nzuri. Kwa mfano, hivi ni Mwalimu gani anaweza akanunua gari akatumia yeye? Lazima akinunua gari anakusudia gari ile imsaidie katika kuzalisha mali, ikionekana barabarani gari ya Mwalimu inakamatwa, gari ya daktari inakamatwa, gari ya Mwanajeshi inakamatwa. Wanajeshi katika maumbile yao ni watu hawataki masihara sana, gari zao zikikamatwa wanazifuata *TRA* wanazichukua, lakini wanaoumia sasa ni hawa wengine Walimu na Madaktari. Kama tuna lengo la kuwasaidia basi tuwasaidie waagize magari. Mwalimu anaweka pesa kidogokidogo anachukua mkopo anapata *Pickup* yake anategemea kuwa imsaidie kupata pesa mbili, tatu za kuendesha familia yake. Unaikamata, unaizuia kwamba hakulipa kodi, si wewe uliyeniambia mimi nisilipe kodi, sasa nilipe kodi vipi na mmeniweka kwenye *exemption* ya kodi? Hivi ni vitu vinasikitisha sana, kama tuna lengo kweli la kuuondoa umasikini basi tuuondoe umasikini kwa nia safi, tusifanye *camouflage,* unampa mtu uhuru kwa mkono wa kushoto lakini unauchukua kwa upande wa kulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala la pili ambalo nilitaka nilizungumzie. Tokea wakati wa Baba wa Taifa, moja kati ya kitu kikubwa sana alichokifanya alihakikisha wanyonge ambao katika maisha yao walikuwa wamezoea kuishi katika nyumba mbovu, mbaya kwa namna moja au nyingine wanasaidiwa, wakaingizwa kwenye nyumba zile zilizokuwa zikitumiwa na watu wengine, wakaishi na wengine mpaka sasa wanaendelea kuishi. Sasa inaonekana labda nia hii nzuri ya kuwafanya wananchi wasitirike sasa inabadilika, tena inabadilika katika *gear* kubwa sana kiasi kwamba inaweza ikaleta mzozo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapomwambia mpangaji atoke kwenye kodi ya shilingi 100,000/= kwa mwezi aende shilingi 400,000/= unategemea pesa hizo atoe wapi? Si unamwambia toka aje mtu mwenye uwezo akae? Hivi kweli tumefikia hapo, kweli katika nchi yetu tumefikia hapo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hili nikiwa na uhakika. Sisi tunakaa kwenye nyumba za Serikali pale Mpwapwa *flats* asilimia kubwa ya wanaokaa mle ni watu wa kawaida, Wabunge hawafiki hata sita, Wakubwa wa Serikali hawafiki hata saba, wanaokaa ni watu wa kawaida, unapopandisha kodi ya nyumba tena inapandishwa kabla ya bajeti hii haijasomwa, kuna mpangaji mmoja Mbunge hapa amekwenda pale kutoka kodi ya shilingi 180,000/= anaambiwa lipa shilingi 350,000/= hivi mamlaka yale wale waliofanya wameyapata wapi na Serikali inanyamaza kimya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hali ndiyo hii tunawafanya wananchi waione nchi yao ngumu, waione Serikali yao mbaya na tusidharau vitu hivi, kwa wenzetu watu wanaongezewa bei ya mkate tu mnasikia vurugu, watu wanaingia barabarani wanafanya fujo, hivi hii *lenience* ya Watanzania wanakuwa ni watu watulivu, watu wasiopenda fujo tunaitumia vibaya katika kuwadhalilisha kiasi hiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani, haiwezekani, haiwezekani na sisi wengine mtatufunga haraka sana lakini hatukubali hata siku moja kutoka kodi ya nyumba ya shilingi 180,000/= twende shilingi 350,000/= kwa sababu Meneja wa *National Housing* anataka hivyo, hatutakubali hicho kitu, hatutakubali hata siku moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije katika kitu ambacho pia kinasumbua watu. Tumeambiwa hapa kuwa utaratibu mpya wa kulipia kodi hasa za magari wanafanya *depreciation*, sawa ni wazo zuri kabisa kwa sababu gari ya mwaka mmoja haiwezi kulingana na gari iliyotumia miaka mitano (5) au kumi (10), lakini nani anatafiti gari imenunuliwa wapi? Kwa sababu gari nyingi leo zinanunuliwa katika minada. Hapa Tanzania ni kwenye minada, ukienda Kenya ni kwenye minada, Dubai kwenye minada, Japan zinakozalishwa gari ni kwenye minada, sasa unapofika mahali wewe unakaa ofisini unaivuta gari unasema *Land Cruiser* hii iliundwa mwaka 2001 kwa vile bei yake ilikuwa inapigiwa miaka 10 tuna-*depreciate* namna hii, haiwezekani hivyo, mtu anakwenda kununua gari ya *dollar* 1000 unamwambia alipe ushuru wa *dollar* 7000? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani hata siku moja, huku ni kuwadhalilisha wananchi na kuwafanya labda wasinunue magari. Kama mnataka watu wasinunue magari mtuambie tuendeshe baiskeli basi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baya zaidi mnageuka wale wauzaji wa mafuta ya petroli, wauzaji wa mafuta ya petroli bei ikiongezwa leo anakwambia bwana bei mpya ni hii hapa, lakini ikipunguzwa bei anakwambia aah mimi nilikuwa na *stock* kubwa mpaka imalizike. Sheria ya *depreciation* inakusudiwa ifanywe baada ya bajeti hii, ukienda Zanzibar pale, ukienda Dar es Salaam na mahali pengine bei hizi zinaanza kutekelezwa hivi sasa, sasa ni sheria gani inatungwa inawahusisha watu waliopita? Utaratibu huu uko wapi? Vitu kama hivi ni lazima Serikali iviangalie kwa kina, wakati wa kuwaonea wananchi kwa vitu vidogovidogo na wanaowaonea ni wale watekelezaji kwa sababu kule haendi Waziri wa Fedha kumtoza mtu fedha, haendi Naibu Waziri, haendi Katibu Mkuu, haendi *Commissioner General* wa *TRA*, lakini wale Watendaji wanatumia fursa hii katika kuwadhalilisha watu na mie naamini ile hela kwa kiasi fulani inakwenda katika mifuko yao. Lazima kuwe na *transparency* katika hili, lazima kuwe na ufuatiliaji, nyie mna

uwezo mkubwa wa kujua minada ina bei gani, fuatilieni minada mjue gari hizo zinauzwa vipi? Watu wanyonge wanaokwenda wakinunua msiwafanye wakaona kuwa kumbe ni mateso kununua gari. Wapo Wabunge hapa ananunua gari kwa dola 3000 anaambiwa alipe milioni 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nimemkuta mtu hapo nje analalamika amenunua gari anaambiwa alipe milioni 24 wakati yeye gari kainunua kwa milioni 12, haiwezekani hata siku moja, utaratibu huo si mzuri. Mie sikutaka kusema mengi lakini nasema hizi ni kero ambazo zinaweza zikawa-*provoke* wananchi na huu utulivu wao tunaouona wanao wakasema kesho basi. Mungu atujalie kwa sababu sote tunapenda amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa. Sasa labda niwasome wale watakaochangia kadri watakavyofuatana. Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Hamadi Rashid, Mheshimiwa Kidawa Hamidu, basi tuendelee Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia machache katika bajeti hii ya Serikali kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja napenda kuunga mkono kwa dhati bajeti hii kwa sababu ni bajeti nzuri, inatekelezeka, lakini vilevile imeweka dhamira nzuri kwa Serikali kuwapunguzia wananchi wake makali ya maisha na imeyaangalia maeneo mbalimbali ambayo yanaweza yakafanyiwa kazi. Maeneo hayo ni mengi na sitaweza kuzungumza yote kwa mfano kwa Mtanzania wa kawaida, bajeti hii itamsaidia sana katika kudhibiti upandaji wa kasi wa bei kwa bidhaa mbalimbali na hii ni nzuri sana. Kwa kufanya hivyo, Serikali itatoa unafuu wa bei za mafuta ambayo yamekuwa yana mchango mkubwa sana katika kupandisha bei ya bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kwamba mwananchi wa kawaida lazima ale, Serikali katika mpango huu imeweka uhakika wa upatikanaji wa chakula. Inapotokea chakula kipo ndipo ambapo mwananchi anaishi vizuri. Kwa upande wa ajira, tunaona kwamba nalo Serikali imeliwekea dhamira kubwa hasahasa kwa vijana. Eneo ambalo litatiliwa mkazo ni kuimarisha **vyuo vya SIDO,** vyuo vya VETA, ambavyo vitaandaliwa ili viweze kuwafundisha vijana wetu, wananchi wetu ujasiriamali. Kwa upande wa wanawake wenzangu, kwa hakika mtalifurahia hilo kwa sababu kama wanawake wote watajifunza ujasiriamali kwa hakika wataingia katika vikundi mbalimbali ili waweze kusaidiwa na Serikali kwa njia mbalimbali. Vyuo Vikuu vilevile vimeangaliwa, vijana wa Vyuo Vikuu watapata unafuu kwa sababu ya Serikali kupanua wigo wake wa Mfuko wa Mikopo ya Wanafunzi wa Vyuo Vikuu, kwa hiyo hapo naona Serikali imeendelea kuwajali wanawake, vijana, pamoja na mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikubaliane kabisa na vipaumbele ambavyo vimewekwa na bajeti hii. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete kwa

kuamua na kutimiza ahadi yake ya kuweka suala la umeme na suala la maji kama vipaumbele vya Taifa katika mpango huu wa bajeti wa mwaka 2011/2012, haya aliyadhamiria na tumeshuhudia ameyaweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kwamba Mawaziri wanaohusika au Wizara zinazohusika, zitakuja hapa na mipango mizuri ambayo sisi kama Wabunge tutaridhika nayo na tutaona kwamba ni hatua moja nzuri ya kuweza kuwapunguzia wananchi makali ya maisha na kuwawekea maisha ambayo ni rahisi. Nakubaliana vilevile na vipaumbele vingine ambavyo vimewekwa katika bajeti hii kwa sababu vyote vina umuhimu mkubwa na ninaamini kila mmoja wetu atakubaliana navyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uzito wa kilimo kama mchangiaji mkubwa wa raslimali za nchi hii na mwajiri mkubwa sana katika Taifa letu, kwani asilimia 75% ya wananchi wa Tanzania wanaajiriwa na kilimo, lakini kilimo chetu kimeendelea hivyo kama kilimo cha kawaida. Hatujaweza kuweka *linkage* kati ya kilimo na viwanda ili viende pamoja kwa sababu huwezi ukaendelea kulima tu uka-*consume* basi, lazima uzalishe ili uweze kupata *products* nyingine ambazo pengine utazitumia kwa njia nyingine au utaweza kusafirisha nchi za nje. Kwa mfano, mpango huu wa kilimo katika Nyanda za Juu Kusini na Kusini kwa ujumla *(SAGCOT),* unahamasisha uzalishaji wa mahindi, matunda, mbogamboga na mambo mengine kama hayo. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa Serikali sasa kama tutazalisha kwa wingi kwa *concentration* hiyo inayowekwa huko Kusini, kama tutazalisha kwa wingi matunda na nafaka mbalimbali maana yake unahitaji viwanda ambavyo vitazalisha. Kwa mfano, Mkoa wa Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma, hii ni Mikoa ambayo ni maarufu sana kwa mazao hayo, wanahitaji viwanda vya kusaga unga viwekwe kule siyo Dar es Salaam, tuhamasishe sekta binafsi iwekeze katika Mikoa hiyo viwanda hivyo ili kupata mazao ambayo yatatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile matunda, Mikoa hii ya Nyanda za Juu kwa mfano Mbeya pale ningetazamia Mbeya Mjini kiwekwe Kiwanda cha Kusindika Matunda kwa sababu matunda yanatoka kona mbalimbali za Mkoa wa Mbeya na hata Mkoa wa Iringa kuna matunda mengi. Kwa hiyo, naomba hii *linkage* iweze kuwepo na iimarishwe ili tuweze kupata viwanda ambavyo navyo vilevile vitazalisha ajira na ajira tunaipigia kelele ni kidogo na ajira hii itakuwa ni ya vijana hasa wanawake kwa wanaume. Kwa hiyo, hapo tutakuwa tumekwenda mbali zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa sekta ya utalii ni mkubwa sana katika nchi yetu. Sekta ya utalii katika kipindi cha miaka ya 2008/2009 ilikuwa inachangia katika *GDP* yetu asilimia 17.3 hizi ni takwimu za Bodi ya Utalii. *Exports earnings* kutokana na utalii zilifikia dola bilioni 1.3. Vilevile tuliweza kuingiza watalii wakati huo wa nje peke yake 786,000. Hili ni eneo kwa wakati huo lilikuwa linaongoza katika kipindi hicho, lilikuwa linaongoza katika mchango wake katika *GDP* yetu. Sasa *concentration* bahati mbaya sana imekuwa ni katika ukanda wa Kaskazini, Serengeti, Manyara, maeneo ya mbuga za wanyama za Kaskazini lakini endapo tungeweza kuzishirikisha pia na kuziinua *National Parks* ambazo ziko katika ukanda wa Kusini na Ukanda wa Magharibi katika mbuga za wanyama za Ruaha, Katavi, Mikumi na Kitulo

huko kwenye mbuga ambayo inavutia sana kwa maua ambayo hayapatikani mahali popote, kwa kweli tungekuwa tumekwenda juu zaidi kuliko kiwango hiki ninachokizungumzia. Kwa hiyo, kuna haja ya Serikali kuisaidia TANAPA ambayo wanafanya kazi nzuri sana. Bodi ya Utalii wanafanya kazi nzuri sana basi Serikali tuyape Mashirika hayo msukumo mkubwa ili yaweze kuboresha Ukanda huu wa Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ndani ya *National Parks* hizi ninazozungumzia, kweli kuna mambo ambayo hayapatikani maeneo mengine kama hayo ya Kitulo niliyoyataja. Maua yanayopatikana Kitulo hayapo duniani kote yako Kitulo na Kitulo ni hapahapa Tanzania. Mtu akitoka mbali akaingia Kitulo akaangalia maua si ameleta e*arnings* za kutosha. Ukienda kama Ruaha *National Park* na hasa baada ya kuongezewa na eneo lile jipya la *National Park,* sasa hivi eneo la Ruaha ni kubwa, *National Park* kubwa kuliko *National Park* yoyote hapa Tanzania. Kwa hiyo, naona kwamba ni eneo *potential* ambalo linaweza likachangia pato la Taifa lakini matatizo ni yaleyale hakuna miundombinu ya kuaminika, hakuna barabara, hakuna viwanja vya ndege, hamna *infrastructur*e yoyote ambayo inawavutia watalii kwenda maeneo hayo. Sasa tubadilike, tu-*concentrate* na *North* lakini sasa tuelekeze *concentration* nyingine upande huu wa Kusini, pato letu litaongezeka kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2008/2009 na 2009/2010, mbuga hizo nazozungumzia za Kaskazini ziliingiza watalii wa ndani na nje 2,260,524 lakini mbuga wa wanyama za Ukanda wa Kusini na Magharibi ziliingiza watalii 124,599, tofauti kubwa sana. Sasa maana yake ni kwamba kuna kazi ya kufanya. Naomba Wizara inayohusika ianze kulifanyia kazi suala hili Serikali yenyewe ijikite katika ku-*promote* suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nitoe ushauri kwamba kwa kuwa maeneo haya ya uhakika katika ku-*promote* utalii, Serikali ihakikishe inajenga barabara za lami kuelekea maeneo hayo. Kwa mfano, eneo kama Katavi, Wazungu wanalitamani mno, lakini hakufikiki, tudhamirie kufanya hivyo. La pili, Uwanja wa Ndege wa Songwe, Mbeya jamani ni hadithi ambayo tumechoka nayo, ebu tekelezeni huu mradi uishe, ni kitu gani ambacho kinafanya kila wakati kuwe na ahadi ya kumaliza lakini haumaliziki? Basi afadhali tungesimamisha miradi mingine tumalize huo mradi ambao umedumu kwa miaka zaidi ya 15 tangu uthamini ulivyofanyika mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine ni kuhakikisha kwamba pengine Serikali ingekuwa inatoa *incentives* kwa wale *Tour Operators,* wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Wakipewa *incentives* basi na wenyewe watajitoa kwa wingi kusafirisha watalii kwenda kwenye mbuga za wanyama. Wakati mwingine unakuta pale Mbeya, Iringa watalii wanazubaazubaa tu hawana uwezo wa kwenda kwa sababu wenye magari wanaona ni gharama sana kwenda kwenye mbuga hizo na kwa sababu viwango vya kodi vimekuwa vikubwa, kwa hiyo, inakuwa kama ni tatizo juu ya tatizo. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iliangalie hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, bajeti hii ni nzuri na tutaiunga mkono lakini lazima kuzingatia masuala ya utawala bora ambayo ni lazima na hasa katika uwajibikaji.

Naomba wataalamu wetu waendelee, wafanye kazi kwa bidii, lazima tuwe na nidhamu na kuzingatia sheria, taratibu na hasa taratibu za manunuzi ya mali za umma, tusinunue bidhaa hewa zisizo na ubora lazima kuzingatia *value for money*. Naomba sana na hapa labda niipongeze Serikali kwa kupiga marufuku kuagiza samani kutoka nje, hilo mimi nalipongeza sana. Ile ilikuwa ni hasara na kuleta umaskini katika Serikali yetu bila sababu. Tuna samani nzuri sana hapa nchini, lakini watu walijielekeza sana nje kwa kufuata mng'aro tu wala sio samani. Suala la rushwa vilevile naomba liangaliwe sana kwa watendaji wetu na hasahasa katika utoaji wa tenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nimefurahia sana bajeti hii safari hii kwa sababu nilizozitoa na mengine sikuweza…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango mzuri, anayefuatia sasa ni Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed ajiandae.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nichangie kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Nianze kwa kusema hotuba hii naiunga mkono asilimia 100 kwa 100 kwa sababu imetekeleza yale ambayo Kamati tuliyokubaliana, lakini yale mengi ambayo wadau waliomba Serikali iingize kwenye mpango huu Serikali imetekeleza. Kwa hiyo, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na wataalamu wake kwa usikivu kwa kweli hata wenzetu leo kwenye bajeti yao nimemsikia Msemaji wa Kambi ya Upinzani anayehusiana na mambo ya bajeti ya Wizara ya Fedha Mheshimiwa Zitto hakukataa wala kukubali bajeti ya Serikali kwa maana hiyo ameikubali bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zitto mwisho alisema kila mtu atimize wajibu wake kwa kufanya hivyo tunaweza, tukiacha kuwa Taifa la walalamikaji tunaweza, tukiendeleza umoja wa Kitaifa, mshikamano na kulinda haki za raia tunaweza, akamalizia kwa kusema ninaamini tunaweza. Mimi nasema tukiacha kuandamana tunaweza, tukiacha kuhamasisha migomo tunaweza, tukiacha kutengeneza uongo tunaweza, Viongozi tuoneshe njia sahihi ili tudumishe amani na utulivu. Mimi naipongeza sana kwa kweli kwa sababu tufike mahali kama Watanzania tuwe kitu kimoja kwa maslahi ya nchi yetu. Tanzania hii ni nchi yetu sote na tuliomo humu ndani nina uhakika wote ni Watanzania hakuna Mkenya humu wala Mganda humu wote ni Watanzania, kwa hiyo, tunayoongea humu ni kwa ajili ya maslahi ya Watanzania wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, bajeti hii naiunga mkono kwa asilimia 100, imezungumzia mambo mengi sana nikiyataja hapa nitamaliza muda kwa sababu muda wenyewe ni mfupi labda nizungumzie machache kidogo. Limesemwa deni la nje, Tanzania bahati nzuri siku za nyuma na bahati nzuri jana lilisemwa na Waziri Wasira, huko nyuma tulikuwa hatukopesheki, lakini kwa sababu tulijiwekea utaratibu mzuri wa kulipa madeni mpaka ikatupelekea tukaingizwa kwenye *HIPC* tukawa tunakopesheka. Ndugu zangu ukiwa unalipa unakuwa muungwana na kulipa ni uungwana. Naomba deni hili lisitafsiriwe kama kwamba deni hili eti ni la jana ndiyo maana limefika hapo lilipofikia, deni hili limefikia pahali likaiva kwa sababu sio la leo ni la muda mrefu na ukikopa leo unalipa baada ya miaka 20, 30 mbele. Kwa hiyo, ndugu zangu deni hili tutaendelea kulilipa, nachoomba kwa Serikali, tunapokopa fedha hizi, zielekezwe kwenye shughuli za maendeleo, zisiende kwenye shughuli za utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo naomba uniruhusu nizungumzie njaa katika Mkoa wa Mwanza hususan Wilaya ya Kwimba na Jimbo la Sumve. Hali ya hewa ni mbaya sana. Chakula safari hii hakuna lakini mbaya zaidi na nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakulima wetu wa zao la pamba mwaka huu tunamshukuru Mwenyezi Mungu bei imefika pale. Bei ya pamba kwa mwaka huu tumeambiwa kwamba ni shilingi 1,300/= ilivyopangwa mwanzo lakini kuna wajanja wanne wakakaa pamoja wakasema hapana tunataka tuwanyonye hawa wakulima tuondoe shilingi 200/= ibaki shilingi 1,100/=. Mheshimiwa Waziri Mkuu, mkulima huyu na bahati nzuri na wewe ni mtoto wa mkulima, mkulima huyu mnamnyang'anya ile shilingi 200/= hana chakula, tunataka tumsaidie namna gani huyu mkulima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri suala hili la bei ya pamba, hizi shilingi 200/= anazonyang'anywa huyu mkulima ambaye kila siku analima lakini hanenepi, naomba bei ya pamba ya kuanzia ibaki shilingi 1,300/= na baadaye ikipanda iende mpaka shilingi 1,500/=, 1,600/= na 1,700/= ili mkulima aweze kunufaika. Tukimwondolea hizi shilingi 200/= ambazo wanasema zinakwenda kwenye Mfuko wa Pamba kitu ambacho sio kweli. Ukiangalia mahesabu yao ya mwaka jana mliyoyasoma juzi, Mwanza ni tofauti kabisa, hakuna *contribution* yoyote kwenye zao la pamba mbali na hii *levy* ya huyu mkulima. Mkulima ameweza ku-*contribute* shilingi bilioni nne kwenye huu Mfuko lakini Bodi ya Pamba yenyewe hata senti tano haijaweka. Sasa leo tunataka tuwaongezee ulaji. Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa tutakuwa tunamwonea huyu mkulima wa Mkoa wa Mwanza na tunaambiwa ni zaidi ya Wilaya 47 zinalima zao la pamba, ili tuwanufaishe wakulima wetu wa zao la pamba, naomba bei ya pamba ianzie shilingi 1,300/= na kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nizungumzie maji ya Ziwa Victoria. Hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais kwenye kampeni maji yatoke Ziwa Victoria yaende Ngudu yaanzie Misungwi. Haiwezikani maji yale yako pua na mdomo eti ukanda ule hata Kagera, Magu, Mwanza Mjini, Bariadi, Bunda maji hakuna lakini maji hayo sasa yatoke Ziwa Victoria yaende mpaka Maswa, yaende mpaka Tabora eti sisi wenye Ziwa tusipate maji. Naomba sana suala hili litazamwe kwa ukaribu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu Mwanza *Airport.* Tumesema sana kuhusu hii Mwanza *Airport*. Nashauri kwa mwaka huu kwa sababu tumeambiwa imetengewa fedha hebu tuanze kukipanua, ukiacha Dar es Salaam na KIA, kiwanja kinachofuata kwa ukubwa ni Mwanza.

**TAARIFA**

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge anayesema sasa kuhusiana na Kiwanja cha Ndege cha Mwanza. Kiwanja cha Ndege cha Mwanza kulikuwa na ndege kubwa kutoka Ulaya zikija kubeba minofu ya samaki lakini kwa sasa ndege hizo hazitui na Tanzania inaendelea kupoteza mapato makubwa yaliyokuwa yanatokana na *landing and parking fees* pamoja na kuongoza ndege. Sasa hivi wafanyabiashara wanachukua minofu ya samaki kutoka Mwanza kwenye magari wanaenda ku-*ship* Nairobi, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge sasa hiyo ni taarifa au ulikuwa unachangia?

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Nilikuwa nampa taarifa kuboresha eneo la Kiwanja cha Ndege.

**MWENYEKITI:** Haya bwana, Mheshimiwa Ndassa endelea pamoja na hiyo amesaidia mchango wako.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru amenisaidia, lakini nilikuwa nazungumzia upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza sikuzungumzia ndege, ndege zote nazijua na bahati nzuri tulikuwa kwenye *Road Board* juzi tulizungumzia suala hili la ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Mwanza lakini nakushukuru kwa nyongeza hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Fulo – Sumve – Nyambiti, tumeizungumzia sana barabara hii, inaunganisha Wilaya tatu, Wilaya ya Kwimba, Misungwi na Mwanza kwa ndugu yangu Mawe Matatu. Naomba barabara hii nayo itazamwe. Mwabuki - Magu kupitia Bukimbwa, barabara hii ni ya ahadi ya Mheshimiwa Rais kwamba itatengenezwa kwa kiwango cha lami, naomba Waziri Magufuli alichukue suala hili ili kusudi liweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme. Nilipoongea na Mheshimiwa Ngeleja alisema safari hii sasa nataka kuthibitisha kama kweli ipo kwenye mpango. Umeme kutoka Talo, Ibindo, Kadashi, Nyashana, Maligisu mpaka Kabila *Centre* kwa Mheshimiwa Limbu. Naomba kwenye mpango wa bajeti safari hii Mheshimiwa Ngeleja niione kama ulivyoniahidi ili tuweze kuunga mkono bajeti yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho Mkongo wa Taifa …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Kengele ya ngapi hiyo?

**MWENYEKITI:** Ya kwanza, endelea.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, Mkongo wa Taifa kwa sababu ya sayansi na teknolojia, bahati nzuri pale Malya kuna Chuo cha Michezo kikubwa tu cha *Eastern Central*. Tunaiomba Serikali iweke Mkongo wa Taifa kutoka Ngudu, Sumve mpaka Malya. Kwa kufanya hivyo, vijana wetu na Chuo chetu kile watakuwa wanapata mafunzo mazuri sana ya kujifunza teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, namwomba sana Waziri Mkuu, tusicheze na pamba kwa Mkoa wa Mwanza, pamba ni siasa, pamba ni uchumi, lakini bahati mbaya safari hii Mkoa wa Mwanza pamoja na Mkoa wa Shinyanga njaa ni kali sana. Nimesema hawa watu wanne, Waziri Mkuu nakujua siku zote huwa unapenda kuingilia kati kama unaona mambo yanaenda vibaya, kama ulivyofanya safari ile, nakuomba na hili wala usilionee haya. Nenda ukalifuatilie vizuri, lakini kwa sababu msimu unaanza tarehe 20 ukifanya haraka itakuwa nzuri zaidi. Naomba mahesabu yao kuanzia mwaka ujao wa fedha yakaguliwe na *Controller and Auditor General* ili tuone ukweli uko wapi kwa sababu haiwezekani fedha za wananchi zinatumika bila kufanyiwa mahesabu ambayo yanajulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango mzuri. Anayefuatia sasa ni Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed atafuatiwa na Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh na baadaye Mheshimiwa Azzan Zungu.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, tumepewa semina leo tusipongeze.

Kwanza, naomba tu katika mpango tulioupitisha jana tulisahau kwamba Elimu ya Juu ni mambo ya Muungano na kwa bahati mbaya katika Mpango, Vyuo Vikuu vya Zanzibar vyote havimo. Naomba kwa sababu unatengenezwa sasa upangwe vizuri, hiyo kasoro ambayo imejitokeza jana irekebishwe na nilimwambia Katibu wa Mipango na Waziri, lakini nalisema hili ili liingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nikubaliane na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba tunahitaji kuweka *reserve* ya *gold*, lilifanyika hili nakumbuka mwaka 1987/1988, Benki Kuu ilikuwa ikinunua dhahabu, kwa bahati mbaya haikuwa na utaratibu mzuri ikanunua dhahabu ambayo haikuwa nzuri, utaratibu ule ukasimamishwa. Hata wakati tunanunua ndege ile ‘F Foka 50’ ilitumika *reserve gold* iliyokuwepo

kununulia ndege ile. Kwa hiyo, uwezekano wa kuweka dhahabu ni bora zaidi kuliko *currency* kwa sababu ya *fluctuations* ambayo inatokea. Dhahabu bado inaendelea kupanda bei na haitegemewi kuteremka. Tulianza na *two hundred dollars ounce*, sasa tupo *one thousands five hundreds dollars ounce*, kwa hiyo kuweka *reserve* ya *gold* ni *better*. Naomba *Central Bank* walifanyie kazi na tuweze kuweka *reserve* ya *Gold*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, naomba sana Waziri Mkuu asimamie *bureaucracy*. *Bureaucracy* inaturudisha nyuma sana na hatuwezi kufika pahala. Hivi sasa ukiandika barua huwezi kupata majibu, ukienda kuonana nao wakubwa watakupa maneno, ukiondoka pale maneno yanakuwa mengine, kwa hiyo utaratibu mzima hauendi. Sasa tunaingia *PPP*, natoa mfano hivi sasa kuna mwekezaji kutoka Japan yuko tayari kujenga *megawatt* 400 za umeme na kutengeneza bomba la gesi kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam. Unapeleka taarifa, unapeleka *e-mails* hakuna hata mmoja anakuambia kama nimepata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Sheria ya *PPP* imetoka, tengenezeni Sheria na Kanuni, weka miradi yote katika hiyo Sheria na Kanuni ambayo inatakiwa iende kwenye *PPP* ili anayetaka kuja ajue kabisa Sheria inasema hivi, miradi ni hii hapa, tuondoe huu urasimu, bila hivyo itabaki hadithi. Weka Sheria, weka Kanuni, *identify projects* ambazo zinatakiwa ziende *under PPP,* ziwe *clear* ili mtu akisoma tu kwenye *website* anajua kwamba Tanzania *under PPP* kuna mradi fulani unatakiwa, Sheria inasema hivi, Kanuni inasema vinginevyo, tutakuwa tunapiga hadithi hapa ndani ya nyumba, Sheria imepita miaka miwili iliyopita, Kanuni imekaa miezi sita na miradi haijakuwa *identified* mpaka leo, hatufiki pahali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne, ni *TIB*, tumeambiwa kwamba kuna Dirisha la Kilimo *TIB*, tumefurahi sana na Benki ya Kilimo ambayo ni hadithi ya siku nyingi, tumeambiwa mwaka huu katika Mpango itakuja, *fine*, lakini yapo malalamiko kwamba kwenye Dirisha la Kilimo la *TIB* siyo rahisi kupata huo mkopo. Wakulima wengi hasa wakulima wa kati wameenda, wamesumbuka sana bila ya kupata mkopo. Naomba Serikali ifanye utafiti, iunde Tume, ikutane na wadau hasa wale wanaokwenda kuomba mkopo, kweli huo urahisi tunaozungumza upo kweli au tunauzungumza nadharia? Vinginevyo utaratibu tunaouona sasa hivi wa *TIB,* Dirisha la Kilimo hautofautiani kabisa na utaratibu wa *Commercial Bank.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tano ni riba, bado riba ni kubwa. Riba inayotozwa kwa mikopo na riba inayotozwa kwa kuweka fedha inatofauti kubwa sana, haiwawezeshi wananchi kutumia Taasisi za Benki na ndiyo maana mpaka leo kuna asilimia 14 tu ya Watanzania ndiyo wanatumia vyombo vya fedha kwa sababu huwezi kwenda kuweka fedha yako ukapata *interest* ndogo wakati *interest* ya kulipa ni kubwa sana. Hili ningeomba lisahihishwe haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri alizungumzia sana suala la Tume ya Pamoja ya Fedha, leo tutakosana na rafiki yangu, tutakosana kwa sababu Tume ilipokutana na Kamati ilileta taarifa yake mwaka 2006 kwa Serikali zote mbili, taarifa hiyo mpaka leo haijafanyiwa kazi na Tume ikalalamika. Inasema tatizo la kwanza ni utaratibu wa

mawasiliano baina ya Tume na Serikali mbili kwamba hayako *clear*. Kwa maana hiyo, wanapeleka mapendekezo, wao kazi yao ni kusubiri tu, lakini hili ni jambo la Kikatiba. Kwa hiyo, tumeendelea kuvunja Katiba ya mwaka 1977, tumeendelea baada ya kuunda Tume na mpaka leo tunaendelea kuvunja Katiba bado Akaunti ya Pamoja haipo. Nakuomba Waziri uje hapa katika Bunge hili utueleze mgawanyo wa mapato na matumizi ya Muungano na akaunti ya Muungano itafunguliwa lini, ni lazima utueleze. Nawaomba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wambane Waziri wa Fedha huko Zanzibar hivyo hivyo, awaeleze ni lini Akaunti hii ya Pamoja itafunguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu gani? Ndugu zetu wa Bara wanalalamika kwamba Zanzibar inabebwa na Wazanzibar wanalalamika kwamba Watanzania Bara wanawaumiza. Sasa njia peke yake ya kujua ukweli huu ni Tume hii kuja wazi, kusema mambo ya Muungano ni haya, gharama zake ni hizi, mapato yake ni haya, tuchangie Mfuko huu ili tuondokane na tatizo hili, kwa nini tunafuga maradhi? Miaka yote hii tunafuga maradhi kwa nini, tumeunda Tume ili kuondoa tatizo hili? Namwomba Waziri aje hapa na maelezo ya kutosha, haya maelezo uliyoweka humu yamo katika vitabu vyako, nimechukua vitabu vya hotuba zote za Waziri, maneno ni yaleyale miaka yote hayajabadilika, mara hii tunataka *statement* ya vitendo katika bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *revenue*, leo asubuhi Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi alielezea juu ya fedha zinazopatikana kutokana na meli zinazovua nje au kwenye Ukanda wetu wa Uchumi *(Economic Zone).* Ukitazama Kitabu cha *Revenue* kwa miaka miwili au mitatu huko nyuma hakuna mapato, mara hii mapato ya leseni ziko kama milioni mia nane hamsini na nane mia sita na themanini na moja, Waziri hapa asubuhi anasema tumekusanya dola milioni mbili, kitabu cha *revenue* hakina hata senti tano za mwaka jana wala mwaka juzi, nikashtuka sana. Ndiyo pale nikanyanyuka asubuhi kumwomba Spika bahati mbaya hakunipa nafasi. Hii taarifa aliyoitoa Waziri haiko Wizara ya Fedha au Mapato ya Serikali yanakusanywa hayaendi Mfuko Mkuu wa Hazina? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana ukisoma taarifa ya ukusanyaji wa mapato bado tunakusanya asilimia arobaini tu ya mapato halisi, kwa sababu fedha haziendi kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina. Ushahidi upo, ukisoma *Hansard* ya asubuhi. Halafu wanasema meli zilizoko nje ni 75, ukichukua kwa *rate* ya dola 35,000 na kitabu hiki kinaonesha hakina hata senti tano, hizi pesa ni nyingi sana. Kwa hiyo, bado hatujashughulikia ukusanyaji wa mapato lakini hata kile tunachokikusanya nacho hakirudi, ndiyo maana juzi tumepewa chenji yetu ile ya dola milioni ishirini na sita kutoka Uingereza wala hatuelezwi ziko wapi, zile za *Radar*, Serikali ipo kimya tu, kwa hiyo pesa ina *hang* tu! Sisi tunaendelea tu kusema ahsante, hata kile chetu kukifuatilia hatuwezi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri anieleze hivi ni kwa nini kwenye *Revenue Book* haioneshi haya mapato ya meli hizi zinazovua nje na Waziri asubuhi alisema kuna meli zingine za Watanzania, hakuna meli ya Mtanzania inavua nje. Meli za Watanzania zinazovua nje ni *Troller Fishing Boat*, zinazovua samaki ya aina ya Kamba. Ndizo zinazotoa leseni dola kumi na nane elfu, mimi nilikuwa nikivua miaka kumi

iliyopita kwa kutumia hizo meli na *rate* haijabadilika mpaka leo. Meli zinazovua *deep sea* za Watanzania hamna, kwa sababu sera yetu ya kuwawezesha Watanzania iko kwenye maneno na vitabu, hakuna Mtanzania anayewezeshwa hapa, hapa Mtanzania akiomba leseni ya jambo fulani anapigwa vita *from left to right* na bahati mbaya na sisi wenyewe kwa wenyewe tunaitana mafisadi tunazidi ku-*dilute* hata wale waliojitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuwe *serious* katika kuwasaidia watu, wavuvi ni watu milioni saba, ukanda wa bahari una tani laki saba za samaki, wala siyo suala la joto wala la nini. Ukienda Pemba kwenye eneo langu mimi la Wawi ndiyo kwenye *deep sea* kule, ukienda kwa Mheshimiwa Masoud, mpaka Mkanyageni kwa Mheshimiwa Mnyaa ndiyo kabisa samaki wako tele, wengi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya *FAO* inasema Tanzania tuna samaki ambao wameishi zaidi ya miaka mia moja hawavuliwi. Ndiyo maana kuna vyombo zaidi ya mia moja vinakuja kuvua, sasa hivi vyombo vinavyokuja kuvua havipambani na *piracy,* tunaopambana na *piracy* ni sisi tu? Vyombo vinavyoiba havipambani na *piracy*? Vinapambana, lakini hakuna sera madhubuti ya kuwawezesha Watanzania. *I hope* huu Mpango tulioupitisha labda utali-*address* baadaye hilo. Nasema labda kwa sababu bado sijaona uwezo wa Tume ulioundwa mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo na mapato ya mifugo. Ng'ombe waliopo Tanzania ni wengi sana. Unahitaji kuvuna maana kuna vitu vingine vya kupanda utie mbolea, vingine ni vya kuvuna, samaki ni wa kuvuna, mifugo ni ya kuvuna. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ukizungumzia *Quick Wins* kwenye uchumi, basi *items* hizi mbili zinakupa *impact* ya haraka sana, inategemea unavyokusanya mapato. Leo Oman wanataka nyama, Emirates yote inataka nyama, kuna mfanyabiashara hapa anasafirisha nyama yaani watu wanaotaka nyama ni wengi. Ni watu kufikiri tu ni njia gani za haraka za kuwawezesha hawa Watanzania wakasafirisha nyama, hatufanyi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba sana suala la msamaha ya kodi. Nina orodha hapa ndefu kidogo, asasi ambazo zina misamaha ya kodi na kadhalika. Waziri hapa katika kusamehe kodi na kufuta misamaha ametoa bilioni ishirini na mbili kati ya bilioni mia nane na sitini na tisa. *We are joking! Let us be serious* katika *issue* hii, halafu katika hotuba ya Waziri anasema kuna kampuni zinazochimba gesi anataka nazo azifutie tena msamaha, sasa huku unatoa huku unaingiza, hatufahamu sasa! Tunajipangaje? *Let us be serious*. Maana yake wale kule wanafanya maandamano usiku lakini siku hizi wakitaka kufanya mchana wanafanya *holiday* maana ni mambo ya Kikatiba haya. Nasema ni muhimu sana Serikali ikajua kwamba bila ya kuwa na utaratibu mzuri wa kupunguza hizi kodi *seriously* na mkae na makampuni haya *seriously* watuambie, kwa mfano, maduka yasiyotozwa ushuru ni kama bilioni ishirini, lakini Kituo cha Uwekezaji peke yake ni bilioni mia moja na sabini na saba. Tunahitaji kukaa na Kituo cha Uwekezaji, hawa watu hawajamaliza miaka mitano? Maana *after five years* ile *tax holiday* inaondoka au wanabadilishana tu mikataba, kwa hiyo tunahitaji kukaa nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa ni suala la masoko, tumezungumza jana suala la masoko na ninaomba nilipanue kidogo. *Tanzanite* hivi sasa soko lake kubwa lipo South Africa, Chai ya Tanzania soko lake liko Dubai, Kahawa tu ndiyo ipo hapo Kilimanjaro. Tunahitaji kuanzisha masoko yetu ili watu waje wanunue bidhaa hapa. Nimeshuhudia Maldives**,** samaki mnunuzi anakwenda mwenyewe kununua pale na anakuwa *registered* kwamba wewe ni mnunuzi wa samaki na wewe ni *registered* kwamba wewe ni muuzaji wa samaki. Kwa hiyo, tunahitaji hizi bidhaa zetu kuzipanulia soko, ukiwa na soko utauza vizuri. Sisi karafuu tunazalisha vizuri kama tumepata kupenya kuuza magendo kule Kenya, maana ukikamatwa na KMKM unapigwa risasi. Watu wanashughulikia mikarafuu wanailimia vizuri, lakini tatizo ni soko. Tupanueni masoko ili watu waweze kufanya biashara na soko kubwa, bidhaa zetu tuuze ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulizungumzia hapa vito tutavitengeneza hapa Tanzania ili watu waje wanunue, hiyo kazi imefikia wapi, mwaka wa tano tunazungumzia hadithi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyopo Mezani sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa leo kuchangia hoja hii, lakini pia nawashukuru na kuwapongeza wanawake wa Mkoa wa Kaskazini kwa kuniwezesha kusimama katika ukumbi huu kwa kunirudisha tena Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Makamu wa Rais wake, Dkt. Mohammed Gharib Bilal, kwa kuchaguliwa kwa ushindi mnono sana kuwa Viongozi Wakuu wa nchi yetu. Aidha, napongeza sana ushindi ulioupata Chama cha Mapinduzi kwa kuvuna Majimbo 187 kati ya majimbo 239, ushindi wa asilimia 78+, ni ushindi wa kujivunia, nakipongeza sana Chama changu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Waziri kwa bajeti nzuri aliyoiandaa na kuileta hapa, ni bajeti iliyowagusa Watanzania wote, ni bajeti ambayo imekusudia kuleta maisha bora kwa Watanzania. Kwa kuthibitisha hayo, ninayoyasema, kuna vielelezo ambavyo vimezungumziwa katika bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema bajeti imewagusa wananchi wote tukianza na wafanyakazi, mbali ya kuwa tumeelezwa hapa kuwa kima cha chini cha mshahara kitaongezwa lakini vilevile posho ya wafanyakazi hawa vilevile imesamehewa kodi. Hii ina maana kuwa kile kiwango cha fedha cha kuchukua nyumbani au *net take home* cha mfanyakazi kitaongezeka na vilevile kwa kufanya hivyo uwezo wake wa kutumia au *purchasing power* yake itakuwa imeongezeka pia. Tunajua kuwa familia zetu ni *extended*

*families* kwa hiyo manufaa hayaendi tu kwa mfanyakazi mmoja mmoja lakini itakwenda pia na wale wote wanaomtegemea. Nakupongeza sana Mheshimiwa Mkulo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hayo tu lakini vilevile wameguswa hapa wakulima. Kuna msamaha wa *VAT* katika zana za kilimo, wameguswa hata wafuga kuku, kuna msamaha wa kodi katika chakula cha kuku, tunajua akina mama wengi na vikundi vyao wanafuga kuku, tunasema akina mama kaeni mkao wa kula, neema inakuja, fugeni kuku kwa wingi, chakula cha kuku kitapungua bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile bajeti hii imemgusa mvuvi, tumeelezwa hapa zile nyuzi za *nylon* za kutengezea nyavu zimeondolewa kodi kwa hiyo wavuvi pia watanufaika. Mbali ya hayo, Watanzania wote watanufaika kwa punguzo la bei ya mafuta ya petrol. Tunajua bei za mafuta ziko juu sana na zikiwa juu maisha ya watu wote yanakuwa ghali kwa sababu usafirishaji wa mazao unakuwa ghali, usafirishaji wa abiria unakuwa ghali kila kitu kinapanda bei lakini kwa vile Serikali yetu ni sikivu, Waziri amesikia kilio cha wananchi, amesikia kilio cha Wabunge, kwamba maisha ni ghali kwa hiyo amekubali kupunguza tozo mbalimbali zilizokuwemo katika bei ya mafuta. Aidha, Mwenyekiti wa Kamati hapa aliposoma taarifa yake, alizungumzia kuwa pia afikirie kupunguza *Excise Duty* na *Import Duty* ili bei izidi kuteremka chini, kwa kufanya hivyo Watanzania wote watanufaika na watakuwa *betteroff* katika maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nije katika kuangalia sura ya bajeti yenyewe. Bajeti yetu tunaweza tukaigawa katika mafungu matatu, yaani mikopo na misaada ya nje, mikopo ya ndani na mikopo ya kibiashara. Hii imechukua karibu asilimia 47.4 ya bajeti yote. Lakini kuna mapato ya ndani ambayo yanaunganisha mapato ya kodi na yasiyo ya kodi, ambayo ni karibu asilimia 50 ya mapato yote. Lakini vile vile kuna mapato ya Halmashauri ambayo ni asilimia 2.6 ya mapato yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia picha hii na tukiangalia matumizi yalivyo tunaona kwamba mapato yetu ya ndani yale ya kodi, yasiyokuwa ya kodi na ya Halmashauri ukijumlisha pamoja unapata karibu trilioni 7.2. Lakini tukija kwenye matumizi ya kawaida ni karibu trilioni 8.6. Hapa kuna karibu pengo la trilioni 1.4. Hii siyo picha nzuri sana na inahitajika kufanyika mikakati ya nguvu na taratibu zote ili kuboresha hivi vyanzo vyetu vya mapato; vyanzo vyetu visivyo vya kodi na vyanzo vyote vingine vya mapato. Tunatakiwa tupanue wigo wa kupata mapato zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye taarifa ya Kamati ya Fedha, iliainishwa kwamba, kuna maeneo mengi tu ambayo bado yanatakiwa kufanyiwa kazi. Eneo moja ni eneo la utalii. Kuna nchi zinajiendesha kwa utalii tu na utalii ndani ya nchi yetu unakua. Lakini sidhani kama kweli tunapata mapato yanayotokana na kianzio hiki ya kutosheleza. Ipo haja ya kufanya *study* kuangalia *potential* ya maeneo hayo ya mapato tunaweza tukapata mapato kwa kiasi gani zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi kama Misri ilipokuwa imetulia wakati huo walikuwa wanapata mapato mengi zaidi kutokana na mambo ya utalii. Watalii wanakwenda kwenye *museum*, kuangalia Mafarao na Wafalme wa Kale, saa zote kuna

*queue* na watu wanapata mapato. Kwa hiyo na sisi tuangalie katika eneo hili la utalii, tuone namna gani tunaweza tukapata *maximum revenue* kutoka sekta hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sekta ya madini, sidhani kama tunapata mapato ya kutosha kutokana na madini yetu. Ipo haja ya kufanya utafiti ili tuone tutanufaika kiasi gani na madini yetu mbali ya kuwa tunapata *royalty,* lakini vile vile tuangalie hawa watu wanachimba madini wanatuachia mahandaki hebu tuwa-*tax heavily* na sisi tunufaike na tuweze vile vile kupata fedha za kuboresha yale mazingira yaliyoharibiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumzia suala la kodi, kila kipindi cha bajeti kikifika tukiangalia vyanzo vipi vya kupata kodi zaidi kunaongezwa kodi katika vileo na sigara. Vyanzo hivi iko siku vitakuja kutuangusha kwa sababu sasa hivi kuna *program* mbalimbali za kuhamasisha watu kutokulewa au kupunguza ulevi tunaambiwa ulevi noma kwenye *Television* na kwenye redio yanatolewa matangazo. Wavutaji wa sigara wanahamasishwa wasivute sigara, sigara zina madhara, sigara zinaua, sigara zinaleta *cancer,* iko siku watahamasika na kuacha kuvua. Wale ambao wazee wanaokunywa na kuvuta sigara watamalizika. Vijana tunawahamasisha wasijiingizea katika uvutaji wa sigara. Hivyo, tuangalie namna gani tunaweza tukapata mapato katika maeneo mengine ili chanzo hiki kisije kikatuangusha. Tunasema walevi kama ni *chronic* wataendelea kulewa kwa sababu hakuna *substitution* ya ulevi mkali. Wakitumia *substitution* ya ulevi mkali ni gongo, gongo ni kosa la jinai, watakamatwa na kufungwa, tumeona wengine wamepofuka macho tumeona kule Kenya na wengine chungu nzima wamekufa kwa sababu ya kunywa vinywaji vikali. Ndiyo maana nasema tuangalie maeneo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile kuna *deficit* katika sura yetu ya bajeti tunatumia mikopo kwa ku-*finance recurrent expenditure* na kuna mfano mmoja ambao umetolewa kwenye mikopo ya ndani tumeandikiwa hapa, imekuwa kama unamkopa Juma kwa kumlipa Jane. Ukurasa wa 48 imeainishwa katika mwaka 2011/2012, Serikali inakusudia kukopa kiasi cha shilingi 1,204.3 bilioni katika soko la fedha la ndani. Kati ya kiasi hiki shilingi hiyo hapo imeainishwa pale kwa kuziba nakisi ya mapato ya Serikali lakini na shilingi bilioni 310.9 ni kwa ajili ya kulipa dhamana zinazoiva. Hapa tunataka kuondoa ile aibu ya kukopa na kushindwa kulipa. Dhamana imeiva tunatakiwa kulipa lakini je tutazipata wapi fedha. Mfano, nilioutoa nimekopa kwa Juma siku alizoniambia nilipe zimefika, nitafanya nini kuficha aibu yangu, namwendea Jane, hebu Jane nikopeshe hizo hela nina shida nazo, kumbe nakwenda kumlipa Juma. Kwa maana hiyo, lile deni linakuwa limebakia pale pale. Hii vile vile inathibitisha na inahakikisha ule umuhimu wa kutafuta vyanzo vipya vya mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia kuhusu vipaumbele. Vipaumbele vilivyoainishwa kwenye bajeti hii ni sahihi, ni muhimu kwa sababu vipaumbele hivi vikitekelezwa ndio msingi wa maendeleo ya nchi yetu. Katika mwelekeo wa Sera za Chama cha Mapinduzi katika miaka ya 2010 hadi 2020 imeainishwa kuwa tutumie fursa za Kijiografia tuliyonayo katika nchi yetu ili tuweze kupata maendeleo. Nchi yetu ni nzuri sana tumejaliwa kila kitu, tuna mabonde, ardhi nzuri, maji na bandari nzuri, tuvitumie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele hivi vilivyotajwa katika bajeti yetu, kipaumbele cha kwanza ni miundombinu. Miundombinu ni sekta muhimu sana katika kuleta maendeleo ya nchi, ndio maana miundombinu imepewa kipaumbele namba moja. Sekta hii imepangiwa karibu asilimia 20.5 ya bajeti yote, kwa maana ya reli, barabara na bandari. Tunataka kufungua nchi yetu, nchi ambazo ni *landlocked* wapitishe mizigo yao kupitia bandari yetu, tujenge reli nzuri, tujenge barabara nzuri ili wasafirishie mizigo, nchi yetu inemeeke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo ya nje na ya ndani inatakiwa kutumika katika sekta kama hizi, sekta ambazo ni *productive*, sekta ambazo zina-*facilitate* ukuaji wa uchumi kwa sababu *in the long run* wanaokuja kuathirika na mikopo hii ni *new generation* ambayo ni kizazi chetu na wajukuu zetu. Kwa hiyo, tukiwekeza katika sekta ambazo ni za uzalishaji, mapato yatakuwa *generated* kutokana na sekta hizi. Kwa hiyo, watu hawata-*suffer* sana kwa sababu kutakuwa na *revenue* ya kutosha kuweza kulipia ile mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele kingine kilichowekwa ni kilimo. Asilimia 73 ya Watanzania wanaishi vijijini wanategemea kilimo kwa maisha yao. Kwa hiyo, ni sawasawa kipaumbele hiki kuwekwa. Lakini ukiangalia asilimia ya bajeti iliyowekwa *to the total budget,* bajeti ya mwaka huu imeshuka kuliko ile ya mwaka jana. Hapa tuna *6.9% while* mwaka jana tulikuwa na asilimia 7.7. Kwa hiyo, lile lengo la *Maputo Declaration la 10% of total budget* kwenda kwenye kilimo bado kuna kazi kubwa ili kuweza kufikiwa. Lakini hata hivyo, ninachokipongeza ni kwamba, kiwango cha fedha zenyewe kimeongezwa kutoka bilioni 903.8 mpaka 926.2 ambazo ni sawa na asilimia 6.8 ya bajeti yote. Kiwango kimeongezwa lakini asilimia imeshuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni uhai, ni lazima tushughulikie suala la maji, ndio maana maji yamepewa kipaumbele. Tafiti zinazofanywa na wataalam kwa kuwauliza watu mmoja mmoja kipaumbele chenu hapa ni nini vijijini na kwingineko, wanasema ni maji. Akinamama wanachoka kujitwika ndoo kichwani alfajiri, usiku wanakwenda kuhangaikia maji mpaka akina mama wanatoka vipara, ni aibu. Tumezoea kuona vipara kwa akinababa tu. Lakini sasa akinamama wanatoka vipara kwa kujitwisha ndoo za maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza bajeti, vipaumbele ni vizuri, lakini kuna tatizo la mtambuka. Tuna tatizo la madawa ya kulevya, watoto wetu, vijana wetu wanaathirika sana. Juzi nimeona kwenye *Television* yule Kiongozi wa *Task force* alikuwa anazungumza, anasema katika mwaka mmoja uliopita 2010 katika mipaka yetu na humu ndani zimekamatwa karibu kilo 190 za madawa ya kulevya. Vijana wetu wanaumia. Kwa hiyo, Serikali iendelee na mikakati yake na iandae mikakati mipya ili tatizo hili tupambane nalo na liondoke katika nchi yetu, linatuharibia watoto wetu, linatuharibia nguvu kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na naipongeza bajeti. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kidawa kwa mchango wako mzuri. Sasa namwita Mheshimiwa Zungu, Mheshimiwa Mgimwa ajiandae.

**MHE. MUSSA AZZAN ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu. Baada ya kumshukuru yeye nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Lakini nimpongeze Waziri wa Fedha, kwa bajeti safi na bajeti inayojali watu na hasa watu wa kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nachukua nafasi kumpongeza Mheshimiwa Stephen Wasira kwa namna alivyoainisha mpango wa miaka mitano ijayo. Napongeza sana yeye na Tume yake. Naunga mkono hoja mapema kwa sababu mazuri yanaanza mapema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo tatizo la kodi, takwimu za *APRM* zinaonyesha katika Watanzania milioni 40 ni Watanzania milioni 1,600,000 tu wanaolipa kodi. Lazima tupanue wigo wa kodi na hasa kwa watu wa kawaida. Tukiweza kuainisha milioni 20 na kila mmoja akalipa milioni 50 kwa mwaka Serikali hii itajiongezea mapato ya trilioni moja. Kwa hiyo, tufanye mpango maalum wa kuhakikisha wananchi wahamasishwe na kulipa kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la *added value* kwenye mchanga wa madini unaotoka nchini mwetu kwenda kufanyiwa kazi nchi za nje. Mikataba iliyokuwepo ya madini inazungumzia tu dhahabu. Lakini mchanga huu unabeba almasi, unabeba *platinum*, unabeba *copper*, unabeba vitu vingi sana ambavyo haviwi *recorded* na kurudishwa kugawanywa kati ya mwekezaji na Serikali. Ningeomba wanaohusika wajaribu kulitazama vizuri suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana suala la Serikali kuwa na s*torage measures, measures* za kupunguza na kubana matumizi, *that is the way forward*. Kuna nchi kama nne Ulaya sasa hivi zimeanzisha *measures* hizi na hizi si *measures* za posho tu, haziendani na posho peke yake. Lakini nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kutokukubali kutumia magari yenye gharama kubwa bila sababu yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nategemea kwa uzalendo na upenzi wa nchi hii labda angeigwa mfano na watendaji wake kwenye Wizara na kwenye Mashirika ya Umma. Sasa nafikiri Serikali ianze mpango sasa siyo wa kuzuia tu kununua mashangingi bali ianze mpango wa kudhibiti matumizi mabaya ya gari za Serikali kwa gharama kubwa sana. Naweza hata kusema kwamba, Mawaziri wote ambao ni Wabunge wamekopeshwa magari, kwa nini wasitumie magari yao waliyokopesha fedha na Serikali, magari haya yakaachwa wakapewa posho ya *petrol* na posho ya kufanyia *maintenance* gari hizi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunajua magari haya yanapokwenda *service* katika mawakala wahusika hakuna gari inarudi chini ya milioni tano. Tujiulize sisi

Wabunge nani anapeleka gari yake binafsi kwa mawakala hawa? Hatupeleki. Lakini gari ya umma inapelekwa kwenye wakala binafsi. Tujaribu kuwa na uzalendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najisikia vibaya, unapoona unapita na chombo kikubwa halafu unaona mama mjamzito anapakiwa kwenye baiskeli kupelekwa kuzaa wakati wewe una nafasi kubwa sana. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Makatibu Wakuu, Mashirika ya Umma, hatuzungumzii Serikali tu, tuwe na *morally grounds*, turudi nyuma tutazame nafasi zetu namna tunavyofanya matanuzi ambayo hayana maana. Naelewa yako maeneo Viongozi Wakuu wa nchi, ambao lazima wawe na magari makubwa, magari ambayo yanakwenda na hadhi yao.

Lakini sisi wengine tujaribu kutazama, sitaki kutaja majina magari kama napiga debe, yako magari ambayo ni *four-wheel* yangeweza kuwa-*maintain* Mawaziri, Makatibu Wakuu, Viongozi wa Mashirika na kadhalika kama kuna safari anakwenda kwenye *pool,* kwenye maeneo maalum, anapewa gari, inampeleke kwenye ziara. Mheshimiwa Waziri Mkuu nakushukuru na nakupongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wala Waheshimiwa Mawaziri, jamani wasinichukie, nazungumza kwa nia njema, maana nisije na hoja muhimu wakanikata bogi, nawaomba *morally grounds* wala si jambo lolote lingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nililisema kwenye bajeti ya mwaka 2009/2010, matumizi ya Serikali au tuseme matanuzi ya Serikali yapungue. *Hostility measures* zinakwenda kwenye mambo mengi yasiyo ya msingi, sio posho peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu nyumba za Serikali, wameuziwa baadhi ya viongozi, wameuziwa kwa masharti. Wameuziwa kwa mikataba ya namna gani nyumba zile zinatakiwa zikae katika maeneo yale. Baadhi ya nyumba hizi mikataba imevunjwa. Kuna watu wamevunja nyumba hizi, wamejenga *condominiums* wanatengeneza fedha juu ya fedha. Sheria mara nyingi zinawabana wale wanyonge. Baadhi ya wakubwa sheria hizi haziwabani, inaonekana sheria zinawapendelea wakubwa. Nataka majibu haya nipewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie katika suala la viwanja. Juzi Manispaa ya Ilala walikuwa wanauza viwanja. Nimepata maombi ya watu zaidi ya 100 viongozi na wao wanataka viwanja. Viwanja vingapi mnataka, kila kikitoka kiwanja kiongozi anataka kiwanja. Pia lazima kuwe na mpango wa bei za viwanja kuwasaidia watu wenye kipato cha chini. Haiwezekani kiwanja ninachonunua mimi na jirani auziwe hivyo, hawezi kutoa, hana milioni tano, mimi ninazo yeye hana. Maeneo haya yakishaainishwa siruhusiwi kwenda huko, hii ipo Malaysia, ndio maana unakuta kuna *squatters* nyingi Dar es Salaam na maeneo mengine kwa sababu hawa watu wa kipato cha chini hawapewi fursa ya kupewa viwanja kwa bei nafuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa maendeleo, sikupata nafasi ya kuchangia *very nice perfect,* hii ndio *the way forward.* Lakini tusiende kwenye *process* tu twende kwenye *substance* ya *process. Mind setting* ya watu ilivyo, kama hawatabadilika na

watakabidhiwa miradi hii, tuta-*fell* sababu ya ubinafsi, tufa-*fell* sababu ya rushwa, tuta-*fell* kwa sababu maamuzi hayatolewi kwa maslahi ya umma bali yanatolewa kwa maslahi yake yeye na huyu anayeingia naye hizo shughuli. Kwa hiyo, lazima tubadilishe *mind setting* zetu. Viongozi, wananchi na wanasiasa wajue tunaelekeza nguvu zetu kwenye mpango huu ili wananchi waone *fruits* za Serikali yao ya awamu hii ambayo ndio imeleta mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume hii, inatakiwa ipewe meno. Maeneo ambayo watendaji watazembea kwa makusudi *he goes back home*, anafungisha virago na wapewe *target*, wanapewa *target* ya mipango ya maendeleo. Anapo-*fell* anaambiwa rudi nyumbani kwako au kwa mke wake au kwa mume wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii ni sikivu, jana Mheshimiwa Mbowe katoa hoja ya msingi sana, Mheshimiwa Wasira akaipokea, hii ndio *spirit* ya nchi yetu. Pale ambapo kuna hoja za msingi zinatoka Kambi ya Upinzani Serikali inatakiwa i-*accommodate* sababu tunazungumzia maslahi ya Kitaifa, sisi kila kitu tunaweza tukajua, lakini wenzetu wakijua pia tu-*accommodate*. Lakini na hawa wenzetu wawe wastaarabu, ili wananchi waone na wao wana uungwana kama tulionao sisi kwa kuwa na busara katika uendeshaji wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuungane pamoja, Vyama vya Upinzani viungane na Serikali kufanya mpango huu ufanikiwe. Mambo ya Chaguzi, mambo ya 2015 wananchi wenyewe watachagua. Watu wasianze kuonyesha kuna mipango mibovu, wao wana mipango mizuri, hiyo haitakuwa sahihi. Twende na *National Spirit* na mkiweza kujitahidi labda 2015 tutawapa viti vingine viwili vingine tutabaki navyo wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme. Umeme si suala la *TV* au suala la kuwasha taa tu, umeme ni uzalishaji, umeme ni ajira, umeme ni makusanyo ya kodi ya *TRA* ambayo yanashuka kutokana na kutokuwa na umeme. Naomba mpango huu na wahusika sasa hivi wajitahidi kuhakikisha mambo haya ya umeme yanapata muono mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu jana alisimama hapa akasema miaka hamsini hamjafanya kitu, nataka nimwambie ndugu yangu nchi hii ina *progress*. Nchi hii imepata mafanikio makubwa mpaka yeye kaweza kuingia Bungeni, bila mafanikio ya nchi hii bado angebaki hukohuko alipokuwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya nasema kutoelewa kwao au kutoona kwao si upofu wao, ni upofu wa mioyo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *message* kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu, nchi hii inawathamini ninyi, nchi hii imewajengea Vyuo, inawapenda, wazazi wanawapenda na sisi tunawapenda na Taifa hili linawategemea nyie, kama kuna mtu anawadanganya mgome huyo mtu anawadanganya, tayari yeye ana *Degree* na ana kazi, iweje wewe huna chochote na ndiyo ugome, kama kuna mtu anafanya hicho, msidanganyike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango hii inategemea vijana wa Vyuo Vikuu wa sasa hivi, rudini mashuleni, kama kuna hoja za msingi, kaeni chini zijadiliwe. *University students* hawavunji magari ya watu wala hawaandamani na mabango, haya wanafanya watu wahuni wa huko nchi zingine sio utamaduni wa nchi hii. Kikwete amewapa Chuo bila hata mpango wa Serikali, hamuoni jamani kuwa ni jambo la kushukuru? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie bandari kwa haraka haraka. Kenya 2008 walivyokuwa kidogo na matatizo kwenye nchi yao, waliweza Mombasa ku-*clear* makontena laki sita na kumi na sita elfu ya futi ishirini, *six-hundred and sixteen thousands containers*. Meli kwenye *port* ya Mombasa haikai zaidi ya siku tatu, ku-*clear container* moja ni siku saba, tuta- *champion* vipi *revenue* ikiwa bado tunazorotesha mipango ya bandari? Ndiyo maana nikaomba *shift* za *TRA* ziende mpaka usiku, masaa ishirini na nne sio kutoa mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo. Lazima tuandae watu na tuwahamasishe, kuna nchi hapa nafikiri Ethiopia imechukua vijana elfu kumi inawaandaa katika kilimo kwa sababu walimaji sasa hivi hawawezi kulima tena, hawa vijana wote wanakimbilia mjini, lazima kuwe na program maalum ya kusaidia hawa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, Serikali isikwepe kushirikiana na watu wa michezo, *TFF*, ili wawe na programu kwenye mashule, Serikali isiepuke kuachana na masuala ya sanaa na muziki wa kizazi kipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, mpango wa maji naupongeza sana ambao umeletwa kwa Mkoa wa Dar es Salaam ambao 2013 utakwisha. Tunaomba Serikali iendelee kujenga daraja la Kigamboni, ni muhimu sana sasa hivi, mradi ambao unasemwa sasa huu ni mwaka wa sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia gharama za hospitali ya Taifa Muhimbili. Vipimo bado vina hali ya juu sana, sisi tunaona kwa sababu tunafuatwa anakuja mtu na cheti cha Hospitali ya Muhimbili, kipimo laki moja, laki moja na nusu, wananchi wa kawaida hawawezi. Itazamwe na hospitali hizi hazitakiwi kufanya biashara, zinatakiwa vitu hivi vikishanunuliwa wasaidie wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pato lingine la Serikali ni bahati nasibu ya Taifa. Sijui kwa nini Serikali haitaki kuji-*engage* kwenye *National Lottery*, kitu ambacho duniani kote kinaendeshwa na vyombo vya umma, ndiyo njia rahisi ya kumtoza mtu kodi. Kwa hiyo, naomba katika mipango ya miaka hii, wajaribu Serikali kutazama upya kurudisha *National Lottery* na kuweza kupata mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kazi za wanafunzi wa Vyuo Vikuu wakati wa likizo. Hizi Halmashauri zitenge bajeti za *summer jobs* kwa hawa wanafunzi, zitawasaidia kutokuzurura, watapata uzoefu, watapata pesa na hizi fujo zote zitakwisha, fujo hizi zipo kwa sababu na wao wanataka kujiona wanatambulika na sisi tunataka tuwaambie tunawatambua, tunawathamini, tunawapenda na pale kwenye matatizo yao wayaseme yashughulikiwe kwa njia za kistaarabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya, nizungumzie kilimo kwanza. Hatuwezi kuwa na kilimo kwanza kama hatuna mpango mzuri wa mbegu, matrekta na pia hatuvuni maji. Lazima tuwe na mpango wa mbegu, JKT mwaka jana walipewa kazi ya kuzalisha mbegu tani laki moja, wameweza tani elfu moja tu kutokana na kuwezeshwa kwao kidogo sana. Kwa hiyo, naomba Serikali iweke mkazo kwenye *issue* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo nashukuru na kama Serikali itafikiria tena suala la JKT alizungumza Mheshimiwa Chomboh jana, ni jambo muhimu sana, Serikali hii, vijana hawa wanayumba sababu hakuna chombo kilichoweza kuwaonyesha *national spirit* na JKT ndiyo itakayokuwa kitu cha kuweza kuwapeleka na kuwapa nidhamu na kuonesha uchungu wa Taifa lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru na nampongeza sana Waziri. Naunga mkono hoja mia kwa mia na ninamtakia kila la heri Mheshimiwa Waziri aendelee, afanikishe na kila mtu aone mabadiliko yatakayofanywa mwaka huu na 2016. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa Zungu kwa mchango mzuri, sasa nitamwita Mheshimiwa William Mgimwa na Mheshimiwa Halima Mdee ajiandae.

**MHE. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba tena kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa *presentation* yake nzuri juu ya bajeti hii. Nina mambo manne ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, nimeona kwamba ni muhimu sana tuanze na *management* yaani *public financial management*. Mheshimiwa Waziri alipokuwa anatoa tathmini ya *quality* ya *management* ya fedha za Serikali alieleza mambo ambayo kwa kweli yalionyesha kwamba *performance* ya *financial management* sio nzuri. La kwanza, alitupa picha kwamba utendaji wa Wizara ulikuwa umepata *unqualified audit reports* ilikuwa imeteremka kutoka 87% to 77% na *qualified audit report* iliongezeka kutoka asilimia 10 mpaka asilimia 20, hii ni *financial year* 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Serikali za Mitaa, kwa maana Halmashauri zetu zilipata *report* inayofanana na hiyo kwamba *unqualified audit* ziliongezeka kutoka 58% mpaka 48.5% kwa mwaka huo huo. Halafu *qualified report* ili-*increase* kutoka 41% mpaka 48.5%. Sasa tathmini hii ya *performance* ya Serikali kiujumla kulingana na *report* ya *Auditor General* inaonyesha kwamba kulikuwa na sababu nne zilizokuwa zimechangia kwa matatizo hayo ya Serikali kuto-*perform* vizuri katika *financial management*. La kwanza, alieleza kwamba kuna upungufu katika *compliance* ya *international financial standards* na la pili alisema Serikali ilikosa mwelekeo mzuri katika utekelezaji wa matakwa ya *Public Procurement Act* ya 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni kwamba, kulikuwa na *weakness* ya *integrated financial management systems* yaani *IFMS* na nne ni kwamba, watendaji wetu wa

Serikali walikuwa hawatekelezi mapendekezo yaliyokuwa yametolewa na kaguzi zilizopita. Sasa katika hii, taarifa ya Waziri ilisema kwamba, wamechukua hatua mbili *to address this weakness*. Hatua ya kwanza, kuna *creation* ya *post* ya *Assistant Accountant General* na ya pili, ni *Treasury Registrar* wamei-*move* kwenda kuwa *Independent Agency*. Sasa hizi ni *measures* ambazo wamezichukua ku-*address* matatizo hayo manne ambayo nimeyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nasema hatua nzuri zimechukuliwa, lakini wanasema Waswahili au kuna usemi wa Kiingereza unasema "*the past is a replica of the future*". Kwa maana ikiwa tutaacha namna hii basi tutegemee hata fedha tunazozizungumza leo *performance* itakuwa kama hivi. Hizi juhudi mbili zilizochukuliwa na Serikali ni nzuri, lakini hazi-*address* matatizo yaliyoainishwa kwa usahihi kabisa na CAG. Kwa mawazo yangu, naona kwamba kunahitaji *critical training* katika maeneo haya ambayo *CAG* ameyabainisha na napendekeza kwamba, basi bajeti yetu kuwe na *reflection* ya *training* katika maeneo haya ambayo *CAG* ameonesha hatua hizi nzuri ambazo ni za ziada zilizochukuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, napenda kuzungumzia juu ya kuiandaa nchi katika *sovereign credit rating.* Sasa hivi tunazungumza uwezeshaji ili watu wa nje waweze kuja hapa wawekeze katika *basic industry* na *agro basic industries* ku-*promote production* na kwa hali hiyo kuongeza mapato ya nchi. Tukishakuwa *rated* tutapata nafasi mbili; kwanza, kupata *creditors*, halafu kuaminiwa na watu wa nje kuja ku-*invest* kwa sababu nchi itakuwa *rated*. Lakini, kuna mambo sita ambayo hao *international ratters whether* tunachukua *modes or standard and poor*, lakini wote wanaangalia mambo yale sita ambayo nikiyaangalia haraka haraka Tanzania imesha-*qualify*, yaani *political stability, economical growth, control and management of budget, control of financial management, inflation and balance of payment improvement.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya tumesha-*qualify* katika *parameters* ambazo tunaweza tukakubalika na kuwa *properly rated* na *international ratters*. *Report* ya Serikali inasema, Serikali inachukua hatua *to procure a consultant* kufanya kazi hii. Nashauri tuharakishe, kwa sababu *it is only through that process* tukishakuwa *ratted* tutapata nafasi ya *credibility* ya kukopeshwa na *investors* ku-*invest heavily* kwa sababu tutakuwa *internationally ratted*. Lakini sasa hivi lazima tutaendelea kuwa na vikwazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, *economic empowerment*. Waziri ameeleza vizuri kwamba kuna mkakati mzuri wa kuwawezesha vijana wetu ili waingie katika *economic process* na kwa hali hiyo ku-*contribute* katika *economic productivity*. Ni vizuri sana, lakini ameweka mikakati mitatu; wa kwanza, wataendelea kutumia utaratibu wa *National Economic Empowerment Policy* ambayo ni nzuri sana na pili, *training of entrepreneurs* na tatu ku-*promote participation* katika *economic activities* kwa kutumia *TASAF*. Ni maeneo mazuri, lakini hizi *productions* tunazozizungumza, hatuwezi tuka- *succeed* ikiwa *we don't quickly transform ourselves* kutumia *energy*, hili lilizungumzwa kwenye bajeti kwa nguvu, kutumia *energy* maana yake tutamke kwa kuongeza uzalishaji kwa

*distribution* ya umeme, hatupati dhambi kwa kukosa kutamka, lazima tutamke hili kwa sababu ndiyo nyenzo ya kisasa itakayo *promote effective production*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, hata tunapozungumza hapa, hata wenye vijiji vyangu vikubwa wanaweza wakajua sasa kwamba, kumbe bajeti itatu-*transform* sisi tulioko kwenye *productive areas* katika vijiji vikubwa hata huko vijijini. Nina vijiji vikubwa kama Magulilwa, Muugama, kiponzero na Wasa, tunapozungumza maneno haya wanaweza kupata *comfort* na kupata imani kwamba sasa Serikali inaposema kuna *economic empowerment* inalenga vichocheo, *drivers* sahihi za *economic empowerment.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kuna suala la revenues from Mining Companies, wote tumeambiwa hapa kwamba *they are not contributing properly on corporate tax* na sababu zimeelezwa. Lakini wao wanaeleza kwamba bado wanaendelea kwa miaka mingi ku-*sustain losses* na zile *losses* zinawa-*justify* wao kutolipa *corporate tax,* kitu ambacho nashauri ni lazima na sisi tuwe *strategically focused* katika suala la msingi la ku-*train Accountants* wetu katika *specialised skills* katika *mining sector*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi tukawa tuna-*investor but for twenty or thirty years* wana-*claim* hawapati *profit*, lakini kwa kiwango gani sisi tumejitayarisha to *prove what they are saying*? *How much are we investing* katika *specialised skills* za ku-*audit specialised firms* kama *mining industries*. Nashauri hayo ni mambo ya msingi, tutamke namna gani na kwa kiwango gani, *we will invest in these areas, to promote economic production.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele ya kwanza imepigwa, lakini naomba nimalizie kwa kusema, ukweli *production* ya *local authorities*, yaani wananchi wetu katika ngazi za Halmashauri, tuweke mikakati ambayo inafanana na mazingira ambayo wananchi wetu wapo na mazingira yale ni hasa ya ku-*empower* walio vijijini kwa maana ya ku-*promote productivity* kwa kuwasaidia kuwapelekea umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja na nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa Mgimwa. Sasa nitamwita Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Mwambalaswa ajiandae. Baada ya Mheshimiwa Mwambalaswa atakuja Mheshimiwa Kairuki.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa fursa hii, lakini vile vile niipongeze kwa dhati kabisa hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, nadhani leo Watanzania wameweza kupima katika upande mmoja na upande mwingine, wapi vichwa vinawaka moto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mwaka wangu wa sita kama Mbunge japokuwa naonekana kijana, lakini Wabunge wenzangu tuliokuwa nao wa CCM watajua kwamba hizi pongezi zao na matumaini yao tulianza nao kipindi hicho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mheshimiwa mmoja alizungumza akasema hatusogei, nikaona watu wanampondaponda sana. Lakini sote tunajua Tanzania sasa hivi pengo kati ya tajiri na maskini ni kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunajua Tanzania ya sasa hivi, miaka mitano kipindi cha mwanzo kile wakati wanaomba ridhaa, maskini walikuwa ni milioni 11, watu ambao wanaishi chini ya mstari wa maskini. Tanzania ya 2011 wameongezeka zaidi ya milioni tatu, tunajua katika bajeti hizihizi mlituahidi kwa kupitia mpango wa MKUKUTA, mtapunguza kwa vijana ukosefu wa ajira kutoka asilimia 12.5 miaka ile ya MKUKUTA wa mwanzo mpaka asilimia 6.5. Leo tunaambiwa na kitabu cha Mpango asilimia 14.6 ya vijana hawana ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo siyo kwa vijana, hiyo ni ukosefu wa ajira *generally*. Vijana wanatengeneza asilimia 60 ya hiyo, sasa tunapongezana tu. *UDOM*, mnaingiza siasa, wanafunzi mliwaahidi wenyewe, alikwenda Waziri Mkuu sijui na Mawaziri wengine mkawaambia mtapata fedha za *field*, inakuja barua wanaambiwa fedha za *field* hazipo, vijana wasitoke barabarani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmekaa vikao vya usiku huko, ndiyo nasikia mkaziwekaweka hatujui, sasa hamwezi kutumia siasa kusuluhisha matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashauri na *Education* nasikia huko kunaanza kuwaka moto kwa sababu wanatakiwa waende kwenye mazoezi. Sasa mtasema CHADEMA inawatuma, tekelezeni wajibu wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tutaandamana, kwa sababu tuna wajibu wa kuwaelimisha wananchi. Tutaandamana mpaka kitakapoeleweka ili kila mmoja atekeleze wajibu wake. Hatujaja kuuza sura hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitachangia kwa uchache, kwanza suala la sekta isiyo rasmi kuingizwa kwenye mfumo wa kodi. Mwaka 2003 tuliliondoa, kulikuwa na sababu za msingi. Hawa Wamachinga, sijui mama ntilie, watu ambao hawajui kesho yao ikoje, tunaenda tunawabinya. Leo Kambi ya Upinzani imeonyesha kwa namna gani makampuni makubwa, makampuni ya madini yanasamehewa kodi bila sababu. Hivi tunajiuliza kwa kudunduliza kutoka kwa hawa maskini ambao hawajui kesho yao ni nini. Serikali itapata pato gani inayoshindwa kufidia kwa hawa watu wanaosamehewa kodi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajikongoja Afrika Mashariki, wenzetu wanasamehe kodi kwa asilimia moja *point* kadhaa, eti sisi asilimia nne, ni aibu. Mimi natoka

Manispaa ya Kinondoni, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni. Kwenye Manispaa zetu kuna tatizo kubwa sana la ukusanyaji wa mapato.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kaa, tupokee Mwongozo. Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia Kanuni ya 64(1)(a), naomba niisome inasema; "Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge (a) hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli."

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni msomaji wa taarifa mbalimbali kwenye vyombo vya habari vya magazeti pamoja na *television.* Ninayo magazeti ambayo nimeyasoma leo ambayo yameeleza kwamba Serikali tayari imeshapeleka fedha katika Chuo Kikuu cha Dodoma kwa ajili ya wanafunzi kufanya mafunzo ya vitendo *(practice).* Sasa msemaji anasema Serikali haijafanya kitu kama hicho, ningependa labda athibitishe hilo au Mheshimiwa Mwenyekiti utoe Mwongozo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani Mheshimiwa Gosbert Blandes ulikuwa unatoa taarifa kwamba pengine Mheshimiwa Halima Mdee hakuwa na taarifa kwamba fedha zimetengwa na kwa sababu wewe umesoma kwenye vyombo vya habari. Lakini pia juzi tuliahidiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri hapa kwamba ndani ya siku tatu hizi mambo haya yatakuwa mazuri. Kwa hiyo labda Mheshimiwa Halima Mdee apokee hiyo taarifa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti,…

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Unajua huu unjuka ni mbaya sana. Kwanza Mheshimiwa Spika, ameshatoa *ruling* leo asubuhi kwamba Miongozo ina taratibu zake na hauwezi kutoa Mwongozo juu ya Mwongozo. Mwenyekiti ameshajibu. Lakini pili, taarifa…

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilinde basi.

**MWENYEKITI:** Hakuwezi kuwa na Mwongozo juu Mwongozo Mheshimiwa Mdee.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Huu ni Mwongozo mwingine Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mdee nafikiri wewe sema tu unapokea taarifa tuendelee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa siwezi kuipokea. Naikataa, haina mashiko. Serikali imechukua hatua baada ya wanafunzi kugoma na wanafunzi tunapozungumza hivi wamerudishwa, wamefukuzwa Chuo. Wanafunzi warudishwe ili mambo yaendelee, tusipoteze fedha za Serikali *unnecessarily. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ...

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mwongozo wa Mwenyekiti. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Ninatumia Kanuni ya 64(1)(g) ambayo inasema; "Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ninam-*recall* vizuri Mheshimiwa Halima Mdee, ametumia kauli ya kuudhi wengine mara mbili. Mara ya kwanza amesema hatujaja kuuza sura hapa, lakini mara ya pili amesema unajua lugha ya mtaani ambayo sisi vijana tunaielewa, lakini hapa si mahali pake kwamba unjuka ni mbaya. Mimi ningeomba Mheshimiwa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge sijakusikia hiyo.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mimi nimemsikia na nina uhakika wenzangu wamemsikia. Hata *Hansard...*

**MWENYEKITI:** Hiyo ya pili uliyoisema sijaipata vizuri.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Ya pili wakati ninaomba Mwongozo wa Mheshimiwa Halima Mdee, amesema unajua unjuka ni mbaya sana.

**MWENYEKITI:** Nini unjuka?

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sisi vijana mimi nidhani ni lugha ambayo inatuudhi. Hapa si mahali pake kwa kutumia lugha za mitaani. Ninakuomba Mheshimiwa Mwenyekiti utoe Mwongozo wako na kumsihi Mheshimiwa Halima Mdee kwa heshima kubwa ninayompa afute kauli zake hizi mbili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zainab Kawawa. Mheshimiwa Mbunge ni kweli kwamba kuna lugha ambazo zilitumika zilikuwa ni kali kidogo.

Hatukuja kuuza sura, unjuka. Mimi nilibakia nimeachwa sikuipata vizuri. *(Makofi/Kicheko)*

Mimi nadhani Bunge lina lugha yake na Mabunge duniani, Bunge letu siyo la kwanza. Mabunge duniani yana taratibu zake na sisi kwenye Kanuni zetu tumesema kabisa kuhusu masuala haya katika kifungu hiki cha 64 kwamba lugha inayotumika basi isiwe inayokerakera hivi na mimi naamini kwa sababu wewe ni Mbunge wa siku nyingi, utajaribu kuona namna ya kurekebisha neno hili. Naomba Mheshimiwa Mbunge ama uondoe au urekebishe uweke *alternative word. (Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema sisi hatukuja kuuza sura Kambi ya Upinzani, hatukuja kuuza sura, tumekuja kufanya kazi, tulikuwa tunajisemea sisi. Tukija kwenye suala la njuka, Zainab anajua. Ukiwa unaanza kidato cha kwanza ukiwa mpya, wewe ni njuka. Unaelewa? Yaani ni kwamba siyo tusi, ila ni *vocabulary* ya kawaida kwa mtu mgeni. Sasa ukizingatia kwamba Mheshimiwa Mbunge... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge samahani, samahani kidogo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Basi Mheshimiwa nisikupotezee muda wako, nimeiondoa nisikupotezee muda wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Endelea!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumzia juu ya dhamira ya Serikali kurudisha leseni za biashara ambapo kwa kiasi kikubwa itawaathiri wafanyabiashara ndogo ndogo. Lakini vile vile nikawa natoa msisitizo wa haja ya Serikali kuangalia kwa uzito hoja ambazo zimependekezwa na Kambi ya Upinzani juu ya kutoa misamaha ya kodi kwa makampuni makubwa yasiyokuwa na sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza hivi kwa sababu ni aibu kwa Serikali kupoteza zaidi ya shilingi bilioni 600 kwa msamaha peke yake. Hapo bado hujagusa mafuta, hapo bado hujagusa dhana ya uwekezaji kuwekeza kwenye madini katika dhana nzima ya kukopa. Sasa mimi nilikuwa nashauri Serikali kama ina dhamira ya kuongeza mapato isiangalie wale maskini, iangalie hiki kikundi cha matajiri na wakati huo huo tuangalie kwa namna gani hawa maskini tunawasogeza ili baadaye waje kusaidia kuongeza pato la Taifa. *(Makofi)*

Kwa Manispaa yetu ya Kinondoni ambayo tunaweza tukasema ni Manispaa yenye uwezo wa kukusanya mapato mengi, kwa mwaka wa fedha uliopita kwa mapato ya ndani peke yake walikusanya shilingi bilioni 15 tu. Mwaka huu kwa sababu ya uwepo wa Wabunge wengine wenye vichwa vingine tukaweza kusogeza mpaka shilingi bilioni 23. Lakini kuna tatizo la msingi ambalo Serikali ikilishughulikia tunaweza tukakuta Manispaa ya Kinondoni inakusanya kwa vyanzo vya ndani zaidi ya hata shilingi bilioni 100, kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiit, ukienda leo Manispaa, ukiwaambia tupatie taarifa ama *database* ya majengo ambayo yapo kwenye Manispaa yenu, kama wanayo taarifa ya mwaka 2005 ama 2006 kushuka chini, ukiiambia Manispaa tupatie taarifa ya wanyabiashara wakubwa na wadogo na wawekezaji wakubwa na wadogo ndani ya Manispaa hawajui. Lakini wakati huo huo vyanzo vya ndani vya Manispaa vinategemea ama wawekezaji kwa mantiki ya kuangalia *0.3 turnover* ambayo wanalipa kodi kwa mwaka. Wanategemea *property tax* hawajui. Sasa sisi tunaomba kwa sababu nyie ndiyo mko *incharge,* si ndiyo mko upande wa huko mwaka 2015 baadaye muangalie hata kwa kutumia gharama, hata kwa kuchukua *consultant* ambaye anafanya kazi kibiashara zaidi, aende aainishe masuala ya msingi ya kuweza kupata mapato kwenye Manispaa ya Kinondoni kwa sababu mimi ndiyo naijua, najua mapungufu yake. *I can guarantee you*, tukiwa na hiyo *database* na tukiwaondoa wale Maafisa Biashara wezi Manispaa yetu ina watu wenye risiti mbili, mbili, risiti moja ya Serikali, risiti moja yake mfukoni na cha ajabu wanapewa ufanyakazi bora. *(Makofi)*

Naomba mtekeleze wajibu wenu ili hawa vijana wetu Wamachinga, mama ntilie, wanaotembeza tembeza biashara hizi ndogo ndogo, wenye viduka vya hapa vya kubangaiza, wasubiri neema ikiwajia kwa kuwa na kwenyewe kuwawezesha waweze kuchangia katika kuliendesha Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika hoja ya pili ya kilimo. Kwanza, ninasikitishwa na masuala kadhaa, hatuko *consistent*, sikatai umuhimu wa vipaumbele ambavyo tumevianisha sasa hivi, lakini hakuna kitu cha muhimu sana kama kuwa na mwendelezo. Tulikuja na kauli mbiu ya Kilimo Kwanza, baada ya kuja na kauli mbiu ya Kilimo Kwanza, kuna haka kakitabu haka, nilipewa Ofisni kwa Mheshimiwa William Lukuvi, tulivyoenda Kamati yetu. Naamini bado kako *valid.* *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haka kakitabu kalisema ambako kalisainiwa na Mheshimiwa Rais, hapa, lazima nionyeshe uhalali, msije mkasema kwamba Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wetu. Akasema nguzo ya pili ya Kilimo Kwanza kuongeza Bajeti ya Serikali kwa ajili ya Kilimo Kwanza, kutenga si chini ya asilimia 10 ya Bajeti ya Serikali kwa sekta ya kilimo. Hakuna asiyejua kwamba sekta ya kilimo ndiyo yenye asilimia kubwa ya nguvu kazi ya ajira zaidi ya asilimia 74. Kwa hiyo, kama tunasema kwamba tunataka kutengeneza ajira, tukiboresha kilimo, *automatically* vijana ambao mnasema wanakuja mjini, watabaki kule vijijini. *(Makofi)*

Lakini Bajeti ya sasa hivi tumepewa shilingi bilioni 930 na kadhaa, sasa hii hoja hapa ya Mheshimiwa Rais ya asilimia 10 maana yake tulitegemea ingekuwa trilioni moja na ushehe, trilioni 1.3. Sasa hapa Mheshimiwa Rais maana yake ndiyo tumepigwa changa la macho kwenye hii. *No consistence. (Makofi)*

Hapa wanasema, kuongeza Bajeti ya umwagiliaji kufikia hekta zisizopungua milioni saba ifikapo mwaka 2015. Haya, tukija kwenye mpango wa jana ambao tumeupitisha, 2015 hekta milioni moja, sasa hivi anavyoviandika Mheshimiwa Rais na mnamsainisha kama hazikuwa *document* halali basi tusingepewa. Ni vitu vya aibu,

mnamtia aibu Mheshimiwa Rais wetu.  Sasa mpango wa kilimo kwenye ukurasa wa 11 wa Bajeti ya Mheshimiwa Waziri, amezungumzia mpango wa mapinduzi, anazungumzia *Southern Agricultural Corridor (SAGCOT).* Lakini nimeupitia huu mpango wa *SAGCOT.* Mpango wa *SAGCOT* ukiuangalia kwanza unavyoonyesha malengo yake makubwa ni wafanyabiashara ama wakulima wakubwa, halafu wale wakulima wadogo wadogo wa-*benefit* kutokana na wale wakulima wakubwa, *out growers* mnawaita sijui.  Hawa wadogo hawa…

Mheshimiwa Mwenyekiit, ukiangalia hizi fedha zilizotengwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, muda wako umekwisha.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimamishwa dakika tano.  *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** *Time keepers* wamezingatia hata hizo dakika.
Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, sasa nitamwita Mheshimiwa Victor Mwambalaswa na baadaye atafuatiwa na Mheshimiwa Angellah Kairuki na baadaye Mheshimiwa Dunstan Kitandula.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi hii na mimi nitoe mawazo yangu machache, kwa hoja hii iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

Awali ya yote, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, rafiki yangu Mheshimiwa Mustafa Mkulo, pamoja na Naibu Mawaziri wake wote wawili na Katibu Mkuu na Makatibu Wakuu Wasaidizi na viongozi wote wa Taasisi kubwa, Benki Kuu, Mamlaka ya Mapato na Takwimu mmefanya kazi nzuri kubwa na nzuri, hongereni sana.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengine lazima waseme, wakiponda waache waponde, lakini midomo tumepewa tu bure na Mwenyezi Mungu.  Napenda kuwashukuru wananchi wangu wa jimbo la Lupa kwa kunichagua kwa mara ya pili kuwawakilisha Bungeni.  Ninawaahidi kuwa sitawaangusha na baada ya Bunge la mwezi wa nne nilipita kwenye Makao Makuu ya Kata, kila Kata kuwashukuru wananchi na kuchapa kazi kutimiza Ilani ya Uchaguzi ya CCM.  Ninawaahidi kuwa nikija mwezi wa tisa Mungu akijalia nitaenda kwenye vijiji vyote na vitongoji vyote na kuchapa kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambalaswa unasema?

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 151 ya Kanuni za Kudumu za Bunge lako Tukufu inasema wazi kwamba pongezi zote za Wabunge zitatolewa na Mheshimiwa Spika na leo asubuhi Mheshimiwa Mwenyekiti tumekumbushwa wakati wa kikao kwamba pongezi zinatolewa na Spika kama ni za Wabunge na zinatolewa na Waziri Mkuu kama ni za Serikali. *(Makofi)*

Sasa Mheshimiwa huyu, Mheshimiwa anayepongeza wapigakura wake, anatupotezea muda, anakiuka Kanuni ya 151. Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Tundu Lissu, sasa wewe ndiyo uliyetupotea muda. Kwa sababu yule alikwishamaliza na alikuwa sasa anaendelea na alikuwa ametumia muda mdogo sana kuupoteza.

Mimi niseme tu, labda niseme tu Waheshimiwa Wabunge, Bunge hili tunafanya kazi kwa *time.* Kama kuna kitu kinachotuongoza hapa, tunafanya kazi kwa *time.* Kama kuna kitu kinachotuongoza hapa ni muda, matumizi ya muda. Sasa kwa yule alikwishapoteza muda, wewe kama una nia ya kusaidia muda huo, basi maana yake ungeacha maana yake sasa ndiyo umepoteza muda zaidi. *(Makofi/Kicheko)*

Mimi niombe sana Waheshimiwa Wabunge, ni vizuri yule ametumia muda wake, hoja zile ni zake ingawa Kanuni inasema, lakini Kanuni haitafsiri peke yake, lazima itafsiriwe pamoja hekima, busara na taratibu za uendeshaji wa Bunge duniani. Mheshimiwa Mwambalaswa endelea. *(Makofi)*

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninawaambia wananchi wangu wa Jimbo la Lupa kwamba safari tuliyopanga ya watu watatu, watatu, kila Kata, mmefanya vizuri, mimi nimefurahi na nikirudi mwezi wa tisa, *Inshallah* tutakwenda kumi, kumi kila Kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo sasa naomba nitoe mchango wangu kwenye Bajeti ya Serikali. Mimi nitajielekeza kwenye manunuzi na udhibiti wa fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imechukua hatua mbalimbali nzuri za kudhibiti mapato ya Serikali. Kwanza mwaka 2006, Serikali iliajiri wahasibu wengi, ikawafundisha, ikawapeleka kwenye Halmashauri kwenda kudhibiti fedha kwenye Halmashauri. Pili, kwa mwaka huu Serikali imemuajiri *Accountant General* Msaidizi ambaye atashughulika na fedha za Halmashauri, moja. Pili, imeajiri Mkaguzi Mkuu wa Ndani; ni jambo zuri sana, Mkaguzi Mkuu wa Ndani kudhibiti fedha za umma. Hii kazi ni nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema pamoja na mambo yote haya ambayo Serikali inayafanya, mimi naipongeza sana lakini natoa ushauri wangu. Leo, Mheshimiwa Waziri Mkuu amenigusa kwenye sakafu ya moyo wangu, Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliwahi kutangaza kwamba, aah, hakutangaza yeye, ilitangazwa kwamba alinunuliwa gari aina ya *VX,* akalikataa! Sasa leo nimemuona anaingia Bungeni

amepanda *GX* yaani amenigusa kweli kweli, kapanda *GX!* Na mimi nasema Mheshimiwa Waziri Mkuu, nikija mwezi wa tisa nitakuletea debe la asali kutoka nyumbani kwetu. Huo ndio uongozi unafanywa kwa matendo, *walk the talk,* amepanda *GX.* Sasa naishauri Serikali, kuwe na sera ya magari ya Serikali, sera ya magari ni ipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Kenya wao gari la Serikali ni *Volkswagen Passat,* ndio wanalotumia, ndio sera yao. Wenzetu wa Zambia, magari wanayotumia ni *Landcruiser Prado* na *Double Cabin.* India wanatumia gari lao kale kadogo kale, sijui kanaitwa *Mohindra*, sijui Mahindra, ndio gari la Serikali! Sasa gari letu ni lipi na sisi? Sasa kama Mheshimiwa Waziri Mkuu anatumia *Landcruiser GX,* ina maana Mawaziri wengine watumie lile *Landcruiser GX Standard,* lile jeupe lenye mkonga lile; ni *four wheel drive,* ni *comfortable,* ndio sera ya magari. Mheshimiwa Waziri Mkuu nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee sasa wataalamu wa ugavi. Bajeti ya Serikali ni shilingi trilioni 13.5. Trilioni 8.6 matumizi ya kawaida, na hii ya kawaida 70% inaenda kwenye manunuzi. Ya maendeleo ni trilioni 4.9 hii mia kwa mia inaenda kwenye manunuzi. Sasa Serikali imefanya jambo zuri sana, inafundisha wahasibu, wakaguzi, peleka kwenye Halmashauri, kwenye Wizara, kwenye Taasisi, safi sana. Lakini wanunuzi, hawa ndio wanaopoteza hela ya Serikali hawa wanunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mifano miwili midogo tu. Ujenzi wa barabara kilometa moja sasa hivi inafikia shilingi bilioni 1.5, lakini ujenzi wa barabara hiyo hiyo ya kilometa moja kwa mpango wa *millenium challenge account,* inakwenda karibu shilingi bilioni moja wanunuzi, kwa hiyo, ni wajibu sasa wa Serikali kuajiri, ku-*train* na kuwasimamia wanunuzi na pia kuimarisha kitengo cha kuwasimamia, kama Serikali inaweza ikaajiri *Accountant General* wa kudhibiti watu wote mpaka kwenye Halmashauri, kuwe na kitengo cha kudhibiti wanunuzi kwenye Idara, kwenye Taasisi na kwenye Halmashauri, hawa ndio wanaosaini mikataba. Nimesema 70% ya kawaida, 100% ya maendeleo, wanunuzi waajiriwe, wafundishwe, ili kuweza kudhibiti fedha za matumizi.

Sasa naomba uniruhusu ninukuu kwenye kitabu cha Bajeti ya Mheshimiwa Mkulo hiki, ukurasa wa 53, kuhusu kudhibiti matumizi ya Serikali. Ukurasa wa 53 pale (b); "Aidha Serikali itaendelea na juhudi zake za kudhibiti matumizi yake kwa kusitisha ununuzi wa magari ya aina zote, isipokuwa kwa sababu maalum na kwa kibali cha Ofisi ya Waziri Mkuu. Vile vile Serikali itasitisha ununuzi wa samani za ofisi, hususan zile zinazoagizwa nje ya nchi. Kupunguza malipo ya posho mbalimbali yasiyokuwa na tija, kupunguza matumizi ya mafuta kwa magari ya Serikali, kupunguza safari za ndani na za nje ikiwa ni pamoja na ukubwa wa misafara na pia kuendelea kupunguza uendeshaji wa semina na warsha, isipokuwa pale inapobidi na kwa kibali cha Ofisi ya Waziri Mkuu." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kupunguza matumizi, kuondoa posho ambazo hazina tija ni ya Serikali. Sasa sisi wanasiasa ambao tunaiteka iwe ya kwetu! Aah, labda niseme hapa, kiongozi wa kwanza duniani ambaye aliachia mshahara wake na stahiki zake zote kutoka kwenye Serikali ni Rais John F. Kennedy wa Marekani, alisema bwana mimi ukoo wangu una hela za kutosha, tunajiweza, kwa hiyo, mshahara wa Serikali na posho zote hizi pelekeni kwenye *charity.* Sasa kama kuna kiongozi wa siasa ambaye yeye ana siri ya kupata mapato mengine au familia yake inajiweza, afanye hivyo, kusiwe na *drama, why the drama? Drama* ni ya nini? *(Makofi)*

Naomba ninukuu tena Bajeti, ukurasa wa 50; "Serikali kwa mwaka 2011/2012 itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za udhibiti wa matumizi ikiwa ni pamoja na kuimarisha ukaguzi wa mishahara, ambapo Maafisa Masuhuli watafanya ukaguzi wa malipo ya mishahara ya Asasi, Taasisi zao kila mwezi." Ni jambo zuri sana hili, naomba wanapodhibiti hii mishahara na mishahara hewa ya watumishi wa Serikali, naomba tuwatilie maanani wafanyakazi katika Halmashauri ambao wako mbali sana na Makao Makuu ya Wilaya, ambako ndio kuna huduma za benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya kama Chunya kuna wafanyakazi walimu, hasa walimu. Mwalimu anatoka Kambi Katoto, mwalimu anatembea zaidi ya kilometa 200 kwenda kuchukua mshahara wake benki! Mwalimu anatoka Udinde, zaidi ya kilometa 200 kwenda benki kuchukua mshahara. Mwalimu anatoka Namkukwe, zaidi ya kilometa 200 kwenda kuchukua mshahara. Akiwa ni mwalimu wa kike, anafika Chunya anakuta mshahara haujafika, anakaa *guest house,* hela hana; inabidi anaolewa kwa nguvu. Akipata mshahara, utaishia kwenye nauli kurudi nyumbani kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akiwa mwanaume, vile vile! Atakuja Chunya, atakuta mshahara wake haujafika benki, kwa hiyo, nusu ya mshahara unaishia kwenye nauli! Naomba sana Serikali iruhusu, iziagize Halmashauri ambazo zina maeneo makubwa sana kama ilivyo Chunya, wapeleke huduma za kibenki karibu na wafanyakazi wetu ili kuwapunguzia adha hii wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba niongelee suala la kupunguza makali ya maisha ya wananchi kwa hali iliyopo hivi sasa. Serikali imesema itachukua hatua madhubuti, kwanza kwa mfano kwenye bei ya petroli, kupunguza tozo ambazo ziko zaidi ya 21 pale.

Lakini nikisoma *Finance Act* ya mwaka 2011, pale katika madhumuni na sababu anasema, "Sehemu ya 8, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya ushuru wa petroli." Sura ya 220, "Marekebisho haya yanakusudia kuwezesha kurahisisha ulipwaji wa tozo za mafuta katika fedha za kigeni, inayoweza kubadilishwa katika shilingi ya Tanzania." Nadhani hapa Serikali, kwa kuwa ina mpango wa kuanza kununua mafuta kwa pamoja kwa kuitumia *TPDC,* itaondoa tozo hizi ambazo ndio zinaongeza bei ya petroli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo Taasisi ambazo zina tozo tatu au nne kwenye bei hiyo hiyo! Kwa mfano, *TBS. TBS* wana tozo mbili, haya makampuni ya mafuta haya, wana tozo tatu au nne kwenye bei hiyo hiyo. Kwa hiyo, Serikali itakapokuwa imeamua imeanza ambapo imesema itafanya mwaka huu, imeanza kununua mafuta kwa pamoja kwa kutumia Taasisi ya Serikali, itaondoa tozo zote hizi na itaondoa mzigo kwa bei ya petroli kwa wananchi na itashusha bei ya bidhaa nyingi za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie, Mheshimiwa Kabwe Zitto, mdogo wangu, nimemfurahia sana. Alipomaliza yeye amesema na ninakachukua kamoja tu anasema, tukiendeleza Umoja wa Kitaifa, mshikamano na kulinda haki za raia, tunaweza. Tukiendeleza Umoja wa Kitaifa Tanzania, tukiendeleza mshikamano wa Watanzania na kulinda haki za raia, tunaweza na mimi nasema, ahsante sana Mheshimiwa Zitto, nasema na sisi wanasiasa tukiweza kuwa na kiasi, *yes we can.* Tuwe na kiasi wanasiasa, sisi ni kioo cha jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa wamesema kuhusu wanafunzi wa *UDOM.* Wanafunzi wa *UDOM* wa *Humanities* hapa, wao ilikuwa haipo kawaida kwenda *field work,* haikuwepo kawaida hiyo! Wakaanza mchakato wa maongezi na Serikali waende *field work.* Wamekwenda kwenye mazungumzo wameongea, wameanza na kugoma goma kwa kushauriwa na watu fulani, lakini sasa jana Serikali imewaambia kwamba hela yenu inaletwa mwende *field,* bado wanagoma! Bado wanagoma kwa sababu ya kushauriwa na watu fulani. Sasa leo wamefukuzwa wanafunzi 400 wa chuo hiki cha *Humanities,* wamefukuzwa. Mnaambiwa hela inakuja, mnagoma nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kama pale ambapo kwenye Muswada wa Katiba, Kamati ya Katiba imesema wadau njooni tuongee Muswada huu wa kuunda chombo cha Katiba, wanakuja kwa maandano, wanataka kuingia getini! Njoo utoe mawazo yako, unagoma nini? Sasa jamani, wanasiasa tukiwa na kiasi, *yes we can. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hiyo. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye hoja hii muhimu ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2011/2012. Napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuja na Bajeti nzuri, Bajeti ambayo imepangika na ambayo inatarajia kumboreshea maisha Mtanzania wa kipato cha chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pia pongezi kwa Serikali kwa misamaha mbalimbali ambayo imeitoa, hususan katika zana za kilimo, mifugo pamoja na uvuvi. Ni

imani yangu kwamba Serikali lengo lake ni kuhakikisha kwamba sekta hizi zinaweza kuzalisha na hivyo kuongeza pato letu la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa jitihada mbalimbali ambazo inazichukua katika kupunguza utegemezi wa Taifa letu katika misaada ya wabia wa maendeleo. Ukiangalia takwimu zetu za mwaka 2007/2008 tulikuwa tukitegemea misaada ya wadau wa maendeleo au wabia wa maendeleo kwa 28%. Lakini jitihada kubwa zimefanywa na Serikali yetu, Serikali ya Chama cha Mapinduzi na hivi sasa ni 17% tu ya pato letu ndio linatoka kwa wabia wa maendeleo. Pongezi sana Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali yangu kwa jitihada mbalimbali inazozichukua katika kudhibiti matumizi, hususan nipongeze katika sera ya ununuzi wa samani. Lakini pia nitoe ombi au rai, tujitahidi na bidhaa nyingine, ukiachilia mbali samani, tuweze kununua za kutoka humu humu ndani nchini kwani kwa kufanya hivyo tutawawezesha watu wengi ambao hawana ajira, waweze kujipatia ajira na hivyo kuchangia katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nipende kumshukuru pia Mheshimiwa Rais wangu, nikiwa kama mwakilishi wa wafanyakazi kupitia chama changu; alihudhuria sherehe yetu ya wafanyakazi yaani siku ya Mei Mosi na alipohudhuria, tulitoa maombi mbalimbali kama wafanyakazi na moja ya maombi hayo ni kuongezewa kima cha chini cha mshahara wa mfanyakazi. Naamini kupitia kwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, tumeelezwa kwamba katika siku za baadaye, kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Wizara ya Kazi, kutakuwa na nyongeza ya mishahara. Ni imani yangu kwamba Serikali itajitahidi na itakuwa imezingatia maombi ya wafanyakazi na ninaamini watahakikisha wanakidhi matarajio ya wafanyakazi hawa, kama walivyoomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kwenda kwenye hoja ya posho. Huko zamani hapa kwenye Bajeti tunaelezwa kwamba zimetolewa msamaha wa kodi, hususan katika Wizara na Taasisi ambazo zinapata ruzuku kutoka katika Serikali. Hili sio jambo jipya, tofauti tu ni kwamba sasa hivi limehalalishwa. Huko awali watumishi mbalimbali mfano wa mashirika ya umma yanayopata ruzuku ya Serikali kwa 100%, mfano Hospitali ya Muhimbili, walikuwa wakikatwa kodi; lakini wa sekta ya umma wengine kama Wizara, walikuwa hawakatwi kodi. Kwa hiyo, nadhani hapa walijitahidi tu kuangalia kuondoa ubaguzi, kwa hiyo, kwa mtumishi wa Serikali, hakuna tofauti yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba wapo wafanyakazi wa aina mbili, wapo wale wa sekta ya umma na wapo wa sekta binafsi. Ukiangalia Bajeti hii ambayo imeletwa na Serikali, inapendekeza kutoa msamaha wa kodi ya posho kwa wafanyakazi

wanaotegemea ruzuku za Serikali. Lakini tunafahamu kwamba pia katika kodi ya ajira yaani *pay as you earn* na watumishi wa sekta binafsi na wenyewe wanachangia kwa kiasi kikubwa, tena kushinda hata wa sekta ya umma na wote wana gharama za maisha ambazo wanatakiwa wazimudu; hivyo basi, kwangu mimi naona hapa kidogo ni ubaguzi na tuiombe tu Serikali ijitahidi kuweza kuliangalia hili na kulirekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, si kila mmoja anayepata posho. Kwa hiyo, kwa hapa kwenye gharama za maisha hapatakuwa na tofauti yoyote. Tuiombe tu Serikali izingatie kuboresha mishahara ya watumishi hawa, hususan ijitahidi kupunguza kodi ya ajira. Hivi sasa kodi ya ajira inayokatwa ni 14%, katika Bajeti ya mwaka 2010 ilikuwa ni 15%, ikapunguzwa kuwa 14%. Kwa hiyo, tuiombe Serikali, kupitia Kambi ya Upinzani wamependekeza 9%, mimi ningeomba hata 5% ikiwezekana hata 2%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe pia katika kodi ya ajira inayotozwa katika kipato cha chini; hivi sasa mtu anayepata mshahara wa 135,000/= kwenda chini hakatwi kodi ya ajira; kwa hiyo, tuiombe Serikali ijitahidi wanapotoa hii nyongeza ya mishahara, ikiwezekana hata laki tatu, laki nne kwenda chini na wao pia wasiweze kukatwa kodi ya ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia takwimu za Mamlaka ya Kodi, watumishi wanachangia shilingi bilioni 832, ukiangalia takwimu za mwezi Mei, 2011, wakati makampuni mbalimbali yanachangia shilingi bilioni 405. Kwa haraka haraka ukiangalia hapo watumishi wanachangia mara mbili zaidi ya makampuni. Lakini watumishi hawa hawapati misamaha ambayo inawasaidia wao kuweza kumudu gharama za maisha. Hapo hapo ukiangalia makampuni wana misamaha mbalimbali ya kodi! Kwa hiyo, nitoe rai tupunguze na ikiwezekana zile *incentives* mbalimbali tunazozitoa kwa makampuni ziangaliwe kwa makini na ikiwezekana kupunguzwa ili jamani mtumishi huyu ambaye anatuchangia zaidi ya mara mbili, asiweze kunyonywa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuchangia kwenye suala la pensheni. Ukiangalia kiwango cha chini kabisa cha mwezi anachopata mtumishi aliyestaafu, anapata 50,000/=. Mimi ningependa kushauri ikiwezekana, tuendane na nchi nyingine, kima cha chini hiki cha pensheni kiendane na kima cha chini cha mshahara. Tukifanya kima cha chini cha mshahara ni 200,000/= basi na kima cha chini cha pensheni yake ya kila mwezi na yenyewe iendane hivyo hivyo 200,000/=. Naamini hiyo itakuwa imesaidia sana kumboreshea yule mstaafu kuweza kumudu gharama za maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuchukua fursa hii kupendekeza riba kwenye mikopo ya wafanyakazi. Hivi sasa tunaona jinsi ambavyo wafanyakazi wetu wanakamuliwa, ukiangalia katika Halmashauri walimu na watu mbalimbali wa kwenye sekta ya afya, wanatozwa riba kweli kweli. Nipendekeze Serikali itenge fungu fulani na

izipeleke kwenye mabenki, kama tunavyofanya *window* hii ya *TIB* kwa ajili ya kilimo, basi fedha hizi ziweze kutumiwa na watumishi kwa riba nafuu, ikiwezekana 5%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo naomba nirudi kwenye posho za *sitting allowance* ambayo imechangiwa katika mpango wetu wa maendeleo ya Taifa. Nipende tu kushauri tumeelezwa kwamba kufutwa au kuisha, lakini mimi ningependa wadau hapa ni wengi na naamini huko nyuma waliopanga posho hizi walikuwa na maana na posho hizi ni muhimu sana, naamini watumishi wana mabaraza mbalimbali ya majadiliano katika utumishi wa umma. Ukiangalia kwa Bunge ipo Tume ya Huduma za Bunge, vilevile kwa Mahakama, kwa hiyo, tukae tuangalie kwa pamoja kabla ya kufanya maamuzi yoyote kwani ni muhimu na walioziweka hizi walikuwa na maana zao na ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kupendekeza kwenye mabadiliko kuhusiana na kodi ya ongezeko la thamani yaani *VAT,* sisi tunatoza asilimia 18, lakini ukiangalia na sisi ni wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao wenzetu wanakatwa asilimia 15. Kwa hiyo, nipendekeze na sisi hatuko kwenye kisiwa, tupunguze ili tuweze kuwa in *harmony* na matakwa mbalimbali ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, na naamini kwa kufanya hivyo mtumishi wa kawaida pamoja na mwananchi mwingine wa kawaida atakuwa ameweza kununua bidhaa na kupata *gain* ya asilimia tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kabla kengele hiyo haijagonga naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, ahsante na nashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Angellah Kairuki mchangiaji wetu wa mwisho lakini kama muda utaruhusu lakini sidhani mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Zakia Meghji. (*Makofi)*

**MHE. ZAKIA H. MEGHJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nami nikushukuru kwa kunipa nafasi hii siku ya leo kuweza kuchangia Bajeti hii ya mwaka 2011/2012, na moja kwa moja niseme naunga mkono Bajeti hii. *(Makofi)*

Napenda pia kwa sababu nazungumza kwa mara ya kwanza kumpongeza Mheshimiwa Spika, mama Anne Makinda kwa kuchaguliwa kuwa mwanamke wa kwanza Spika Tanzania na naona wenzetu wa Uganda wametufuata nyayo kumchagua Rebecca Kadaga kuwa naye Spika. *(Makofi)*

Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Naibu Mawaziri, pamoja na timu yote iliyoandaa Bajeti hii na napenda kwa kupitia Wizara ya Fedha kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi au Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi kwa Bajeti hii nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti hii kwa kweli imepongezwa na vyombo na taasisi mbalimbali na wananchi mbalimbali, lakini tunajua kwamba baadhi ya Wapinzani wataiponda tu na wataipinga, kwa sababu wao ni Wapinzani hata kama kitu kizuri watasema si kizuri, hata kama kitu kimefanyiwa kazi watasema hakijafanyiwa kazi. Mara nyingine hata kama kitu cheusi watasema basi ni cheupe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti hii nasema ni nzuri kwa sababu zifutazo; kwanza kabisa inaanza kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi baada ya uchaguzi. Wakati wa kampeni za uchaguzi vyama mbalimbali vilikwenda kwa wananchi kuomba kura na vilieleza ilani zao ni jambo gani ambalo watafanya wakiingia madarakani. Kwa hiyo, hili nalo baada ya kuingia madarakani ahadi ya Chama cha Mapinduzi inatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba vipaumbele vyote ambavyo vimetolewa ni kutokana na ahadi hiyo hiyo ya Chama cha Mapinduzi, ukiangalia maji ukachukua Ilani ya Chama cha Mapinduzi ipo ukurasa wa 67 mpaka 71, ukiangalia umeme, ukiangalia maji, ukurasa 119 mpaka 121, ukiangalia miundombinu na usafiri pamoja na usafirishaji ukurasa wa 72 mpaka 82, kilimo na umwagiliaji ukurasa wa 29 mpaka 38, kupanua ajira ukurasa wa 92 mpaka 97 kwa maana hiyo kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi iliahidi kufanya haya na imeanza na inafanya haya. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nasema kwanza kabisa ni nzuri, inaanza kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ahadi ambayo chama hiki kimetoa kwa wananchi, ahadi ni deni na hili deni tunaanza kulitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, imeshirikisha au imechagua vipaumbele ambavyo nimevitaja, vipaumbele vichache, vipaumbele vitano na mwaka jana ilikuwa vipaumbele 13. Tatu, ni kwamba Tume ya Mipango imefanya kazi kwa karibu sana kipindi hiki na Wizara ya Fedha baada ya uchambuzi mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, Bajeti hii kwa kweli ni ya matumaini makubwa sana, binadamu siku zote lazima aishi kwa matumaini, na Bajeti hii kwa kweli kabisa tukiwa wa kweli tunasema ni Bajeti ya kutoa matumaini. *(Makofi)*

Tano, ni Bajeti ambayo inaibua fursa zaidi na kuweka mazingira ya uwezeshaji na pia mazingira ya uwekezaji. Mwisho, inahusika na changamoto zilizokuwepo siyo tu Kimataifa lakini pia changamoto ambazo zilizokuwepo Kitaifa, Tanzania siyo kisiwa, Tanzania ni sehemu ya ulimwengu kwa hiyo inaangalia changamoto zilizokuwa za Tanzania lakini changamoto zingine ambazo zitapanua na kufungua Tanzania na nchi nyingine mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mafanikio yake na lazima tuseme yaende sambamba nafikiri mimi kuna mambo matatu; kwanza ni utekelezaji kwa haya yote katika kipindi hiki; pili, ni ufuatiliaji, jambo ambalo pia nafikiri lina umuhimu mkubwa sana na nidhamu katika kazi, nidhamu katika matumizi kuna mambo mengi ambayo

yamezungumzwa lakini yanahitaji kwa kweli nidhamu na nafikiri kwamba ukichukua *equation* ya mambo haya matatu unapata *is equally to* mafanikio ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie baadhi tu ya vipengele vilivyomo katika Bajeti hii, kwanza miundombinu hasa hasa ya barabara, reli, bandari na anga ambayo nasema kwamba itaifungua nchi yetu na itafungua nchi yetu ikipakana na nchi mbalimbali za jirani, nchi yetu inapakana na nchi nyingi na hata biashara, ukichukua biashara ya bandari, biashara ya *transit cargo* kwa mfano zinazopita nchini kwetu kwenda nchi nyingine hizi ni fedha nyingi sana ambazo zinaweza kupatikana na kwa maana hiyo kuweza kuinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwamba uwekezaji imara ni ule ambao unavuka nchi, ni *cross border*, kwa sababu hata mwaka huu tu nafikiri kama miezi miwili iliyopita kulifanyika mkutano kule Istanbul wa nchi maskini kuliko zote, Tanzania ikishiriki kama nchi mojawapo ya *LDCs,* na suala mojawapo ambalo lilizungumzwa ni suala zima la uwekezaji katika *cross boundary* hasa hasa uwekezaji katika suala zima la miundombinu, kwa maana miundombinu ya barabara, reli na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia na labda niseme kwa hili la miundombinu hasa ukizungumzia suala la ndege, tunaona kwamba wenzetu ambao wenye ndege wenyewe na ukiangalia suala la utalii sehemu kubwa ya fedha za watalii zinabaki katika nchi zile ambazo zina ndege, kwa mfano *Kenya Airways*, *KLM* na kadhalika. Asilimia 60 ya fedha ambazo anatumia mtalii, asilimia 60 ni tiketi ambayo mtalii anakata, kwa maana hiyo ni kwamba tayari tunapoanza asilimia 60 Tanzania inakuwa haiipati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia tena bei ya mafuta na petroli, nitoe pongezi kubwa sana kwa Serikali na kwa Waziri wa Fedha na timu yake kwa kutoongeza bei ya petroli, kwanza haijaongezwa japokuwa dunia nzima bei ya petroli imekuwa ikipanda hasa kwenye vituo vya mafuta. Waziri wa Fedha ameeleza kuwa kuna kodi nyingi sana katika kila lita ya petroli nafikiri amesema kodi kama 21 ambazo zilizokuwepo na akasema kwamba mafuta yataagizwa kwa pamoja.

Lakini pili ni kwamba tozo, baadhi ya tozo hizi zitaondolewa, bado hatujui ni tozo gani na kwa kiasi gani kodi hii itapungua. Lakini ningependa kutoa tahadhari moja kwamba pamoja na kuangalia tozo hizi mbalimbali, kodi ambazo zinatozwa kwa mfano na *EWURA, SUMATRA, TBS* na kadhalika. Tozo ile ya *road toll*, naomba tozo ile ya *road toll* ibaki pale pale, tozo ya *road toll* nafikiri ni kama shilingi 200 katika kila lita ya mafuta na tozo hii iliwekwa kutokea Serikali ya Awamu ya Tatu na ikaendelezwa na Awamu ya Nne na ni tozo hii ndiyo ambayo imesadia sana kujenga barabara zetu kwa pesa zetu wenyewe. Kwa hiyo ni muhimu wakati tutaangalia kwa kweli tozo hii naomba Mheshimiwa Mwenyekiti, liangaliwe kwamba isiondolewe suala hili la tozo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia suala la kilimo na umwagiliaji, na hapa nasema kwamba katika umwagiliaji na katika kilimo kuna *program* ile *Agricultural Sector Development Program (ASDP)* ambayo pamoja na mambo mengine

inazungumzia kuongeza thamani ya bidhaa pamoja na umwagiliaji na nafikiri kwamba hii ndiyo sekta hasa hasa ukizungumzia umwagiliaji, kwa sababu unapozungumzia umwagiliaji unakuwa una uhakika wa kilimo, ama sivyo unakuwa huna uhakika kwa sababu ya kutegemea mvua. Lakini nafikiri ni sekta hii ndiyo ambayo itaweza kumeza pia vijana wengi katika ajira lakini lazima iwe inavutia, haiwezekani kwamba kijana ukamwambia akalime na kulima kwa jembe la mkono ukategemea kwamba atakwenda kijijini kulima. Kwa hiyo, vyovyote vile kuna haja ya kubadilisha kama vile ambavyo imependekezwa.

Napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa kufungua dirisha la mikopo kwa wakulima pale *TIB* na kila Bajeti kuweza kuwaongezea hii ilikuwa ahadi ya Waziri wa Fedha na kwa kweli ahadi ameweza kuitimiza kwamba kwa mwaka huu zimepelekwa shilingi bilioni 50 na kwa dirisha lile la kilimo zimepelekwa shilingi bilioni 20 na mpaka sasa hivi kuzifanya ziwe shilingi bilioni 42, kwa hiyo, natoa pongeza kwa Waziri wa Fedha na kwa maana hiyo kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo wasiwasi wangu ni kwenye Bajeti ya kilimo na umwagiliaji ambayo imepata ongezeko la asilimia 2.5, sote tunajua kwamba miundombinu ya umwagiliaji ina gharama kubwa sana, sasa sina uhakika na najua kwamba kupanga ni kuchagua na najua kwamba kuna suala la rasilimali lakini sijui tutafanya nini kuhakikisha jambo hili linafanyika. Kwa sababu suala la chakula ni suala muhimu sana. Tunajua kwamba mfumuko wa bei kwa sehemu kubwa sana unatokana pia na chakula asilimia karibu 47 ya mfumuko wa bei ni kwenye mfuko ule wa chakula. Kwa hiyo, jambo hili kwa kweli likizingatiwa hata mfumuko wa bei utaweza kuondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia juu ya mikopo ya Serikali, nazungumzia hapa zaidi mikopo ya ndani, siyo mikopo ile ya nje na kama walipozungumza Wabunge wengine kwamba mikopo ya nje inapochukuliwa basi itumike zaidi kwa ajili ya maendeleo na siyo kwa ajili ya vitu vingine. Sasa mikopo ya ndani na hasa kama tunapozungumzia kushirikisha sekta binafsi sasa unakuta kwa pale ambapo Serikali inakopa kutoka mabenki ya ndani na wakati huo huo inataka kuimarisha sekta binafsi inaleta tatizo la msongamano au tatizo la *crowding*, kwa sababu Serikali na sekta binafsi inakwenda kwenye *source* hiyo hiyo na kinachotokea mara nyingi sana ni kupanda kwa ukubwa kwa riba na pia kupunguza uwekezaji katika sekta binafsi. Unaweza kuona kwamba kwenye kitabu cha *Tanzania Five year Development Plan 2011/2015* ukurasa wa 14, ukurasa wa 14 inaonyesha jinsi gani ambapo sekta binafsi iliweza kukopa kwenye mabenki lakini baada ya hapo imepungua kwa mfano mwaka 2005 sekta binafsi ilikopa asilimia 30, mwaka 2006 ikakopa asilimia 40 kwa hiyo, ikaongezeka wakati ule ilikuwa Serikali haikopi sana kwenye soko la ndani. Mwaka 2007 ikapanda zaidi ikawa asilimia 43, mwaka 2008 ikawa asilimia 45 lakini mwaka 2009 ilishuka iliteremka kufikia 9.6, mwaka 2010 imepanda kidogo kufikia asilimia 20.

Kwa hiyo, je, swali ni kwamba kushuka huku kunatokana na msongamano, msongamano kwa maana ya *crowding* ya mkopo ambayo inafanywa na Serikali au vipi

na je, athari yake kwa uwekezaji wa ndani utakuwa namna gani? Mheshimiwa Waziri wa Fedha labda pengine anaweza kutueleza baadaye juu ya jambo hili. *(Makofi)*

Mimi ningefikiria kwamba tungetilia mkazo sana sasa hivi juu ya mikopo ile ya *sovereign bond* na mchakato huu ulianza miaka kadhaa, mwaka 2005 lakini sasa uchumi umeimarika zaidi na kwa maana hiyo una nafasi zaidi kubwa ya kuweza kupata mikopo hiyo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge muda wako umekwisha.

**MHE. ZAKIA H. MEGHJI:** Mheshimiwa Mwenykiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia hautoshi mchangiaji yoyote kuchangia maana ni chini ya dakika kumi, kwa hiyo, sidhani kama kuna yeyote anaweza kukubali kuchangia. Kwa kesho asubuhi saa tatu tutaanza na maswali na baadaye baada ya maswali wachangiaji watakaofuatia na watakaoanza watakuwa Mheshimiwa Dunstan Kitandula, baadaye Mheshimiwa Ali Khamis Seif na Mheshimiwa Kisyeri Chambiri, na wengine wataendelea.

Wakati mjadala unaendelea, niliombwa Mwongozo na mara zote katika Bunge linapotokea suala la Mwongozo na suala linalohusu Kanuni basi suala hilo linakuwa ni *paramount*, kwa hiyo, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa alipokuwa anaongea Mheshimiwa Tundu Lissu aliomba Mwongozo kutumia kifungu cha 151 na nilitoa Mwongozo lakini kwa kuwa tunataka ufahamu zaidi wa Kanuni na kama tunavyokubaliana kwamba wengi ni wageni basi ni vizuri nikakisoma ili muone Mwongozo wangu nilioutoa ulivyokuwa, kinasema hivi; “ Endapo litatokea jambo lolote ambalo mhusika wake au muathirika wa jambo hilo anastahili kupewa pongezi au pole na Wabunge basi Spika atatoa pongezi au pole kwa mhusika au muathirika wa jambo hilo kwa niaba ya Wabunge wote.”

Lakini cha pili kinasema; “Baada ya Spika kutoa pongezi au pole kwa mhusika au kwa muathirika wa jambo lolote kwa ajili ya kuokoa muda wa majadiliano, Mbunge yeyote hatoruhusiwa kutoa pongezi au pole kwa mhusika au muathirika wa jambo hilo wakati wowote wa majadiliano Bungeni.”

Na cha tatu kinaendele kwa upande wa Serikali, sasa tafsiri ya kifungu hiki ni kwa jambo ambalo limemgusa pengine Mbunge mwenzetu kubwa kama msiba au jambo la pongezi ni kwa jambo kubwa ambalo pengine mtu amekuwa amepata cheo, amekuwa *promoted*. Lakini pia kwa majanga makubwa kwa mfano umetokea msiba ulio-*involve* watu wengi, hatuwezi tukakaa hapa wanasiasa tusiseme chochote. Kwa hiyo, Spika anaweza akafanya hivyo kwa niaba yetu sote. Kwa hiyo, kwa Mheshimiwa Mwambalaswa kwa kuwapongeza watu wa Kata zake, Jimbo lake la Lupa, lile ni jambo lake na Spika hajawahi kufanya hivyo kwa niaba yake. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwambalaswa alikuwa sahihi, aliyosema tunaendelea kujifunza, Kanuni hizi huwezi kuzizoea, wote hatuzijui tunaendelea kujifunza kila siku, lakini naamini tujitahidi mara zote kusaidia muda wa Bunge usipotee bure. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna mtu alidondosha *modem* hii nafikiri nyeupe kama yupo basi ataonana na Makatibu hapa wataweza kumpatia. Basi kwa kuwa muda wetu umekwisha na wachangiaji waliochangia ndiyo hao, nichukue nafasi kuliahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.41 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi,*
*Tarehe 16 Juni, 2011 saa tatu asubuhi)*